# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

# CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MAGARINI CONSTITUENCY HELD AT MARAFA PRIMARY SCHOOL

ON

## Friday 3rd May 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MAGARINI CONSTITUENCY**

**FRIDAY, MAY 3, 2002 AT MARAFA PRIMARY SCHOOL**

**Present:**

Com. Abida Ali Aroni (Chairlady)
Com. Riunga Kaiji
Com. Abdirizak A. Nunow

**Secretariat Staff in Attendance:**

John Watibini - Programme Officer
Hilda Mikaga - Asst. Programme Officer
Gladys Osimbo - Verbatim Reporter
Rose Samba - Sign Language Interpreter

Mkutano uliaza saa tatu 9.45 a.m na Com. Abida Ali in chair.

**Com. Abida:** Ningependa kuwashukuru kwa kufika, na tungeomba kama kuna mtu atajitokeza ili kutuanzishia mkutano wetu kwa sala, halafu tuendelee; a volunteer, Bwana Chief, sijui kama ungetuombea.

**Chief**: Na tuombe. Baba katika jina la Yesu tunakushukuru, tunaliinua jina lako. Mungu mwenyezi ambaye hujabadilika tunakushukuru kwa ajili ya wakati na majira ambayo umepata kutufikisha. Tazama Baba tumetarajia siku ya leo kwa hamu, na Mungu umepata kukubali Bwana. Umepata kutuleta katika mahali hapa, hata na wageni wetu ambao tumepata kuwatarajia wamepata kufika, wakiwa Bwana wamesafiri katika hali ya usalama. Tunakushukuru Baba tunapoanza shughuli ya leo, tunaiweka mikononi mwako, Baba umesema kila jambo upate kuhusishwa ili ukapate kuongoza. Naamini Bwana umepata kusikia, na Bwana utafanya sawa na mapenzi yako. Ni katika jina la Yesu tumeomba na kuamini. Amen.

**Com. Abida:** Ahsante, kwa kuanzia. Tutawajulisha wanatume, pamoja na timu ambayo tuko nayo hapa, halafu tutafuata utaratibu kulingana na vile ambavyo mmejiandikisha. Tutawapa dakika kumi, kwa watu ambao wana oral submission, na ambao wameandika, tutawapa dakika tano tu kujaribu kusummarise, kwa sababu baadaye tutapata nafasi ya kusoma hizo nakala amabzo mtakuwa mmewasilisha kwa tume. Na kwa kuanzia, kwa upande wangu wa kushoto, ni Commissioner Dr. Abdirizak Nunow, halafu upande wangu wa kulia, ni Commissioner Bwana Riunga Raiji.

**Com. Riunga**: Hamjambo?

**Com. Abida**: Na mimi naitwa Abida Ali Aroni, na nitawajulisha wenzetu ambao tumefwatana nao wakati huu. Tuna Bwana John Watibini, ambaye ni Programme Officer katika tume.

**Watibini**: Hamjambo?

**Com. Abida**: Tuna, Hilda Miringa, Tuna Gladys Osimbo, na Rose Samba. Halafu nitamjulisha Bwana Kingi, ambaye ni Co-ordinator wa sehemu hii, na pengine ikiwa kuna watu wowote kutoka katika kamati ya constituency, mngetujulisha ni akina nani ambao wako hapa.

**JafaKingi**: Hamjambo? Katika sehemu hii tuna wanakamati wetu ambao wanatuakilisha katika tarafa hii. Mwanzo kabisa tuna Bwana Peter Thoya, yeye ni mwana kamati. Tuna Loise Kashuto pale, yeye ni mwana kamati, na tuna Shadrack Charo yeye ni mwana kamati. Bado tunangoja James Kerimo ambaye ataingia, yeye ni mwana kamati, anatuwakilisha upande wa Adu.

**Com. Abida**: Sasa utaratibu mwingine ambao tunafuata ni kwamba ikiwa kuna mtu yoyote ambaye ni mlemavu, hawezi kusikia, tuna Yunis, tuna Rose Samba ambaye ataweza kufanya sign language. Kwa hivyo mtatujulisha ikiwa kuna mtu yoyote ambaye anataka usaidizi kama huo. Na baada ya kutoa maoni, mtakwenda kwenye meza hii kujiandikisha, kwa sababu karatasi ambaye iko hapa, ni registration form. Lakini pengine kuna watu ambao wamejiandikisha lakini hawana maoni. Kwa hivyo tuna register rasmi ambacho ni kitabu. Baada ya kuzungumza, itakubidi uende pale na kutoa maelezo yako, ili iende katika data center ya tume; kuhakikisha kwamba kila mtu atakaye kuwa amezungumza, maoni yake yameweza kuandikwa. Na tutaanza na Bwana Nzovu K. Ahmed. Bwana Nzovu, tafathali njoo hapa mbele, toa maoni yako, tutakupatia dakika kumi. Na uwanze na jina lako kwa sababu tuna record.

**Bwana Nzovu**: Mimi kwa jina naitwa Nzovu Kalama Ahmed. Natoka katika Tarafa ya Tarasha.

**Com. Abida**: Endelea.

**Nzovu**: Katika Katiba ya Kenya, kutokana na maoni yangu, ningependa sheria ya kutokuwa na imani na kiongozi yoyote ambaye anawakilisha raia, iwe iko; kura ya turufu. Kama vile diwani, awe akichaguliwa baada ya muda fulani, ikiwa hafai, aweze kuondolewa na kura ya turufu. Au, bunge akiwa hafai, aweze kuondolewa na kura ya turufu.

Na ningependa kwa maoni yangu, viongozi wa raia, kama vile machifu na manaibu wao, wawe wanaweza kuchaguliwa na raia, kwa sababu viongozi hawa wameharibu sana mambo ya wananchi. Wana viongozi wao ambao waliwachagua kama vile, wazee wa vijiji. Haswa hawa wazee wa vijiji wanadhulumu sana raia.

Katika Katiba ya Kenya ya wakati huu, nataka uuzaji wa ardhi kwa wageni kama vile Waitaliani, Wahindi, au wageni wengine ambao sio wa Kenya, ipigwe marufuku; kwa sababu raia wengi wa Kenya wamepokonywa ardhi zao, na wakafukuzwa, na wakawa ma-squatter. Kwa hivyo hii sheria ya kuuza ardhi kwa wageni ambao siyo Wakenya ikikatazwa, raia wa Kenya wataishi maisha mazuri. Na vile vile ikiwa nchi ya Kenya itaendelea kuuzwa, vizazi vijavyo vitakosa ardhi ya kuishi kwa sababu, ardhi yote itakuwa imeuziwa wageni, na Kenya itabaki kama koloni.

Katiba ya Kenya ambaye inakuja, iwalinde sana kina mama, maanake akina mama huonewa sana. Akina mama mtu huolewa akazaa hata kama ni watoto ishirini, lakini siku akikosana na bwana yake hufukuzwa na akaondoka bila kitu. Hatapatiwa angalo chochote, kule atakuwa amezeeka, hana kitu cha kufanya, maanake yeye ni mzee, amezaa na amekosana na bwana akafukuzwa akaenda kwao. Lakini ningependa Katiba ya Kenya, wakina mama kama hao wawe wanalindwa. Wakati ule wanakosana na bwana yake, na yeye amemzalia watoto, akimfukuza awe anaweza kumlipa ridhaa, ili aweze kuishi kwao kwa kumaliza maisha yake.

Katiba ya Kenya ya wakati ujao, tungependa Kenya iwe na vyama vya siasa kama vitano peke yake; kwa sababu vyama vingi zaidi ya kumi ama ishirini, vingine huwa vinapoteza raia tu. Lakini vingekuwa kama vyama vitano hivi, vingekuwa na nguvu ya kusema ukweli, au kusaidia raia sawasawa. Kwa mfano kuna vyama vingine vinafika sehemu ya kuambia raia kuwa wasijenge mashule, kwa sababu chama fulani kimeongoza, kwa hivyo hatuna haja na chama fulani. Lakini vikiwa vyama vichache na vina nguvu, vinaweza kusaidia kila aina ya maendeleo ya Wakenya.

Katika Katiba ya Kenya, tungependa viongozi, kama vile Chief Kadhi au Kadhi, awe anafanya kuchaguliwa na serikali, ili kupunguza lile tatizo la kuwa hawajulikani wanachaguliwa na akina nani, ili anapokosa serikali iwe inaweza kumuondoa na kumchagua mwingine. Huo ndio mwisho wa maoni yangu.

**Com. Abida**: Asante, jiandikishe pale, na ikiwa una nakala unaweza kupeana hapo mwisho pia. Margret Jefa?

**Margret**: Kwa majina naitwa Margret Jefa, ninasimamia Shirika la N.C.S.W., na nitazungumza maoni yangu. Utangulizi; katika Katiba hii yetu ya Kenya ambayo tuko nayo sasa, haina utangulizi, na tungehitaji, au ningetaka iwe na utangulizi ambao utataja jinsi tulivyopata uhuru kutokana kwa wakoloni. Itaje walio mwaga damu, na walio teseka, mpaka tukapata uhuru Kenya, kama Hayati Jomo Kenyatta. Pia itaje jinsi tutakavyopigana na kutojua kusoma na kuandika, na pia kuangalia afya zetu, na kuondoa umaskini.

Uraia: mtu yoyote wa kuzaliwa Kenya, awa raia moja kwa moja. Utoaji wa uraia, ufuate ule wa kupewa kitambulisho, vinavyo onyesha, kabila lako, na mtaa uliotoka, tarafa na wilaya. Waume au wake wanao olewa hapa Kenya, watambuliwe kuwa ni raia bila jinsi visia zozote.Mtoto anayezaliwa ni mzazi mmoja, huyo atangulie kuwa raia moja kwa moja. Majukumu ya raia;

kwanza awe na makao, awe amejiandikisha, na ana kitambulisho cha Kenya. Pia aweze kuipenda nchi yake na kuitumikia, ili aweze kuonyesha uzalendo wake. Pia ajue kuitetea nchi yake.

Ulinzi na usalama: Rais awe Amri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Silaha. Katiba na iruhusu uwezo wa kipekee, katika hali ya hatari yoyote, kwa usalama wa nchi.

Vyama vya kisiasa: Katiba ielekeze uundaji, uongozi, na tabia ya vyama vya kisiasa. Idadi ya vyama iwe maalum, hii itaonyesha mwelekeo kwa wananchi, na visizidi vyama vitano. Kila chama na kijigharamie kifedha, sio pesa za uma.

Miundo, na aina ya serikali. Mimi naunga mkono serikali ya majimbo, amabayo mamlaka ya nchi yamegawanywa baina ya serikali kuu na majimbo. Hii itawezesha utawala uwe karibu na wananchi. Kila jimbo litaweza kutumia raslimali zake kwa kuendesha miradi ya maendeleo bila maonevu. Pia itapeana nafasi za kazi kwa vijana.

Bunge: tuendelee kuwa na dhana ya wabunge wa kuteuliwa. Mabadiliko ambayo tunayataka, nafasi hizo za wateule, ziwachiwe wanawake, walemavu na vijana; kwa sababu hao ndio ambao si wengi bungeni. Tukiangalia kama bunge letu ambalo tuko nalo sasa lina wabunge mia mbili ishirini na wawili, wanawake tisa peke yao ndio wako katika hilo bunge. Ni hao tisa ni wanne ndio wamechaguliwa, watano ni wale wamefanya kuteuliwa. Halafu kuna wabunge saba ambao wameteuliwa wanaume. Sasa hii ni kuonyesha hiyo demokrasi haikufwanywa; wanawake ndio wachache tena wanateuliwa wengi wanaume. Kwa nini? Kwa hivyo ikiwa ni lazima tuwe na sehemu hizi za kuteuwa, basi wateuliwe wakina mama, manake ndiye wachache kwa bunge, ndiyo nambari yao iweze kufikiana na ya wazee. Bungeni kuwe na hatua maalum za kuongeza wanawake. Kutengwe viti maalumu kwa kila District, hiyo ndiyo itakayonyesha demokrasi. Rais akichaguliwa mwanaume Vice awe mwanamke. Marupurupu na mishahara ya ……

**Com. Abida**: Songea kidogo karibu na microphone.

**Margret**: wabunge, hii inapaswa kuchunguzwa vizuri. Kwa hali ya uchumi wa hapa Kenya, kuna wengine ambao wanatatizika sana upande wa mishahara; lakini tunapata wabunge wanajiongezea kila wakati, na hivyo wamejiongezea pesa nyingi na bado wanahitaji kuongezea. Ukiangalia upande wa madiwani, hawaongezwi chochote, wako pale pale, na hao ndiyo wanakaa na wananchi huko chini. Kwa hivyo hapo hao wabunge kule kujiongezea kusiwe hivyo. Tungeomba pengine Katiba hii iweke kiwango maalum cha wabunge, lakini sio kila siku kujiongezea, na ikiongeza, basi iongeze hata kwa zile wizara nyingine. Tuko na watu muhimu sana, ambao hata hao wabunge wanawategemea, kama madaktari, kama walimu, lakini tunaona hao wote wako chini, ni wao tu wanapanda kila siku. Kazi ya bunge inapasa abaki na siku maalum na masaa siyo kila siku, sababu yeye amechaguliwa na wananchi. Akiwa atabaki huko Nairobi, kwa kuwa yako bunge, muda huu wote wananchi wake atawaona saa ngapi? Kwa hivyo bunge, awe na masaa maalum yakubaki kule, na masaa mengi aje asikize wanachi, ili alete ya wananchi huko; maana yake sisi tumewatuma: siyo hao wakae huko wakijiropokea mambo yao ni waje huku kwetu tuwatume.

Mahakama nyingi zimeingiliwa na ufisadi. Haki za watu wengi zimeangamia. Katiba itilie manani maswala ya mahakama, manake wananchi sote, tumetegemea mambo kama hayo. Ikuwa kuna matatizo tunajua utaenda kwa mahakama. Na ikiwa mahakama hayo haiangalii mtu na shida zake, bali yanaangalia mtu mwenye pesa, basi watu wengi wanapata shida. Kwa hivyo kuwe na mahakama ambayo yatakuwa thabiti ambayo yatakuwa yakiendelea kwa kuangalia sehemu zote, sio kupendelea watu. Hiyo ndiyo sisi tutakuwa tumepata kimbilio. Kuwe na mahakama maalum itakayo ongoza kesi za wakina mama, kama zile za kunajisiwa, au mambo mengine ya kinyumbani, iwe inaweza kuangalia vizuri; maanake kuna mambo mengine ni ya siri. Ikiwa itakuwa ni pale kuwekwa mahali ambako pako wazi, saa nyingine mambo mengine yanashinda kutamkwa, kwa hivyo kufanywe mahali ambapo kutakuwa kwa siri kidogo, ambapo kila mtu anaweza kuzungumzia yale ambayo ako naye.

Makundi yanayoweza kudhuriwa; nikiwa mimi niko katika kundi moja la wale ambaye wanadhuriwa, ambalo tunatambua kama kundi la akina mama, kundi la walemavu, na hata kundi la vijana, haya ni makudi maalum ambayo hapa Kenya yako mstari wa mbele kudhuriwa, au kudhurika. Hii Katiba tuliyo nayo, haiyangalii maswala ya akina mama, imeachia mila na desturi, ndizo zinazo wagandamiza wakina mama. Tunataka Katiba hii iyondoe mila na desturi mbaya, zinazo wafanya wakina mama kuwa watumwa.

Kitu ambacho nimekiona katika huku kugandamizwa sisi wakina mama.Kitu cha kwanza ni kulipiwa mahari. Msichana anapozaliwa, hata kuna majina ambayo anabatizwa, anaweza kuitwa mali, anaweza kuitwa huyu ni kahunda, yani kumaanisha kabisa yeye amezaliwa kama kitu cha biashara kwenye hiyo jamii. Kwa hivyo mama yoyote, hatambuliki kama kitu cha maana, anachukuliwa kama ni kitu ambacho kinaweza kuuzwa kama mbuzi, kama kuku, na hayo yote yamechangiwa na huku kulipiwa mali. Sisi tunaita mali wenzetu wanaita mahari, lakini ni vimoja. Sasa ikiwa itakuwa hivyo, mimi maoni yangu ningesema hii mali iyondolewa, ili kila mmoja aweze kuwa huru; ikiwa tunahitaji kweli uhuru na demokrasi katika Kenya yetu. Msichana anapo pendana na mvulana, kuwe kuna cheti maalum ambacho hicho ni cha kuwaunganisha. Kama jamii hii yetu, sisi watu wa huku Marafa, utakuta msichana amependana na mvulana ameolewa, hata pengine amezaa; halafu utakuta babake anaenda kumchukua yule msichana wake, kwakua anasema hajapewa mali. Sasa ni kama kuwatesa wale watoto, anatatiza yale mapenzi yao kwa sababu yeye ni lazima alipwe mali. Kitu kama hiki kimechangia utumwa sana. Kwa hivyo ningehitaji, Katiba hii yetu, iangaliye haki hizi za wanawake.

Mwanamke pia anapowachana na bwanake, kama mwenzangu aliyekuwa hapo amesema, hilo jambo, mtu anaolewa pengine mnaenda kukaa miaka ishirini, ni jenge nyumba, ninunue mali pamoja na wewe, ni lime, ni pande, tuwe na rasimali nyingi sana katika mji.Lakini mama mimi hata ninavyo zeeka hivi ni kirudi kwetu, zile elfu mbili babangu alizochukua kutoka kwa yule bwana, ni zirudi zote, zile mali ambazo mimi nimechuma na huyo bwana siwezi kupata, hata mtoto mwenyewe sitapata. Mtoto wangu niliemzaa, sina haki naye. Mali yangu hata kama nimenunua mbuzi, pengine bwana amekuwa tu mlevi, hakununua chochote, mali zote nimemwachia, yeye ndiye tajiri mimi nabaki maskini.Kwa hivyo, hapa kwa mali kuangaliwe. Mali zigawanywe sawasawa, ikiwa kumetokea shida yoyote. Nikiondoka, watoto wangu niondoke nao wakiwa ni wadogo. Niende

nikawalee kwa njia nzuri, na baba yao akiwa amesimama pale akileta chakula kwa watoto wake sio anisukumie mimi tu, yeye abaki. Tumewalete sote duniani. Kwa hivyo mimi huduma yangu itakuwa ni kuwalinda wale watoto, ikiwa ni kuwapikia, kuwaosha, kuwafanyia kila kitu. Lakini pesa zile za kugaramia, baba alete, mpaka watoto watakapo jiamulia wenyewe. Hiyo iwe hivyo na mali tuzigawanye sawasawa. Ikiwa ni ngombe wawili nichukue wangu moja, na yeye abaki na wake. Nyumba peke yake ndio sitakupokonya, lakini ikiwa kuna mali nyingine, nipate nikajenge nyumba kule ninakoenda.

Haya, na hapa mahali kwa urithi, mama kusema ukweli harithi chochote, na haya mambo haya yote, yako kwa zile tabia zetu, yaani desturi na mila. Mila zetu nyingi zimekuwa za kugandamiza wanawake, sio mila za kulinda kila mmoja. Mila nyingi huku kwetu ni za kugandamiza wakina mama. Utakuta hali ya urithi, kwa mfano, bahati mbaya imeniinglia bwanangu ameniacha. Mali zile zote nitapokonywa na ndugu ya bwana. Kwanza nitarithiwa mimi, na hiyo ndiyo njama yao wameiweka; saa ile wananidanganya wanirithi, wanaitaka ile mali. Kwa hivyo nitaanza kurithiwa mimi haijalishi bwanangu amekufa na ukimwi, haijalishi bwanangu amekufa kwa ugonjwa gani. Lakini ni lazima nitarithiwa kwa kuwa nimeonekana niko na mali. Baada ya muda kidogo ninaachwa na watoto. Mali yote anachukua, kwa kuwa anasema ni mali yao. Kwa hivyo mambo ya urithi baba akiondoka ulimwenguni, mali iwachiwe mama. Mama akiondoka ulimwenguni, mali ibaki na bwana na watoto.Hiyo ndio itakuwa ni sawa, na hiyo ichunguzwe vizuri na Katiba. Hizo ni zile mila ambazo zinatuharibia kabisa sisi wakina mama.

Mama huyu pia, kwa bwana amekosa urithi, murudishe kule kwao alikotoka. Babake hata akiwa ni tajiri wa aina gani, hahesabiwi msichana yoyote kuwa anaweza kurithi mali ya babake. Hata ikigawanywa, akiwa yeye ndiye mtoto wa kwanza mkubwa yeye yuko inje tayari. Ni vijana peke yao ndio wanaotambuliwa katika urithi huko kwetu, na hao ndio watarithi. Kwa hivyo huyu mama, Katiba na imshugulikie, isituwachie tukagandamizwa na hizi mila zetu. Mama naye ataje fungu, kama baba yake anagawanywa mali, haijalishi amekufa, haijalishi ako hai. Lakini akiwa anagawanyia mali watoto wake, mimi pia kama Pazo nami, nirithi mali ya babangu, maanake niko na haki.

Haya, ufwa. Mambo ya ufwa ni ile sheria ya mwanamke akifiliwa aolewe, hiyo nishaitaja. Hiyo ni desturi mbaya, na iondolewa kabisa, na iwe sheria hii haiko. Sio sawa mawanamke kurithiwa na ndugu ya bwanake anapofiliwa. Mila hizi utazipata sana kwa Wajaluo au kwa wa Giriama, Mijikenda, hawa ndio wenye mila hizi za kuchukuana ufwa. Na hizi ni mila ambazo zimepoteza watu wengi sana manake siku hizi sio kuzuri, sio kama zamani, kuna mambo mengi ya hatari sasa mtu akionekana bado anaonekana yuko vizuri, vizuri, wanafikiri ni mzuri, kumbe ana shida; halafu anachukua mji mzima anaumaliza. Maanake unaoelewa na bwana huyu akifa, yule mwingine, hata anaweza kuolewa na mtoto ambaye amezaliwa pale pale ukimwangalia, wambiwa lazima uolewe na huyu ukitaka kuishi hapa. Kwa hivyo hayo yaondolewe.

Mambo mengine ambayo yanayo gandamiza wakina mama, ni kama huku kupasha tohara. Upashaji tohara uko sehemu nyingi sana na hizi ni desturi za watu fulani, na ni mila za watu fulani. Lakini ni mila mbaya sana. Hizi si kwa manufaa ya yule mama, lakini ni kwa manufaa ya wale wazee, wakina baba. Mila hii ya kugandamiza akina mama, pia kokote ilipo Kenya hii, iondolewe, maanake imechangia hata maafa kwa wasichana wetu.

Haki za watoto, wasichana kama nilivyowaelezea hapo mwanzoni, wasichana wamechukuliwa kama biashara; na kwa vile ni biashara hao wasichana, utakuta mtoto wa miaka sita anaweza kutafutiwa bwana mzee wa miaka sabini, aolewe. Na saa ingine wanatolewa hata huko mashule ili wakapewe hawa waume, watu wachukuwe mali. Ndiyo mimi nimesama mali iondolewe ndiyo inatuharibia kabisa. Watu kama hawa, kuwe na sheria, na ikiwa ni kifungo, basi kifungo hicho na kiwekwe kiwe uniform. Sio leo huyu anaenda kufungwa siku mbili, yule anaenda kufagia kwa chifu, yule anaenda kufanya hivi, wanatolewa. Hapana . Iwe sheria kabisa hapa Kenya. Mtu akipatikana na kosa kama hili, kifungo hicho kisipungue miaka mitano, afungwe huko jela. Huyu wakuchukua mtoto mdogo kupatia mume. Hizi ziko katika mambo ya ndoa zile za kulazimisha.

Haya, shida nyingine ambayo tuko nayo huku kwetu, msichana au mvulana ampenda fulani, lakini baba ana amri ya kusema mpaka mimi nichague. Yani wananyimwa haki zao watoto; anasema mpaka yeye amchagulie kama ni bibi wa kuoa yeye ndiye anajua bibi mzuri, kana msichana mzuri yeye ndiye anayemjua. Lakini hayo mapenzi nafikiri hachaguliwi namna hiyo. Kwa hivyo saa ingine wanaleta shida, wanasumbua watoto. Kwa hivyo watoto wawekwe huru nao, ili waweze kujiamulia mambo yao.

Kuna tabia nyingine mbaya inayoendelea, ya wazee wetu, yaani mababa, wananyemelea binti zetu, kufanya mapenzi nao. Hiki ni kitu ambacho kimeendelea sana na tunakijua. Baba anaacha mtoto, anaacha mama, anafuata mtoto, na hili ni jambo la kuhuzunisha, ambalo hata mtu akishtakiwa, unaona kosa hilo lina chukuliwa kihafifu sana; halionekani kama ni kosa kubwa, manake yule utakae mkuta pale mwenye kuhukumu pengine ni mwanaume. Yule ambaye atakusikiza hiyo kesi kwanza utaanza na Chifu. Chifu hataichukulia uzito manake yeye pia huyu ni mume mwenzake. Anakusukuma tu, ukienda huko mbele unapambana na wanaume, hivyo hivyo. Sasa mwisho unakuta yule msichana anabaki na kuteseka. Sasa hili ni teso ambalo limetukumba sisi wazazi, na watoto wetu wakike. Kwa hivyo sisi wakina mama tupate nafasi nzuri na sisi. Baba anaponyemelea msichana wangu, basi nikimleta, hiyo sheria, iwe imewekwa ni sheria ya kila mtu. Sio sheria ya huyu mume wangu leo nimuone, kesho yule anastarehe pale; na mtoto wangu ako hapa. Hi inatuletea shida sana, maanake hata watu wengine ambayo ni viongozi, ambaye ni wafanyi kazi wa serikali wananyemelea hawa wasichana wao. Tuko na kesi ambayo huyo mtu yuko huru kabisa, na ni mfanyi kazi mkubwa wa serikali. Lakini amenyemelea mtoto, tena mtoto amepimwa ameonekana ako HIV positive, na baba anafanya kazi. Hi ni namna gani? Kwa hivyo tafadhalini, nyinyi ambayo mumechukua maoni, msiache maoni, hata mukiona ni maoni ya kipuzi, kipuzi yachukueni hivyo hivyo, tena mkayazungumze kwa nguvu, ili yandikwe vizuri kwa hiyo Katiba. Wazazi kama hawa wanahitaji kuhukumiwa kifo; Maanake hawana maana kabisa katika jamii.

Walemavu. Walemavu mara nyingi sana nao wametengwa; kama hilo kundi la kina mama. Hao wametengwa hata kijamii. Hapo nyuma, hizi jamii zetu hizi, zilikuwa ukizaa mtoto ambaye anaonekana ana kasoro, mtoto huyu ni auwawe, atupwe kabisa hafai kwa jamii, maana yake analeta aibu kwa jamii. Lakini je? Mtoto alikuandikia application umzae hivyo? Mtoto umemzaa, halafu unaenda kumua, umtupe kwa sababu ana kasoro, hakuzaliwa mtoto wa kawaida. Hizi zilikuwa ziko kwa hizo mila, lakini mimi nataka niseme hivi, mtu yoyote anayezaa mtoto mlemavu, serikali imwangalie vizuri mtoto huyu asome, achukuliwe kama wale watoto wengine. Manake ulemavu tumeona siyo ugonjwa, mtu akiwa amelemaa siyo mgonjwa, anazo kazi nyingi ambazo

anaweza kuzifanya katika jamii, anaweza kufanya kazi, hata kuinua hata serikali yetu. Manake tukisikiza huko bunge, kuna yule mama yule Sinyo ambaye hata haoni, lakini si ako huko? Na kila siku tunamskia yeye ndiye anayezungumza hata kushinda wale wabunge wenye miguu miwili na macho yao. Anawatetea wananchi. Kwa nini? Kwa hivyo hawa walemavu wa aina yoyote watambuliwe, na serikali iweke kitu maalum ambacho kitawagaramia kama fedha. Akiwa mlemavu ametoka kwa jamii maskini, basi asiwachwe akahangaikia pale, maana yake yeye ni mlemavu. Lakini kitu ambacho kinaweza kumweka kwenye maisha ya kiwawasawa, ni elimu. Kwa hivyo walemavu watengewe pesa ili wasome vizuri, na pia wapangiwe kazi ambazo wanaweza kuzifanya vizuri, waajiriwe.Sio wasome, halafu waachwe wakizunguka huku na huku. Waajiriwe kazi.

Haya. Nitaingilia mambo mengine hapo chini. Kuna haki za kimisingi, tuko na hukumu ya kifo hiyo ambao inaendelea tayari, mtu anahukumia hata kifo. Mimi ile ninavyo onelea, hukumu ya kifo ibaki hapo hapo. Kwa sababu pengine mimi ndiye nimeua mtu ninaweza kusema iyondolewe. Je mtu awe mtoto wangu, aje amchome kisu amue, nikifika kule hukumu ya kifo, haiko. Yeye mtu, siku mbili, unamwona ametolewa amekuja. Je nitafurahia? Basi itaondolewa, huko kwa serikali, lakini kule kisu na mimi niko nacho mkononi, nitamuwinda. Kwa hivyo sheria ibaki, ukiua uuwawe, hiyo ndiyo mshahara.

Kitu chengine ambacho nimekiangalia katika hizi haki za kimsingi. Serikali yetu ina misitu maalum, ambayo inayo hawa wanyama wa msituni, ina mambo mengi inayoangalia. Lakini nikiangalia sana ninaona, binadamu ameachwa kando kidogo. Yaani wanyama wa msituni kama ndovu, wako maanani zaidi, kwa serikali yetu, kushinda mwanadamu.Ni juzi tu hapa, Bridge hapa mwananmke alikatwa akatolewa matumbo na mtoto akauwawa,lakini hiyo haionekani kama ina maana. Yule mnyama basi ukamua, ukishikwa utakiona. Mimi naona basi ikiwa serikali inatambua wanyama zaidi ya binadamu; kwa nini isiweke seng’ enge katika hiyo misitu yake yote ya spaki ili wale wanyama wakabaki pale, na wananchi wakaishi kwa amani. Iangalie wananchizaidi kuliko wale wanyama.

Watu wanaostaafu. Kuna kiwango cha miaka ambacho wafanyi kazi huwa ni wastaafu. Hiyo ni vizuri kwenda kupumzika. Lakini kwa nini marupurupu yao hawapewi wakitoka wakatoka nayo? Imechangiya maafa mengi sana kwa watu wetu. Mtu anambiwa amestaafu basi hizo pesa, huko kwa serikali utazifuata, utazifuata, utazifuata, mpaka ufe na magonjwa yale ya moyo. Sheria iwe kabisa ya kuwa mtu akistaafu, asitoke bila bahasha yake pale, hata ukimwambia leo unastaafu, basi awe amepangiwa mzigo yake; atoke aende kwake. Siyo kumpitisha pitisha kama ambaye hakufanya kazi. Kwa hivyo hiyo iwe sheria kabisa. Mtu akistaafu, astaafu na vitu vyake atoke navyo, aende. Sio kumtesa, mpaka afe, awache hiyo mali, haya ifwatwe mpaka ishinde haipatikani. Hiyo ni kunyanyasa wananchi na haiyonyeshi kuwa serikali iko kwa democracy.

Kuna hiyo miaka iliyopita, serikali ilitangaza kupunguza watu, lakini mimi nataka niseme, haikufanya haki. Hii ilitoa maonevu makali sana. Taratibu zile zilizofutwa hatujui sheria ipi, au kifungu cha sheria kilichofuatwa. Lakini mimi nataka niseme kulikuwa na unyanyasaji mkubwa sana. Mtoto ameanza kazi miezi miwili tu, anaenda kupumzishwa. Ikiwa ni watu wanapunguzwa, kwa nini msiangalie wale wamezeeka wakatoka wakaenda nyumbani? Mnachukua wale watoto hata wanaanza kazi, ati wanapunguzwa. Hapo serikali ilichangiya uonevu mkali sana. Pia zile pesa, siku hiyo waliambiwa wataenda kustaafu,

wamepelekwa seminar, wakaambiwa watapewa pesa ili waanze biashara. Pesa zile hata leo wengine hawajapata hata ndururu, na wamestaafu, na ni watoto wadogo. Je, watoto wetu waende wapi? Kwa hivyo mimi ningeomba Katiba iangalie mambo haya, madogo madogo na iyaweke sheria maanake, kuna wafanyi kazi wengine ambao wako kwa hayo mamlaka, ambayo wanayatumia kibinafsi, na wananyanyasa wale wengine. Kwa hivyo hapo iangaliwe vizuri, na tunasikia wengine wanaanza kurudishwa makazini, basi ikiwa nikurudishwa kazi niwarudishe hao huko juu na hata huku tulipo, warudi, wafanye kazi, ikiwa imeonekana ni sawa, sio taratibu za kupangwa nusu nusu.

Mambo ya uchaguzi; huwa yana muda wake maalum. Wakati watu wanapoenda kuchagua, au wakati tunaingia kwa campaign; huchaguliwa wakati wa mvua kabisaa, na mafuriko, na hii imewafanya watu wengi wamekosa haki zao za kupiga hata kura. Maanake, mahali mtu niuende na dhow, au upate boat, ndiyo uvuke uende ukapige kura, hutaenda. Masanduku yenyewe kuna sehemu nyingine, hata hayaji kabisa, kwa sababu ya mvua. Je? watu wa pale ambaye hawakupelekewa masanduku, watapiga kura? Kwa hivyo ningeomba tume hii iangalie siku zile ambazo ni nzuri za jua, za ukame, iweke siku hizo kuwa ndizo za kufanya campaign na uchaguzi; ili kuwezesha kila mtu apate ile haki yake ya kupiga kura na kumchagua yule anayemtaka. Nikisema hivyo najua tume inajua zile siku ambazo zinafaa, mzichunguze vizuri. Ni siku mbaya sana sehemu hizi, kwa hivyo kwa hayo machache, nasema Mungu awabariki.

**Com. Abida**:Tumempa mama muda mwingi, kwa sababu kawaida hata tukitizama, tunaona hakuna akina mama. Tukasema tumpe nafasi ya akina mama watatu, pengine anazungumza kwa niaba yao. Lakini tujaribu kuzungumza kwa dakika kumi; tunamuita bwana Elijah Kenga. Elijah Kenga, dakika kumi tafadhali, utakuwa hauna bahati kama the councillor. Kenga.

**Elijah Kenga**: Kwa jina naitwa Elijah Shauri Kenga. Maoni ya Katiba. Vyama vya kisiasa visizidi vinane, katika nchi ya Kenya. Kila jimbo liwe na chama kimoja. Na kuwe na serikali ya majimbo. Uchumi uliyofifia uinuliwe. Makabila makubwa yasionee makabila madogo. Miradi itekelezwe sawasawa bila kuchelewa, ndivyo raia wapate raha. Machifu, sub-chifu, na wazee wa kijiji, wachaguliwe ni raia wa sehemu hiyo. Wakikosea raia, na sababu yakutosha, watolewe na wachaguliwe wengine kabla ya kustaafu.

Clan, Land; clan land zote ziwe chini ya uwezo wa wazee wa kimila (clan elders). Tajiri asipatiwe pahali watu wanapokaa. Serikali ikitaka kutumia mahali hapo, au tajiri, ni lazima waulizwe wazee kabla ya ofisi kukubali ku-lease hapo mahali. Kwa sababu maonevu mengi yamekuwako. Tajiri ana lease mahali ambako kunaishi watu mia tatu; na wale watu wanasetwa, wanaondolewa na mali zao zinaharibiwa, na wanabaki kitupu. Tajiri anafaidika, watu wengi wanondolewa, na mtu moja ndiye tu anayefaidika.

Maisha. Maisha ni magumu sana, kufikia wakati wa sasa, elimu ni ghali, vyakula ni ghali, matibabu ni ghali, eeh kusafiri ni ghali, kulima ni ghali, uchumi umerudi chini sana. Ufisadi ni mwingi, wizi mwingi, kunyanyasa kwingi, magonjwa mengi, migomo ya watenda kazi wa serikali ni mingi. Misaada ya kutoka nje ya Kenya, ikija hapa, kwa miradi fulani haitekelezwi sawa sawa. Na

hii serikali iyangalie sana mambo kama haya, maanake tumebanwa kabisa, tumebanwa, hatuna nafasi. Tukienda huku tunazuiwa, tukirudi huku maisha yametubana kabisa.

Ikiwa mtenda kazi ambaye anapokea mshahara kama elfu sita, tena anagoma kwa sababu aongezwe mshahara , je? yule ambaye hana kazi kabisa, kazi yake ni kutumia kifua akila, atafanya nini? Katiba iangalie hapo, tupate suluhisho kamili.

Mali ya asili naomba turuhusiwe kidogo, ili tupate kuchuma; miti ya kujengea mbao, na makaa. Hivi ni vitu vya kusaidia wananchi, ili wapate kujimudu katika maisha makali yaliyoko sasa. Naomba waruhusiwe bahari na samaki kama, crabs, kamba, na tunaomba Katiba iondoe license, ili wananchi wapate kujichumia, waweze kujimudu maisha makali yalioko.

Miradi na misaada. Utakuta misaada ya kutoka nchi za nje ikija hapa, ileyenuiwa mradi Fulani; ile miradi haitekelezwi kama itakikanavyo. Utakuta miradi inapotea, inafifia kabla haijatimia. Kwa hivyo ikiwa inawezekana eeh, Katiba ijayo, wale ndugu wenye kutupatia misaada, waje wasimamie ile miradi mpaka waone imekuwa sawasawa, ndiyo waikibadhi serikali.

Dini: Dini za kuhubiri watu wasitumie madawa, zile ziondolewe Kenya, maanake zinaleta hatari. Dini kazi yake ni kuhubiri neno la Mungu tu, na kuwaonya wale ambao wanatenda maovu, lakini si kuhukumu. Na nita unga mkono yule aliyesema makadhi na wale ambao wanafanya kazi kwa uonevu, basi waachishwe kuhukumu; maanake koti liko. Sheria ya kusema imepitishwa, bila kupingwa; lilofungwa hapa, limefungwa hata mbinguni. Sheria hii iyndolewe, kwa sababu ina uonevu Fulani; wanapitisha mambo ambayo yanaonea watu wakiwa ni watu wachache, basi wanafikiria maoni ya watu wengi. Hatimaye huharibu ama huumiza watu sheria hiyo.

Uridhi. Mwanamke hawezi kupata uridhi kwa sababu mwanamke, wakati wowote anaweza kuolewa ni watu karibu sita. Kwa hivyo utampa uridhi hapa, atakwenda kula na nani? Na yeye anaweza kuolewa na huyu, kesho anabadilisha nia, anaolewa na yule, kesho kutwa anabadilisha nia, anaolewa na yule. Kwa hivyo hapo napinga.

Upande wa mila. Mila ndiyo ziweko, utamaduni uweko, kwa sababu ndio asili yetu. Hatuwezi kupinga mila, na wasichana waolewe kwa mahari, hiyo ndio desturi yetu ya Kiafrika. Sisi sio wazungu, tu Waafrika. Kwa hivyo mila hizo kama za kuoana, zibaki vile, vile na zilindwe. Mtu, kwa mfano mwanamke akifarakana na bwanake, wakati wa kuachana, sheria iko, hata kwetu iko Kiafrika. Ikiwa kuna haki ya huyo mtu apate watoto, anaweza kupata watoto; lakini kama hakuna haki, hapati. Na kukosa haki kwa kwetu, ikiwa hakutoa mahari, watoto si wake, huyo mwanamke. Lakini akiwa bwana hakutowa mali, wale watoto hawezi kuwapata. Lakini mahari yakiwa yametolewa, bwana ana haki ya kupata watoto. Kwa hivyo nimepata nafasi kidogo, lakini hayo niliyoyasema, mwenzangu atakuja kuongezea. Kwa hivyo nashukuru asanteni.

**Com. Abida:** Nataka unifafanulie tu kitu kimoja katika maoni yako. Ungependelea tuhifadhi mila na utamaduni wa Kiafrika?

**Elijah Shauri Kenga:** eehee.

**Com. Abida:** Na unasema kwamba mahari yaendelee kulipwa?

**Elijah Shauri Kenga:** eehee

**Com. Abida:** Huwa mahari hayo ni kiasi gani?

**Elijah Shauri Kenga:** Mahari, hayana kiwango kwa wakati wa sasa haijakaliwa chini na kuwekwa kiwango, kwa hivyo kila mzee wa kila mwenye mtoto anafikiria mahari anayopenda, na hapo pia na sema kuweko kiwango kamili

**Com. Abida:** Ungependelea kiwango gani?

**Elijah Shauri Kenga:** Hiyo siwezi kukata manake mimi.

**Com. Abida:** Ahsante

**Elijah Shauri Kenga:** Nina mtoto wangu na mwingine ana mtoto wake.

**Com. Abida:** Ahsante

**Elijah Shauri Kenga:** Mila zifaazo, zidumu, mila zisizofaa ziachwe.

**Com. Abida:** Julius, jina lake lingine halisomeki sawa sawa, sijui kama ni Mmenzi au Menza. Julius Menza, na ambao hawajajiandikisha ukiwa una maoni, kuna meza kule, ambao wameingia kwa wakati huu, mjiandikishe tafadhali. Endelea.

**Julius Menza:** Kwa jina naitwa Julius Menza kutoka Takamura Location. Utangulizi ni muhimu sana kuandika utangulizi katika Katiba yetu. Hii sharti ioneshe harakati zetu katika ukoloni, na kujikomboa kwetu; na mwanzo mpya wa kupigana na ukoloni mambo leo uliyoshuhudiwa miaka ya hivi karibuni. Utangulizi uonyeshe kiwiliwili chetu katika kutafuta haki. Itekelezwe kwa wote, na wananchi wote, bila ubaguzi wa rangi, au ukabila wawe na uhuru na kunufaika katika raslimali zetu za jadi. Pia ionyeshe malengo yetu ya kuishi katika amani kama jamii moja katika taifa huru. Kanuni za kuongoza sera ya dola. Sera ya maongozi yetu sharti iwepo katika Katiba yetu. Kwamba sisi tutaishi na msimamo wa watu waliohuru, na maongozi ya kidemocrasia. Kwamba kwa nia moja kutokana na tuliyoyashuhudia tunapinga na kukomesha magendo, ukabila hautaruhusiwa kutugawanya, mbali tutaishi tukifurahia tofauti zetu za kijamii. Jamii yote ya Kenya ni moja na kwamba tutasima kumaliza umaskini, magonjwa na kutojuwa kusoma na kuandika. Watoto wote waliofikia umri wa kwenda shule watapelekwa shule,

wawe matajiri, au maskini, na hii itekelezwe kisheria.

Ukuu wa Katiba. Katiba ya Kenya ndiyo mamlaka ya utawala wetu, na sharti iheshimiwe na wote. Bunge lipewe uwezo tu, wa kutoa mwongozo wa taratiba ya kugeuza Katiba, wala halina uwezo wa kubadilisha Katiba. Bunge linaweza kuunda sheria ndogo (by-laws) na hata kuziondoa lakini Katiba itabadilishwa na fungamano la kitaifa la wa Kenya, kutoka sehemu zote nchini. Huu utakuwa ni mkutano maalum wa kujadili Katiba, baada ya malalamishi kuwa yamewasilishwa kwa mkuu wa sheria. Mikutano hii itaongozwa na tume maalum ya Katiba.

Uraia. Raia wa Kenya ni yule mtu ambaye amezaliwa nchini Kenya, na ambaye vizazi viwili nyuma wazazi wake waliishi Kenya. Mtu huyu ni Mkenya moja kwa moja. Anaekubaliwa kuwa Mkenya ni yule anayechagua kuwa Mkenya kwa hiari yake mwenyewe. Isipokuwa mtu huyo, anapoamua kufanya hivyo, akane uraia wa inchi ingine iwayo yoyote. Mtu anayezaliwa na raia wa nchi mbili, apewe uraia wa kushikila, mpaka atakapokomaa, na kufanya uamuzi wake mwenyewe kuwa raia wa nchi ile mzazi wake mmoja anatoka. Uraia wa nchi mbili hauruhusiwi nchini Kenya, kwa kuwa watu hawa ndiyo mara nyingi huwa majambazi, au wakora katika nchi walizotoka. Mkenya mwanaume ajapooa mwanamke wa taifa jingine, basi mwanamke huyo, ana haki ya kupewa uraia. Hata hivyo ni vyema kupata habari kamili za mwanamke huyo, kwani wengi wa wanawake hao huwa wakongwe na lengo kamili la kuolewa huwa halipo; hivyo hutumia nafasi hiyo kufanya ujasusi, kutoa habari muhimu kwa vyombo vya habari vya nchi yao. Iwapo atakana na uraia wake vyema, na ikiwa hataki kufanya hivyo; basi huyo asipewe uraia. Vitambulisho vya aina ya passport vipewe Wakenya halisi.

Ulinzi na Usalama wa taifa. Usalama wa taifa letu ni muhimu sana kwetu sote hata ingawa ni muhimu Rais kuwa na mamlaka ya vyombo vya ulinzi, matumizi yake sharti yaidhinishwe na bunge. Vikosi vya usalama sharti view na nithamu, na hii itawezekana iwapo kutaundwa tume ya majeshi au vikosi vya usalama. Mamlaka ya nchi yapewe mamlaka ya kutetea kila sehemu ya nchi, na wananchi wetu; mbali kutangaza vita ni jukumu la bunge pamoja na vyombo vyote viwili vya serikali. Rais asiwe amri jeshi mkuu kwa kuwa yeye hafahamu wajibu au kazi ya askari. Hii itaokoa kutumika vibaya vyombo au mali ya serikali.

Vyama vya kisiasa: Vyama vya kisiasa ni sehemu muhimu sana katika shughuli za kiraia, hata hivyo, hakuna maana kuandikisha vyama kiholela, kwa kuwa vinaonyesha ulafi wa watu wanaozianzisha. Vyama vya siasa vingeshugulikia miradi ya maendeleo kulingana na sera zao. Hii ingeonyesha kwa vitendo yale wanaosema kama propaganda. Haina maana vyama kuonekana vikiandikishwa wanachama wakati wa kura pekee. Vyama hupokea fedha kutoka kwa umma, na hata mashirika mengine, na serikali za nchi za nje. Kama vyombo vya umma, vitakikane kutoa hesabu kwa umma, na hata mipango yao. Hii itafanya kuwe na mashindano ya kufanya vyama kuwa na nguvu. Vyama vya kisiasa vya kikabila vifutiliwe mbali. Iwapo chama kitafanya kazi, basi kiwashawishi raia katika manifesto zao, na zitie juhudi kutoa huduma. Vyama vya kisiasa viwe vinne pekee. Vyama vya kisiasa vifadhiliwe na serikali kwa kuwa vyama vyote ni mali ya umma. Serikali itenge fedha itakayotumiwa kufadhili vyama iwapo ni vyama vichache. Vyama vitoe hesabu za mapato na matumizi kwa serikali, kwa kuwa vyama vyote na mali zao ni sehemu na mali ya Wakenya. Kwa njia hii serikali iliyopo itaweza kufanya kazi na vyama vilivyopo, na kuondoa uhasama, na

kusumba mbaya kwamba, wengine ni serikali, na wengine ni wapinzani.

Miundo na aina za serikali. Muundo wa serikali ni muhimu sana katika kuwafanya wananchi kuwajibika katika kazi na shughuli za serikali. Hii itawezeka iwapo wananchi wana mamlaka katika huduma hizi. Tuunde mfano wa serikali za majimbo, kwa njia hii, mamlaka yagawanywe katika serikali kuu, na majimbo. Watu wawajibike katika shughuli za jimbo lao, kwa njia hii kutakuwa na mashindano na maendeleo kupatikana kwa haraka sana. Rasli mali na ushuru upatikanao katika jimbo kwa sehemu kubwa, asilimia sabini na tano, itumike katika jimbo lenyewe. Serikali kuu ipewe mamlaka kiasi.

Bunge. Uteuzi wa mawaziri, viongozi na tasisi kuu za elimu, mashirika ya serikali, vyuo vikuu, maafisa wakitaifa, na mabalozi, waidhinishwe na bunge. Umri wa mtu anayetaka ubunge, asiwe chini ya umri wa miaka thelathini na tano. Na rais asiwe chini ya miaka arubaine na tano. Mitihani ya lugha haitoshi; anayetaka kuchaguliwa, angalau awe na cheti cha kuthibitisha amesoma angalau diploma na rais awe na shahada ya digri ya kwanza. Maadili na tabia za mtu sharti zichunguzwe kwa makini, ndipo mtu huyo aruhusiwe kugombea kiti. Iwapo mbunge hawahudumii waliompeleka bunge, raia wawe na mamlaka ya kumwondoa kwa kura ya maoni. Kuanzishwe ofisi ya ombudsman ambayo itapokea malalamiko kuhusu utawala kutoka kwa wananchi. Ofisi ziwekwe kutoka mashinani.

Wabunge wafanye kazi kulingana na maagizo ya watu waliowatuma kuwawaakilishe bungeni. Mishahara na marupurupu ya wabunge iamuliwe na tume maalum wala sio wao wenyewe. Wabunge wa kuteuliwa sharti wachanguliwe kulingana na Katiba; wawe waakilishi wa watu walio wachache, wala sio kama vile ilikuwa ikifanywa. Wanawake wapewe nafasi maalum katika bunge ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za kitaifa.

Serikali ya mseto iundwe ili kuondoa uhasama uliyopo wakati huu. Rais asiwe na kura turufu ya kupinga sheria iliyopitishwa na bunge. Hata hivyo kuwepo tume ambayo itachunguza kwa makini sheria kabla ya rais kuweka sahihi sheria mpya. Hii itahakikisha sheria mpya haigongani na sheria iliopo inchini.

Mamlaka ya nchi: Mtu anayetaka kugombea kiti cha rais sharti awe na degree ya kwanza, ana ufahamu na uzoefu wa kutumikia wananchi, tabia yake ni ya kuridhisha, asiye na rekodi mbaya katika maisha, kama wizi au mauwaji. Mtu asiwe chini ya umri wa miaka arobaini na tano. Rais aongoze kwa vipindi viwili vya miaka mine iwapo atachaguliwa mara mbili. Utawala wa mikoa ni muhimu uweko lakini viongozi hawa wachanguliwe kwa kura.

Mahakama zetu ziwe huru na zisiingiliwe kutoka upande wowote. Mundo uliopo hautoshelezi hivyo kimahitaji. Mahakama kuu ya juu kabisa iundwe. Kuwe na mahakama ya Katiba kurahisisha kazi ya mahakimu. Maafisa wa mahakama wateuliwe na tume ya mahakama wala sio rais wa nchi. Maafisa wa mahakama wawe watu waliohitimu katika masomo ya sheria, angalau kiwango cha diploma au zaidi. Katiba impe kila mwananchi haki ya kudumu bila kubagua rangi, dini, au kabila.

Viongozi wa mabaraza, wenyekiti au meya, wachaguliwe moja kwa moja na wananchi, wala si madiwani kama ambavyo imekuwa ikifanyika. Kipindi cha miaka miwili ni muda mfupi sana muda huu uongezwe hadi miaka mitatu. Hata hivyo wananchiwawe na kipindi cha kupima kazi ya viongozi hawa kwa njia ya maoni kila mwaka. Iwapo kazi hairidhishi, kiongozi aondolewe.

Mabaraza ya mji na wilaya yawe huru, na yawe na mamlaka ya kuendeleza sehemu zao; ingawa yatoe reporti kwa wananchi na serikali kuu. Madiwani wawe watu wenye elimu ya kiwango, angalau kidato cha nne, au elimu inayoweza kulinganishwa na hiyo. Wawe watu wenye nia na tabia nzuri, walio na uzoefu wa kazi za kuhudumia umma, na wasio na rekodi mbaya. Kuweko na masharti ya kimaadili kwa wagombea viti vya mudiwani. Wananchi wawe na uwezo wa kumrudisha nyumbani diwani kwa njia ya kura za maoni kila mwaka; iwapo diwani hatimizi wajibu wake wa kuwaakilisha, wawe na hiari ya kumuondoa mamlakani. Mishahara na marupurupu ya madiwani ikatwe na tume maalum zitakazo teuliwa, ingawa madiwani wasiweko katika tume hizo. Madiwani maalum wateuliwe, ingawa sheria zifuatiwe kikamilifu kwa jambo hili kwamba wawe watu wanaowakiliisha watu wachache katika jamii. Waziri wa serikali za wilaya asipewe mamlaka ya kuvunja baraza, ingawa awe akitoa ushauri na mwongozo wa mambo yanavyostahili kwenda.

Muundo na utaratibu wa uchaguzi: Utaratibu wa uchaguzi utoe nafasi kwa, urithi na upokeaji wa uwezo: mamlaka ya rais yawe kwa speaker wakati wa uchaguzi, hali kadhalika, speaker hataruhusiwa kupigania rais wakati unapowadia. Rais anapochaguliwa anaaze kazi baada ya miezi mitatu. Rais aapishwe na viongozi wa kidini, mbele ya viongozi wengine wa serikali hasa hakimu mkuu na kiongozi wa watumishi wa umma. Katiba iweke masharti juu ya usalama wa kiongozi akiondoka. Asanteni.

**(Interjection not clear)**

**Com. Abida**: Fedinand Kahindi Katana.

**Fedinand**: Asante. Kwa jina ni Fedinand Kahindi Katana. Mimi nasimama hapa ni kuwa mwenye kiti wa kamati ya Locaiton ya Garashi, ambayo ilichaguliwa na viongozi wote wa Garashi Location. Kamati hii ilijaribu kuwa na vikao vine, na iliweza kutoka na haya ambayo nitayasoma kwa kifupi, ama haraka haraka, kama mlivyopendekeza. Haya ni maswala na maswali kwa ajili yamijadala ya hadharani, na yafuatayo ndio maoni ya marekebisho ya Katiba; kama yalivyopendekezwa na wakazi wa Location ya Garashi. Watu wa Garashi, kuhusu utangulizi, kwa vile Katiba ya sasa haina utangulizi, kwa kauli moja kamati ile ilipitisha kwamba, utangulizi uweko. Sitaenda ndani zaidi. Pia kuwe na tajiriba za kitaifa kama vile haki, amani, umoja na upendo.

Kanuni za kuongoza sera za dola: kamati ilipitisha kwamba tuwe na kauli kwenye Katiba, za kuongoza sera za dola. Kuhusu Katiba, imekubalika kwamba isirekebishwe kwa asilimia sitini na tano pekee. Ikiwa kutarekebishwa Katiba, wananchi wote

wawe na mikutano ya maoni katika kubadilishwa Katiba.Mikutano hiyo ya maoni iongozwe na tume ya kurekebisha Katiba.

Uraia: Utaoaji wa uraia uwe katika sehemu zifuatazo. Uraia wa kuzaliwa, uraia wa kuandikishwa, uraia wa ndoa.Haki na majukumu ya raia yawe sawa.Katiba isiruhusu uraia wa nchi mbili.

Ulinzi na usalaama wa kitaifa: Kwa sababu wakazi wa Location ya Garashi wamekubali serikali ya majimbo, basi wamependekeza, ulinzi wa ndani uangaliwe na majimbo, hali wa nje uangaliwe na rais. Rais awe amiri jeshi mkuu, na awe na uwezo wa kutangaza hali ya vita na hali ya hatari. Askari wale wa kijeshi inaonekana labda muda wao ni kidogo, kwa hivyo imependekezwa kwamba, ule muda wa kufunzwa askari uongezwe, na wapewe vifaa vya kisasa za kukabiliana na wahalifu sugu. Mipaka ilindwe daima, na kunapokuwa na shida rais awe anaona hayo. Bunge liweze kujadili na kupendekeza kwa rais hali za hatari na vita. Wahalifu wapewe athabu kali zaidi. Katiba izuie ufisadi wakati wa uajiri wa wana jeshi.

Vyama vya kisiasa: Mbali na vyama vya kisiasa, kuna masilahi ya umma ya kisiasa pia, vihakikishe kuwa haki inadumishwa. Katiba iyelekeze uundaji, uongozi na tabia za vyama vya kisiaa. Vyama visiwe na idadi maalum: Shughuli za vyama, zigaramiwe na vyama vyenyewe.

Miundo na aina ya serikali: Tufuate muundo wa serikari ya ubunge ambapo waziri mkuu anachaguliwa na chama chenye uwezo zaidi bungeni, na rais abaki kama ishara ya utaifa. Rais afungue na kufunga bunge, yani achaguliwe inje ya siasa. Waziri mkuu aunde serikali. Pia tusifuate muundo wa serikali moja, bali tuwe na serikali ya majimbo: kwa sababu Kenya ni kubwa, rasimali zitawafaidi wakazi, uongozi utaletwa karibu zaidi na wananchi, utapunguza ufisadi, na ukosefu wa kazi.

Bunge, kuwe na mabadiliko kuhusu umri wa anayetaka kugombea raisa, badala ya miaka thelathini na mitano, iwe miaka hamsini. Wananchi wawe na haki ya kumrejesha nyumbani bunge wao. Watumia kura ya kutokuwa na imani. Serikali ikate kauli kuhusu mishahara na marupurupu ya wabunge, wala sio wabunge wenyewe. Katiba ifuate serikali ya mseto, ambapo vyama vingine vinaweza kushirikiana kuunda serikali. Kuwe na njia maalum kuwaadhibu wabunge, ambao wanasababisha bunge kutokuwa na quorum. Bunge liwe na uwezo wa kutunga sheria, na kuhakikisha zinatekelezwa. Wabunge wawe na ofisi kwenye sehemu zao za uwakilishi. Kuwe na ofisi maalum ya kupeleka malalamishi: ombudsman. Kuwe na chemba mbili kwenye bunge. Senate (upper house), house of representatives (lower house), na majimbo yawe na uwezo wa kujitegemea.

Mamlaka ya nchi. Katiba ifafanue masharti ya kutimizwa na wagombea wa kiti cha rais. Umri wa miaka hamsini na usizidi miaka sabini, kiwango cha elimu kiwe cha kutoka form four na zaidi, awe mwenye sifa nzuri. Kuwe na kiwango maalum cha rais kuongoza vipindi viwili za maika mitano. Majukumu ya Rais yaelezwe kwenye Katiba, kama vile awe amiri Jeshi mkuu wa majeshi yote, na kiongozi wa serikali. Katiba itoe kibali cha kumuondoa rais mamlakani kwa kitendo kisicho halali. Hali zinazoweza kumuondoa mamlakani ni kama vile ufisadi, kutumia mamlaka vibaya, na tabia isiyo kubalika. Taratibu za kumwondoa mamlakani kuwe na kura ya kutokuwa na imani naye, uhusiano wa bunge na rais ule wa kufunga na kufungua

bunge. Rais anapochaguliwa asiwe mbunge, maana hataweza kuwakilisha vivilvyo, watu wake bungeni.

Tunahitaji utawala wa mkoa ukifuata muundo wa majimbo. Mahakama: Katiba iruhusu kuundwa kwa mahakama ya Katiba. Maafisa wachaguliwe na Paliamentary Judicial Committee. Kiwango cha elimu cha chini zaidi cha maafisa, kiwe sahada ya sheria (degree). Maafisa wapewe vipindi vya miaka kumi, wanithamishwe kulingana na mujibu wa sheria za kazi zao. Kazi na majukumu ya kadhi iwachiliwe waislamu wenyewe. Maswala yakimahakama yaydola yashughulikiwe na mahakama peke yake. Katiba ihakikishe kila mwananchi anaweza kuhudumiwa na mahakama, kwa kupunguza gharama za kesi. Ikiwezekana hata kama hana pesa; ahudumiwe, halafu alipe baadaye. Sheria zilizopitishwa na bunge zichunguzwe na wataalam kabla ya kutumika. Uhuru wa mahakama unaingiliwa na hongo, pamoja na serikali kuu. Katiba itoe adhabu kali kwa mahakama, mahakimu wafisadi, ikiwezekana, waachishwe kazi zao. Mahakamu waajiriwe na Public Service Commission.

Serikali za mitaa: Mayor na wenye viti wa mabaraza wachaguliwe moja kwa moja na wananchi. Wawe mamlakani kwa kipindi cha miaka mitano. Mabaraza yafanye kazi chini ya serikali kuu. Maafisa wakuu, watunze mali za mabaraza. Uwezo wa kuamua mambo na matumizi, uwachiwe madiwani. Kiwango cha elimu cha chini zaidi kiwe K.C.P.E., C.P.E. darasa la nane au la saba; kwa anayetaka kugombea udiwani. Mitihani ya lugha uliofanyiwa wagombea viti vya udiwani uendelee. Katiba ionyeshe masharti; kimaadili, na kitabia, kwa wagombea viti vya udiwani. Diwani atakayepoteza imani kwa watu waliomchagua aregeshwe nyumbani, kwa utaratibu wa kura ya kutokuwa na imani.

Malalamishi yapitie kwa, complains committee, ama mikutano ya viongozi, na mishahara na marupurupu ya madiwani iwekwe na serikali. Tuwe na madiwani walio teuliwa; wateuliwe kulingana na idadi ya madiwani waliochaguliwa. Mfano, chama cha siasa kikiwa na madiwani watatu kiteuwe moja. Diwani anaopochaguliwa ahudumie wananchi wote, wala sio wa chama kilichomchagua peke yake. Waziri wa serikali za wilaya awe na uwezo wa kuvunja mabaraza; wananchi wapendekeze kwanza, waziri achunguze ndio aweze kuvunja baraza.

Mundo na utaratibu wa uchaguzi. Tufuate mfumo wa uakilishi katika uchaguzi, mwenye kura nyingi atangazwe mshindi. Wanaume na wanawake wapewe nafasi sawa katika bunge, na serikali za mitaa. Kusiwe na asilimia ambayo wagombea viti wawekewe, lakini yule atakaye pita na wingi wa kura, hata akama ni moja, atangazwe mshindi. Wagombea viti wanaokosa kuteuliwa na vyama vyao, wasibadili vyama na kuomba uteuzi katika vyama vingine; mpaka uchaguzi mwingine. Mtu binafsi, yuko huru kuomba maoni ya kuhama na kujiunga na chama kingine. Ikiwa ni chama kimejiunga na kingine, basi uchaguzi ufanywe kutoka mashinani, hadi ngazi za juu. Tuwe na viti vilivyotengezwa kwa walemavu. Tuendele kuwa na mfumo wa maeneo ya kigeografia ya maeneo. Sehemu za ubunge, na madiwani ziongezwe kukiwa na uhitaji. Utaratibu wa uchaguzi urahisishwe. Kura zipigwe na kuhesabiwa kwenye vituo. Kusiwe na kiwango cha juu cha matumizi ya fedha za uchaguzi kwa kila mgombea kiti. Tarehe ya uchaguzi itajwe kwenye Katiba. Rais asichaguliwe moja kwa moja, kwa vile wakazi wa Garashi wameamua kuwa na serikali ya majimbo; kwa hivyo rais achaguliwe na bunge.

Utaratibu wa uchaguzi wa elfu mbili na mbili uwe wa siri. Uchaguzi wa udiwani ubunge na urais uwe siku tofauti. Kura zihesabiwe kwenye kituo (polling station). Idadi ya ma-commissioner wa uchaguzi ibaki hiyo hiyo, ishirini na mbili na mwenyekiti. Ma-commissioner wawe na degree ya sheria. Wachaguliwe na vyama vya kisiasa, halafu bunge liwapitishe. Wawe na usalama wa kikazi. Wafanye kazi kwa kipindi cha miaka mitano. Waondolewe kulingana na mujibu wa sheria. Shughuli za commisiners zigaramiwe na serikali.

Haki za kimsingi: Masharti ya Katiba kuhusu haki za kimsingi hayatoshi. Hukumu ya kifo iendelee, Katiba ilinde haki za kimsingi ya Wakenya wote.Serikali ihakikishe Wakenya wote wanafurahia haki za kimsingi kama, elimu, afya, usalama, maji, makaazi, chakula, na ajira. Katika haki za kimsingi; maswala kama gharama, usambazaji, na ajira, yana paswa kushughulikiwa na Katiba. Kuwe na elimu, matibabu ya bure kwa kila mwananchi, ikiwezekana, elimu ya bure hadi form four. Kuwe na huduma za mobile clinics hasa kule ambako hakuna zahanati karibu.Serikali ipeyane makaazi kwa chokora, maskini, na wakongwe. Wakati wa njaa, serikali isaidie kwa kutoa chakula, isimamie bei za mazao, itoe mikopo kwa wakulima. Upande wa ujira serikali ihakikishe mtu moja, kazi moja. Katiba ihakikishie wafanyi kazi, haki ya uwakilishi katika vyama vya wafanyi kazi. Wakenya wawe na haki ya kupaswha habari zilizoko mikononi mwa serikali. Kusiwe na ubaguzi wakati mahitaji ya kimsingi yanapotolewa. Pengo la mshahara baina ya mfanya kazi wa juu na wa chini lipunguzwe.

Haki za makundi yanayoweza kudhuriwa. Mahitaji ya walemavu hayakushughlikiwa kikamilifu. Mahitaji ya walemavu ambayo yanapasa kushughulikiwa na Katiba ni kama vile; elimu ya bure, itoe vifaa vya walemavu shuleni, itoe matibabu ya bure, iwaajiri wakalimani, hasa wakati wa kesi. Kutolewe fidia kwa wazaliwao walemavu. Hao ni wale ambao wanazaliwa walemavu moja kwa koja. Ujenzi wa nyumba, na magari, ufikirie masilahi ya walemavu. Katiba inaweza kulinda haki za watoto kupitia sheria za kulinda haki za watoto. Kusiwe na ubaguzi baina ya wanawake, wanaume, vijana na walemavu.

Haki za ridhaa na mumiliki wa mwisho wa ardhi awe mtu binafsi. Waridhi wa ardhi, wawe mama na watoto. Yasiendelee kuwepo mapatano ya ardhi ya kijamii yaliokwepo kabla ya uhuru sababu hiyo italeta ukabila na uskwota. Kuwe na vizuwizi katika umilikaji wa ardhi. Kuwe na kiwango cha juu zaidi kuhusu umilikaji wa ardhi.Katiba ihakikishe haki ya kila mkenya kumiliki ardhi. Kuwe na kanuni za umilikaji wa ardhi, miongoni mwa watu wasiokuwa raia.

Haki za kijamii na tofauti za kitamaduni, kikabila, na kieneo: Tofauti za kitamaduni na kikabila zilindwe na kuendelezwe. Kwa mfano, utamaduni wa mijikenda umeingiliwa na serikali, kwa kupiga marufuku pombe ya mnazi wakati wa mahari; ambapo kwa kawaida mijikenda wanalipa mali wakihesabu ndama. Kama ni ndama nane, hawa ni ngombe wanane, jike. Kama ni ndama tisa, ni ngombe tisa jike. Lakini ndani yake, ni lazima kuwe na kajama ishirini na nne za pombe ya mnazi, lazima ziweko. Na asiye lipa kajama ishirini na nne, anakosa haki ya kupata watoto. Kwenye sherehe zote za kitamaduni, lazima pombe ya mnazi iwepo. Kwa hivyo mapendekezo yalioko ni kwamba, mnazi usimamiwe, kwa kutoa leseni kwa mgema yule analitoa lile pombe atoe license kwa council. Huo ni ushuru kwa council. Yule anasafirisha pombe hiyo, akate license kwa council; hiyo ni kuleta pesa kwa council. Na kule atakalolipeleka kuwe na kilabu maalum, ambacho kilabu kile mwenye kilabu hicho atakata license;

ambalo pia ni pato kwa council. Pili. Kuwe na masaa maalum ya unyuaji wa hiyo pombe. Kama vile mabar yanavyouza pombe ile ya beer.

Mahari: Kwa sababu hali ya pesa inazidi kudidimia, mambo haya ya mahari ipunguzwe; na kuna hali ya kitamaduni hii, na sijui kama tunaweza kuyaondoa, lakini si rahisi, tuseme kuwa tunaondoa utamaduni huu, mtu anapokosea. Kwa mfano, mama anapofumaniwa, huwa analipa makosa; lakini imefika kiwango cha kwamba, wengine hudai malu zaidi ya ile mahari aliyolipa yeye. Hii isiweko. Ikiwa ni malu, ni makosa tu ya kumwadhibu yule baba aliyefumaniwa. Kwa hivyo ipunguzwe iwe chini. Tuwe na lugha moja ya kitaifa. Katiba itambue, na iendeleze lugha za kienyeji.

Uwongozi na matumizi ya mali asili.Uwezo wa kuthibiti uongozi na matumizi ya mali asili uwachiwe majimbo. Bunge liendelee kuamrisha ukusanyaji na matumizi ya fedha za umma, kwa kushauriana na majimbo. Njia nyingine zinazoweza kutumiwa na serikali, bali na kodi, kukusanya pesa; ni misaada na mikopo kama vile investments. Ugawaji raslimali za kitaifa, ufanyike katika hali ya kumfaidi zaidi yule mwananchi ambaye yuko karibu na raslimali hiyo. Serikali ihusikike katika ugawaji raslimali. Mbali na mkaguzi na msimamizi mkuu wa fedha za umma, kufichuwa kashfa za pesa, awe na mamlaka ya kuwachukulia hatua wafujaji wa mali za umma. Msimamizi na mkaguzi mkuu aajiriwe na tume ya huduma za umma. Wanachama wa tume ya huduma za umma, Public Service Commission, wateuliwe na bunge. Tunapasa tuwe na kanuni za maadili kwa maafisa wa umma. Maafisa wa umma walazimishwe kutangaza mali zao. Tunaweza kuwavutia watalamu wa Kenya kufanya kazi katika mashirika, kwa kuwapa mishahara mizuri.

Mazingira na mali ya asili. Maswala ya uhifadhi na mazingira inayopaswa kuingizwa kwenye Katiba ni uwindaji, ukataji miti, uvuvi, wanyama pori, uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa mimea, uuaji wa binadamu na wanyama. Wakazi wa sehemu ambayo mali asili iko, wawe na uwezo wa kumiliki. Mali asili zipasazo kulindwa na Katiba ni maji, misitu, ardhi, wanyama, na madini. Wanajamii wana, jukumu la kulinda usafi, na kudumisha na kuendeleza raslimali. Mwenye jukumu la kusimamia na kulinda mali asili ni serikali.

Utawala wa kushirikisha. Maswala yanayohusu mashirika ya kiraia, yanayopaswa kushughulikiwa na Katiba, ni pesa, usimamizi, na maongozi. Dola iyelekeze utenda kazi wa mashirika ya kiraia, na vyombo vya habari. Utaratibu ufaao ni wakuto wabagua kwa hali za kijinsia: vijana, wazee, na makundi ya watu wachache.

Uhusiano wa kimataifa utendaji kazi na maswala ya uhusiano wakimataifa uwachiwe mamlaka ya nchi pekee, hasa wizara ya mambo ya nje. Bunge liwe na jukumu la kushauri, kujadili hoja, kupendekeza kuhusu maswala ya uhusiano wa kimataifa. Bunge litoe mwongozo na mamlaka ya nchi, kama vile waziri wa mambo ya nje. Serikali iwe inatekeleza. Maafikiano na mapatano ya kimataifa, na kimaeneo, yasiwe na athari moja kwa moja katika sheria za nchi. Zinaweza kutekelezwa wakishauriana na bunge.

Tume za kiKatiba, tasisi, na afisi. Tunahitaji tume za Katiba, tasisi, na afisi kama hizi, tume ya kurekebisha Katiba, tume ya haki

za binadamu, tume ya jinsia, tume dhidi ya ufisadi, tume ya ardhi. Katika Katiba hii kuanzishwe ofisi ya mpokeaji malalamishi, yani ombudsman. Urithi na upokaji wa uwezo. Spika wa bunge awe na mamlaka ya nchi wakati wa uchaguzi wa urais. Rais aliyechaguliwa aanze kazi yake, miezi miwili baada ya uchaguzi; rais aapishwe na jaji mkuu (Chief Justice). Katiba iweke masharti kwa manufaa ya rais anayeondoka; kuhusu usalama na maslahi. Katika maslahi, marupurupu yapigwe tochi, na kupunguzwa, kulingana na uchumi wa nchi. Asiwe na kinga dhidi ya mashtaka. Ni hayo tu, asanteni.

**Com. Abida:** Asante, utajiandikisha pale. Rachael Kahindi.

**Rachael Kahindi:** Mimi naitwa Rachael Kahindi. Nawasomea memorandum yaakina mama kutoka Marafa Division, na National Commission on the Status of Women. Katiba iwe na utangulizi. Wanawake wa kato ya Marafa wameona kwamba, kuweko na utangulizi kwenye katika mkataba. Kwenye Katiba mpya yafwatayo yawekwe kwenye utangulizi huo. Jinsi vile tulivyo pigania uhuru kwa kuteswa na wakoloni na kumwaga damu; ya kiwemo majina ya wale wahusika waliokuwa mstari wa mbele bila kubagua wanawake. Kwa mfano, Mekatilili kutoka huko wilaya ya Kilifi. Sifa za rais wa Kenya wa kwanza, na mwaka tuliopata uhuru, jamhuri, ikiwemo mwezi na tarehe; waziri wa kwanza mwanamke, meya wa kwanza mwanamke, jaji wa kwanza mwanamke, PC wa kwanza mwanamke, na wale walioshika nyadhifa mbali mbali za uwongozi wa serikali, na mashirika. Kusistiza kuwepo kwa demokrasia iliyokomaa sahihi. Kusisitiza juu ya umuhimu wa kuangamiza umaskini, magonjwa na kutojuwa kusoma na kuandika; umoja wa kitaifa, kuangamiza ukabila, kuinua hali ya uchumi, na kuangamiza ufisadi. Katiba itambue umuhimu wa wanawake, walemavu, na watoto, katika kuchangia mabadiliko ya kimaendeleo, kutokana na ujuzi maalum walionao, haswa mama.

Matatizo ya akina mama katika Katiba: Kwanza mila na desturi. Kulipiwa mahari. pesa zinazotolewa na bwana kama mahari zisiitwe mahari, bali shukrani, ama zawadi ya bwana kupewa mzazi. Watu hawa wawili wanakuwa huru hii inaondoa utumwa. Mzazi anafaidi kutoka na watu hawa wawili. Tunataka mahari yaondolewe. Kila atakaye olewa apewe kibali maalum (Marriage Certificate).

Urithi wa mali kwa mwanamke kutoka kwa wazazi wake: Mtoto wa kike ahesabiwe katika urithi wa mali za kwao, sawa sawa na mtoto wa kiume. Kutohusishwa kwenye kutoa maoni, ama kukata shauri kwa kina mama, kukosa mamlaka kinyumbani, mashauri ya familia yahusishwe wote katika jamii, baba, mama na watoto wote kwa miradi yote, kwa mfano maendeleo ya kielimu, uuzaji wa ardhi. Kamati zote za maendeleo kwanzia vijijini hadi ngazi za ki taifa, kina mama wachukue nafasi, hii itaondoa ubaguzi wa kina mama, walemavu, na vijana; wasitengwe katika kukata shauri.

Malu: Malu ni faini inayotozwa bwana anaposhukiwa akifanya mapenzi na bibi wa mwenzake kwa wa mijikenda. Mali yastahili kuondolewa inachangia umalaya, na kuongeza kuenea kwa magonjwa ya zinaa. Malu inaaibisha jamii nzima. Malu iondolewe ili bwana na bibi waheshimiane. Tunaendelea na kukosa mamlaka. Mke nyumbani: maswala ya watoto, mama awe na uwezo, hata kama baba hayuko.

Raslimali za nyumbani: mama na baba wajiandikishe wote, majina yao yaandikwe kwa mali zao zote zitakazo orodheshwa wakati wa maisha yao.

Kubaguliwa kwa mtoto msichana: mtoto msichana hatambuliwi kwa umuhimu katika jamii, ki elimu. Msichana hunyimwa haki za ki-elimu, hata haki za uridhi. Msichana akitiwa mimba shuleni yeye hufukuzwa shuleni, na mvulana huwachwa kuendelea na elimu. Mapendekezo. Mtoto wa kike apewe elimu sawa sawa na wa kiume, kama atakavyoweza. Serikali inunue vitabu, na vifaa vingine, kusaidia watoto wote, hasa wasichana. Elimu iwe ya bure kwa shule za msingi, darasa la kwanza hadi la nane. Msichana akitiwa mimba, yule anayehusika achukuwe jukumu la kulea mtoto atakaye zaliwa mpaka awe mkubwa. Kuridhiwa baada ya kufiliwa na bwana, kunyang'anywa mali: mambo ya kuridhiwa baada ya kufiliwa na bwana yaondolewe. Mali iliyowachwa ni ya bibi. Wazazi wa bwana aliyefariki wapewe robo ya mali hii iliyowachwa.

Sheria za kifamilia: kina baba kulala na binti zao. Kina baba hao wanastahili kushtakiwa na kuhukumiwa kunyongwa. Kuwe na mahakama ya kisiri kwa kesi za kubaka. Mtu akibaka msichana, akatwe sehemu za siri, ahasiwe.

Kukosa uhuru wa kibiashara kwa kina mama.

Mnazi: kuuza mnazi ndio biashara yetu muhimu ambayo imewekewa vikwazo. Kuwe na utafiti ili zile bidhaa za mnazi, ziwezekuuzwa, ili uwe na manufaa kwa wanaokuza. Mnazi uhahalishwe bungeni, ili mnazi usaidie uchumi hapa Pwani. Mnazi uuzwe. Kiwanda cha utafiti wa mnazi, kijengwe hapa pwani, viwanda vingine vidogo, vidogo, kama vile cha korosho, virudishwe hapa, ili biashara iweze kuendelea.

Ufisadi: ufisadi umechangia kudhofika kwa uchumi na biashara. Kwa mfano, mbao, makaa na kuni. Mahongo yamezidi sana. Ufisadi ukomeshwe; na mtu yoyote akipatikana na hatia ya ufisadi, aachishwe kazi, kama ameajiriwa. Kuwe na sheria ya kuhukumiwa, kukatwa mkono.

Ubaguzi wa ajira: vijana wengi, Kenya nzima wamesoma na kubaki bila kazi: Jambo hili limesababishwa na ubaguzi wa kuaajiri, kwa kutafuta ujuzi, kama wa miaka mitano kwanza. Kuwe na sheria, vijana wapate nafasi ya kwanza kuandikwa kazi, baada ya kumaliza masomo yao vioni, maana ni vigumu kuwa na ujuzi kabla ya kuajiriwa kazi hiyo. Ukosefu wa kazi Kenya umechangiwa na ubaguzi.

Uraia: raia wa Kenya awe amezaliwa hapa, na wazazi wa hapa. Mtoto wa kuzaliwa na mzazi mmoja ni raia bila swali. Katiba ya Kenya iruhusu uraia wa nchi mbili. Raia wawe na vitambulisho vya kawaida. Uraia wa mtoto aweze kujulikana kwa jina la mzazi wake ambaye yuko karibu, baba au mama. Aweze kuitwa jina lake kwenye kitambulisho.

Vyama vya kisiasa: vyama vya kisiasa viwe na idadi, na visiwe zaidi ya vitatu. Vyama vijitegemee kupitia kwa wanachama

wao kugharimia shughuli zaki siasa.  Yeyote anataka kugombea kiti cha udiwani, ubunge, au uraisi, lazima awe amesajiliwa na chama fulani.

Muundo wa serikali:  tufuate muundo wa serikali ya majimbo, ambapo mamlaka ya nchi na bunge yamegawanywa baina ya serikali kuu, na majimbo maalum.  Kwa nini?  Tuweze kugawa mamlaka, raslimali, na ushuru na nafasi za kazi kwa wenyeji.

Bunge:  Lugha zitakazotumika ni tatu.  Kiswahili, Kingereza na Kienyeji.  Hayo ndio mabadiliko yatakayofuatwa.  Kuwe na tume maalum itakayochunguza mishahara na marupurupu ya wabunge.  Rais akiwa mume, naibu awe mke, na rais akiwa mke naibu awe mume.  Kila wilaya itenge kiti kimoja cha bunge maalum, kitakachogombewa na kina mama pekee, kwa kutetea haki za akina mama.  Wabunge wateule wachiwe wakina mama, na walemavu, na vijani ili, tupate kuwa sambamba.  Bunge liwe na uwezo wakupitisha mambo bila kumtegemea rais.  Masaa ya wabunge yawekwe maalum, kuenda bungeni; isiwe ni kila siku, ili wawahudimie wananchi.

Mamlaka ya nchi:  rais awe raia wa Kenya wa kuzaliwa.  Awe amechaguliwa kuwa bunge, aweze kugombea kiti cha urais. Vipindi vya rais viwe viwili, vya miaka mitano, mitano.

Serikali za mitaa:  Wenyeviti wa ma baraza ya miji wachaguliwe na wananchi, hii ni pamoja na meya, vipindi viwe vya miaka mitano kwa, wenyeviti na meya wa mabaraza.  Madiwani wawe wamesoma kiwango cha elimu kidato cha nne.  Kama diwani ni mlegevu atolewe na kura ya maoni (vote of no confidence).  Kutoa nafasi kwa watu wengine kugombea nafasi hiyo. Asanteni ni hayo machache.

**Com. Abida:**  Tafadhali ikiwa una nakala ukisoma yote, naona aibu kuwachisha lakini naona, tufuate utaratibu uliowekwa.

**George Mtawali Kazungu:**  Kwa majina naitwa George Mtawali Kazungu, na kabla sijatoa maoni, ningetaka kuomba ruhusa kwamba, hapa kuna wenzangu wawili ambao wamenipatia maoni yao; na kwa sababu wamekosa nafasi za kufika hapa, wameniomba ni wasomee.

**Com. Abida:**  Tafadhali ukiwa una nakala peyana pale, sababu nitakupa dakika tano peke yake.  Ikiwa kuna nakala zimeandikwa utaratibu ni kwamba unapeana pale, na kupa dakika tano pekee yake kila mara.  Sasa fanya management: ukitaka kusoma za wenzako sawa, ikiwa zako, nakupa dakika tano.

**George Mtwali Kazungu:**  Okay, sasa, mimi nitasoma zile zangu za wenzangu pengine nitapeana pale.  Maoni ambayo nayasoma hapa, ni maoni ambayo ni ya wanachama washirikisho, kutoka Marafa Division; na kwa vile Shirikisho ni chama cha kisiasa, ambacho kinajulikana sana hapa pwani, hicho kimekuwa kikiimba wimbo wa majimbo, tangu miaka ya nyuma: kwa hivyo utakuta maoni yetu zaidi yamelalia upande huo.  Na nasitikika ama tumepeana maoni hayo kwa lugha ya Kiingereza, na

nitasoma kama ilivyo. Kwa hivyo wale ambayo hawasikii lugha hii watanisamehe.

We want a new Kenya of Majimbo, the constitution should be changed to allow the creation of federal states of the Republic of Kenya; that is majimbo. The constitution should allow each state to form its own regional federal state assemblies; refered to as majimbo. The constitution should allow the regional states to come together to make the new Kenya of majimbo, the federal republic of Kenya, whose capital will be in Nairobi, the seat of the federal government. By virtue of the federal constitution, no jimbo shall secede from the rest of the federal republic of Kenya. The federal state in majimbo political philosophy, shall be: the costal federal state, the Eastern federal state, the North Eastern state, the Nairobi federal capital state, the Central province federal state, the Rift Valley federal state, and the Western Kenya federal state, the Nyanza federal state. Why do we want a new Kenya of majimbo? The present unitary system of government; where for the past thirty nine years, since Kenya's independence in 1963, the entire country has been ruled from the capital, Nairobi. The Government has failed in fostering good governance, transparency and accountability. The government has instead created a state of plunder and poverty, with tribal domination among the people of Kenya. The federal system of government, we hope, will put to an end these kind of misrule; through power sharing with people in all federal regional states of Majimbo, in the republic of Kenya.

Regions: People should elect their representatives to the regional assemblies, which form the nucleus of the federal state. Constitutionally established the state governments, majimbo regional assemblies, will have their own state. Governors will be directly elected by the people. The federal state through, a constitutional arrangement, will join together in the formation of the federal state of the Republic of Kenya.

Mode of Government: Presidential elections with a running mate, will be through direct voting on a two term, of five years rotation basis; from each region. Parliament to create the number of ministries required. The President will have powers to nominate professionals to the post of cabinet minister. All chief executives appointments of federal government departments, including the exchequer, governor of the central bank the auditor general, ambassadors, high commissioners, and the attorney general will be vetted by parliament.

Education: Each state should propose to run its end user education system, with the establishment of their own regional education boards. Each region should have its own state university, and a regional quota system of intake, to the existing state universities. Education be compulsory. Free education from standard one to eight, and the Government to assist those who can not afford university fees.

Security, Law and Order: The new constitution should be changed, to ensure that human life and property, are given full security cover at all times; night and day, to ensure that law and order is maintained fully, under the rule of state and federal law commission. No detention without trial. Hakuna kuwekwa mtu kuzuizini bila kuwonekana kweli kwamba ana hatia. The new constitution should guarantee, the right to live and travel in any region within the federal republic of Kenya; without any

hindrance, or obstruction on tribal, colour or religious considerations. The right of ownership of property any where in the Federal Republic of Kenya; should also be guaranteed by the Constitution.

The Civil Service. Each regional state shall run its own civil service, with provision for interstate labour exchange programmes; designed to off-set both professional and unskilled labour force in other regions, when and where jobs are available. The constitution should allow trade unions, to thrive and practice free bargaining and negotiations. Equal jobs for equal pay opportunity for all, in any given state, of the federal republic of Kenya.

Land. Land ownership and trust land. Sessional paper number 10 of 1965, must be revisited to seal of all the loopholes. The constitution should revoke all the wrongly issued title deeds, government lands in all regional states, that is majimbo, to be held in trust for posterity. There should be regularization and standardization of land allocation, giving more preference to agro-commercial and export companies. The constitution should establish in each regional state; the regional commissioners land offices, to oversee the region's land tenure rights. Regional land control boards should be manned by elected local residents, to curb grabbing. Regional states anti-corruption commissions, with powers to prosecute offenders; should be formed.

State corporations. State corporations if well managed, could provide financial resources. So there is no need for them to be privatised. Road, water works, and forest resources, should also not be privatized. Those to be privatized must be fully discussed, by the stake holders. Kenya ports and Harbours authorities should be under respective authorities, and not be privatized.

Federal Majimbo Funding And Financing: 70% of the revenue collected by the regional government should be retained and 30% remitted to the federal government. The Federal Government should look after the federal parliament, immigration, the federal armed forces, foreign missions and the judiciary. Government assets, in each region should be handed over to those regions they are situated in. Imports and exports to be taxed at their points of exit and entry of the Federal Republic.

Human rights observance. The Republic of Kenya is already a signatory to the UN Human Rights Charter. So the new constitution should enhance greater observance of the UN Charter. Exercise greater freedom of speech and association. Advocate more transparency and openness through a public complains commission and the office of the ombudsman. No ethnic group is to be expelled, or discriminated against, in any federal jimbo of the Republic. No regional government will base their governance on ethnicity, colour bar, or religion. Gender equality: the constitution should ensure that, at least 30% of senior jobs in the public service go to women.

**Com. Abida:** Please summarize.

**George:** Yes I am finishing, Yaa namaliza. External borrowing. The new Constitution should promote and welcome foreign investments, support by foreign donors to the regional governments such as the World bank, IMF, and bilateral institutions.

Elections. Voters registration be a continuos process. ID Card age issuance be reduced to 15 years. Village elders, assistant chief, chief, councillors, MP's to be elected. Na hawa kama wanafanya makosa, waitwe na wazungumziwe hali yao. Mayors, county council chairmen to be directly elected by the people. Finally, mnazi, tunataka Katiba hii yetu ihalalishe mnazi, iwe ni pombe sawa sawa. Mnazi si pombe kama zile zingine ambazo tunazisikia kule juu kama, chang'aa, busaa na kadhalika; ni kitu natural hata namna inavyopatikana. Kama mnazi vile unavyopatikana ni kitu cha kimiujiza, kama vile mama azae mtoto na akose, maziwa.

**Com. Abida:** Tafadhali zungumza kwenye microphone.

**George:** Akose kuwa na maziwa, mama akijifungua kama hana maziwa, ndio hali ya mnazi. Unaweza kupanda mnazi huo na ukose pombe kabisa, upande mnazi ule upate pombe nyingi, kwa hivyo ni kitu natural; hatuoni kwa sababu mnazi usiwe halali, kama zile beer zingine. Kama vile mwenzangu alivyosema, tujaribu kufanya utafiti, na ule utengenezwe kiufundi, uwe na soko nchi za nje. Asante.

**Com. Abida:** Asante, Joshua Ngowa, Joshua Ngowa.

**Raymond Mwaro:** Sawa, kwa jina naitwa Raymond Mwaro. Maoni yangu serikali ambayo itafatia, ninayoitaka mimi, ni serikali ya majimbo.Oni langu la pili, uteuzi unapofanywa katika bunge, iangalie yule anayeteua watu kuwa mbunge maalum, au waziri; kuchagua awe anachagua watu kutoka wilaya zote.

Ufanyaji kazi: kama tunavo, fanya kazi hapa nchini, tunafanya kazi, wengine usiku, wengine mchana. lakini katika idara hii ya polisi, wachunguze kosa la mtu sawa sawa ndio mtu akamatwe. Si kushika mtu ametoka kazini usiku, na anamwambia mimi nimetoka kazini; yeye anasema "kaa pale", anapoteza wakati wa mtu. Kama mtu huyu, akikosekana kuwa ana kosa, basi askari huyu akimchukua namba yake; astakiwe, na alipe makosa na masaa yale ambayo amempotezea mtu huyo.

Watoto wawe wa bwana kwa, sababu, kwanza kabisa watoto huitwa kwa jina la baba, sababu ametoa mali: tena hata mbari pia, huitwa katika bari ya baba, hivyo kumfanya mtoto awe na msimamo maalum. Lakini tunapomwambia mtoto huyu ni wa mama, yeye hajui kule mbari yake inakaa vipi: akifika kule anapigwa, anaambiwa wewe siyo wa hapa. Sasa huyo mtoto huenda akawa chokora na akatatiza nchi. Kwa hivyo lazima awe wa baba. Serikali itie manani sana jambo hilo; kwamba mtoto awe wa baba siku zote za maisha yake.

Mali na iendelee kulipwa kwa wazazi; bila hivyo, wanawake watakua wajeuri, na kufanya lolote watakalo, na hii itasababisha

watoto chokora inchini Kenya.

Mahakama. Baada ya mtu kusomewa mastaka yake, mtu huyo apewe free bond, awe akiitikia siku zake za kesi. Si kuwekwa ndani na hajajulikana kwamba ana makosa. Hii ni kufanya mtu anaconda, na hata hana makosa, yule mshtaki mwenyewe anabaki kule akiwa na afya zake; mara tu kesi inapozungumzwa anakutwa yeye mshtaka ni mwongo, na inachukilwa vile vile tu. Hii inaleta vibaya sana kati uraia wetu hapa nchini Kenya. Kwa hivyo mahakama ni lazima itilie maanani mtu kama amesomewa mashtaka yake; hapo hapo anapewa free bond, na anaendelea kuitikia, mpaka kesi yake itakaposikizwa.

Kitu kingine. Katika uraia, kama serikali zaidi imeingia hata katika maboma, haitoi uhuru sawa sawa katika watoto wetu. Pengine mtoto mtu anaweza kumchapa, sababu yeye anaendelea kuiba mle nyumbani; ananza kumtia tabia njema, akimpiga sana, basi mama anaruka anaenda kustaki kwa Chief mzee anawekwa ndani. Kwa sababu anasema amepasua pasua ukimwangalia kule kwa Chief, yule mtoto hata hakupasuliwa. Ni kwa sababu mama hawa wengine, pengine ana chuki, hamtaki yule bwana, ndiposa anaenda kuleta visingiziwi ambavyo si vya halali. Mzee huyu anawekwa ndani. Hayo ni maoni yangu. Mungu awabariki.

**Com. Abida:** Asante, Menza Cornelius, George Kombe

**Injection:** George Kombe,

**Com. Abida:** Robert Vitalis, Robert Vitalis

**Interjection:** Vitalis

**Com. Abida:** Mnaogopa, au mna mambo gani? Kahindi Kitsao.

**Interjection:** Kahindi Kitsao

**Com. Abida:** Kazungu Tuva, , George Harry, Naomi Mkane, labda kina mama watazungumza, Naomi yuko wapi? Hudson Mbaya, wananchi wa sehemu hamtaki kuandikia Katiba, tunahuzunika. Hudson Mbaya, Kingi Ngumbao, Daniel Mwendwa.

**Interjection:** Daniel Mwendwa

**Daniel Mwenda:** Asante, kwa majina naitwa Daniel Mwendwa. Nitaanza na elimu. Elimu ya sasa imeonekana ni too expensive. Ningeomba Katiba ambayo tunayo sasa ikiwa inawezekana irudishe ile elimu ya 7-4-2 and University; badala ya 8-4-4. Kwa upande wa malipo, watoto wawe wakilipa shillingi ishirini, kama vile walikuwa wakilipa hapo mwanzo. Kwa

sababu watoto ni wengi, na wakilipa shilingi ishirini, zitakuwa pesa nyingi. Serikali ilipie gharama za shule za msingi, kama vile ilikuwa inafanya hapo mwanzo. Kuna watu wengine wanaitwa maofisas, wanatembea na mapiki piki, wakifika shule, committee za shule zinaambiwa ya kwamba pikipiki haina mafuta. Wazazi wachange pesa waweke mafuta. Yule mtu aliyempa ile pikipiki, ni naomba Katiba ya sasa, impatie mafuta; ili mwananchi apunguziwe matatizo hayo.

Mitihani. Kumekuwa na mitihani miingi ya mtoto, hata hana nafasi ya kupumzika. Hapo mwanzo watoto walikuwa wanafanya terminal and finals. Ingefaa jambo nzuri ikiwa itarudishwa kama zamani. Mtoto akifanya terminals mara tatu, ana qualify kwenda darasa lile lingine mwaka ujao; na aendelee mpaka amalize.

Afya. Tuliambiwa mwanzo ya kwamba tunatumia cost-sharing, lakini sasa imekuwa cost-bearing. Unaweza kupeleka mtoto hospitali upewe bill, and at the same time uambiwe ukachukue dawa pharmacy. Ningeomba kama inawezekana, hata kama itakuwa cost-sharing, lakini iwe ni at least twenty shillings per patient: halafu serikali ipeane dawa zinazofaa. Dispensary zote ziwe na maternity wing, kwa sababu kuna dispensary ambazo ziko mbali sana; na hakuna ngari na mama akiwa mja mzito, itakuwa ni vigumu kumtoa pale na kumpeleka mahali anapohitajika; na anaweza kufa hapa njiani. Kwa hivyo kama inawezekana, constitution ya sasa I provide maternity wings to all dispensaries, ili wakina mama waweze kuzaa, bila matatizo.

Operation. Ukienda district hospitals, unaambiwa ulipe deposit fulani, wakina baba wengine hawawezi ku-afford those seven thousand, ningeomba serikali ya sasa ilinde mwananchi, ikiwa mama ni mja mzito na labda ameshindwa kuzaa, mpaka afanyiwe operation, aweze kufanyiwa upasuaji bila malipo. Na ikiwa ni lazima, akopeshwe, aende nyumbani, akatafute pesa, aje alipe. Nakuwe kuna sheria ya kumlinda akiwa nyumbani, ili alazimishwe kuja kulipa hiyo bill: ili yule mama na yule mtoto wawe wanaweza kupata afya nzuri.

Haki za watoto. Kimila wakati huu kinasema ya kwamba mtoto apewe baba yake mama aende ninaonelea, sheria za sasa, Katiba ya sasa; yule mtoto baba na mama wakitengana, yule mtoto alindwe na wale watu wawili, kwa sababu mtoto hana makosa. Bibi na baba ndio wamekosana, mtoto hakukosea mtu yeyote. Nialindwe mpaka afikishe miaka eighteen, from there mtoto a decide ataweza kuishi kwa nani. Yeye mwenyewe, siyo kulazimishwa na kimila wala court. Yeye mwenyewe akifikisha eighteen years ataamua ataishi kwa baba, ama kwa mama.

Pombe ya mnazi ihalalishwe, lakini ifanyiwe marekebisho fulani; isiuziwe mustuni ama barabarani. Ijengewe nyumba safi, iwe biashara kama zile zingine, wakate licenses. Na mtoto ambaye anasoma, ama yuko under eighteen years, asiruhusiwe kuingia pale na kunywa pombe; kwa sababu hatapata nafasi ya kusoma vizuri. Ifanyiwe utafiti iweze kuuzwa nationwide.

Headquarters. Imekuwa ni mtindo wa serikali kupeleka headquarters zote Nairobi. Ningeomba Katiba ya sasa, headquarters zipelekwe katika district level. Iwe ukiwa na shida zako, ukipeleka kwa DC, unahudumiwa, unarudi nyumbani. Bila kuambiwa, enda ukachukue barua Nairobi, enda ukachukue hii Nairobi, zipelekwe kwa DC. DC awe huru wa kumaliza kesi zote si zile

ndogo ndogo tu.

Ridhaa, imekuwa mtu akianguka na gari, anafanya kesi ten years, na inapotea hivo hivo. Ningeomba Katiba ya sasa, imlinde mwananchi, akianguka na gari; after three months, analipwa. Na ikiwa shamba limelishwa na wanyama porini, after two months analipwa. Sio mahindi yanaliwa na wanyama, halipwi; na wewe ukumua yule mnyama, unafungwa. Itakuwa si vizuri.

Rais. Rais apewe miaka mitano, five years. Ikiwa atakuwa mzuri, au mbaya after ten years, aende akapumzike. Councillors na MPs, wasichaguliwe wakiwa na chini ya form four level.

Ministries. Rais asichaguwe waziri ambaye hajahitimu na wizara hiyo. Ikiwa rais atamchagua waziri wa elimu, ni awe amesomea mambo ya elimu, ili aweze ku handle walimu kwa njia inayofaa. Na ikiwa ni upande wa health, awe amehitimu kwa upande wa udaktari, ili aweze ku-manage hiyo wizara vile inavyostahili. Waziri ni apewe mamlaka kamili, ya kusimamia wizara yake. Ikiwa ni mkutano uko mahali fulani,waziri ni aende kwa huo mkutano na PS wake; wakajadili kile kinachoendelea halafu watuletee report. Sio kuna mukutano wa malaria ama wa ukimwi halafu rais aende. Hana elimu ya mambo ya malaria, anaenda kusema nini huko. Waziri aende yeye mwenyewe, amalize, arudi. Waziri wasipewe transfer ovyio ovyio; baada ya mwezi moja, ametolewa hapa, amewekwa pale, baada ya miezi mbili ametolewa pale, atafanya kazi siku gani? Akipewa wizara ni ai-manage kwa muda wa miaka mitatu ama miaka mitano yote, unless pawe na shida fulani sisemi akae pale ikiwa hafaii, lakini awe anapewa wakati mzuri wa kufanya kazi katika ile ministry.

Ma-judges na attorney generals. Wawe wakipewa promotion na Public Service Commission. Sio rais achague mtu amweke pale, halafu akae pale mpaka afe, ama a retire. Ni kuwe na utaratibu fulani wa kuwapaatia promotion, ili wafike kiwango hicho. Rais awe anaweza kushtakiwa hata akiwa rais. Awe anaweza kushtakiwa kama mwananchi yoyote yule, sio aachiliwe pale aendele kudhulumu watu, mpaka siku ile atafutwa kazi, haifai hiyo. Chiefs, assistant chiefs waajiriwe na serikali, lakini wapewe transfers. Anaweza kuajiriwa hapa Marafa, na apewa transfer aenda akafanye Taveta; kama vile ma DO wanafanya kazi, sio lazima akaishi hapa.

Kwa upande wa county council, wapewe mamlaka ya kufanya developments iwe county council mahali ilipo inaweza ku-develop mahali pale pale na zile pesa wako nazo. Na watengwe pesa za kutosha na serikali, wafanye maendeleo ya sehemu zao.

Nominated MPs. Ikiwa mtu amegombea kiti na ameshindwa, inamaanisha ya kwamba mwananchi amemkataa, asichaguliwe na rais. Ikiwa ni lazima kuwe na nomination, rais achague mtu mwingine ambaye hakusimama kabisa; kwa sababu yule aliyesimama tumemkataa, wewe unamchukua umpeleke huko, anakuja kufanya kazi na nani? Nominated MP, he does not represent anybody, kwa hivyo hastahili kupewa ministry; ni awe MP tu, kwa sababu sisi hatukumtuma, wewe ndio umemuita huko. Kwa hivyo hakuna haja apewe wizara. Nominated MP asiwe vice president awe MP peke yake mpaka miaka mitano,

halafu aondoke. Nafikiri ni hayo tu. Asante.

**Com. Abida:** Asante, jiandikishe hapo, Bwana Vincent Nyawa.

**Vincent**: Kwa jina mimi naitwa Vincent Nyawa. Mengi niliokuwa nayo, naona yamezungumzwa.

**Com. Abida**: Yazungumze tena kuyatia mkazo, hakuna wasiwasi.

**Vincent**: Okay. Ya kwanza ni hii mambo haya mila. Maoni yangu ni kwamba mila itiliwe mkazo sana. Kwa sababu kuna msemo unaosema, "asiye na mila ni mtumwa". Na kama mila itatiliwa mkazo, basi tukija upande wa kuoana: ingawa wengi wamesema mali iondolewe lakini mali ni kiunganisho kati ya babake msichana na wazazi wa bwana. Kwa hivyo mali ni kitu muhimu sana, kwa hivyo mali iendelee kutolewa. Lakini, mali ya siku hizi imezidi sana, na imezidi kwa sababu, yule anayetoa hiyo mahari, ni upande moja: upande wa bwana. Maoni yangu ni kwamba, hii mahari ipewe msichana na bwana yake. Kwa hivyo, hizo pande zote mbili; wenye msichana na wenye mvulana, watoe nusu. Hili jambo ni muhimu sana. Hili jambo ni muhimu sana tukikuja wakati wa divorce, kwa sababu, watoto watagawanywa sawasawa. Nusu waende kwa mvulana na nusu waende kwa msichana.

Hali ya kuridhi. Msichana ana haki kabisa ya kuridhi, sawasawa na mvulana; kwa sababu mama amechangia na baba amechangia. Kwa hivyo mali ya baba ni sawa msichana apate haki yake, na mvulana apate haki yake.

Kuna hii malu. Tumezungumza mambo ya malu hapa, lakini kuna malu aina mbili. Moja ni mbaya kabisa ni maoni yangi itolewe kabisa, lakini kuna malu aina nyingine, ambayo ni maoni yangu iendelee. Malu ya kwanza ni hii ambayo ni punishment, mtu akizini na bibi wa mwenzake. Ikiondolewa hii ndio nimewambia wale wazinifu waendele kabisa; na hiyo itaendeleza hii mambo ya magonjwa; Kwa hivyo hii malu ya aina hii iendelee.

Ya pili ni hii malu ambayo bwana amekosa na bibi yake, kiwango cha ku-divorce. Bibi anakuja nyumbani, lakini kwa sababu hamkumshika sikio, kuna ile mila ya kumshika sikio bibi, na kumpeleka kwa babake; amwambie, "mimi mtoto wako sina haja naye, nitafutie mali yangu, atafute bwana mwingine". Kama bwana hakusema hivyo, na msichana hapo aamue akaolewe na bwana mwingine, huyu bwana wazamani atakuja atamwambia yule baba: "sasa nitafutie mali yangu, tena na malu, umemchukua msichana, ukampeleka kwa bwana mwingine". Malu hiyo haina maana; mtu apatiwe kile chake alichotoa, siyo interest juu yake. Kwa hivyo malu haina maana kabisa, itolewe.

Pili ni umilikaji wa mashamba. Kuna hizi sheria za mashamba, ambazo zilifanyika hapa Pwani, ambazo zinasemekana ni za Mazrui. Hii mambo ya Mazrui na hizi coastral treaties, mimi niliyasoma katika history; sijui kama ni ukweli, lakini mimi naona kama ni urongo. Kwa sababu; ni Mwafrika gani wakati misukosuko ya slavery, ni wakati gani Mwafrika alizungumza na

Mwarabu mpaka kukawa na sheria hizi za mashamba? Hizo ten miles kutoka baharini kuja upande huu, si za Waarabu. Mimi naonelea, kuwe hakuna mambo ya ten miles, kila mtu agawanyiwe shamba pahali aliko na title deeds zitolewe. Maanaake, watu wote, ni wa Pwani. Na hizo title deeds za wakati huo, bado zinafanya kazi mpaka dakika hii? Kwa hivyo kama title deed za baada ya independence; zitolewe, lakini siyo hizi title deeds za pande hiyo. Na kuna hii transfer of land. Kama mtu amenunua shamba ile harakati ya ku-transfer irahisishwe kabisa. Hata ikiwezekana ofisi za tume ya mashamba ziletwe kwenye district level. Ili haya mambo ya mashamba-na iwe na kila kitu kabisa, title deeds, survey, makaratasi yote yatengenezwe tayari, mtu anapata title deed yake. Siyo iende mpaka Nairobi, inaenda kukwama kabisa,, mpaka title inapotea namna hiyo.

Kuna hii sheria ya rais ako juu ya ya, ya sheria. Hii sheria imetumia vibaya, kwa muna mwingi sana. Sheria hii imefanya hata marafiki wa president, relativesna even tribes zikuwe above the law. Maanake kama mimi ni rais leo na hapa kuna rafiki yangu nikiwa niko above the law, hata rafiki yangu inakuja automatic atakuwa above the law. Kwa hivyo, hiyo sheria iwe scrapped off kabisa. Na kila mtu kulingana na matendo yake ahukumiwe hivo hivo tu.

Huko mahakamani kuna maneno mengi sana yanayoendelea. Mtu anashtakiwa lakini haya pia yamezungumzwa tayari. Kuna haya mambo ya free bond, mtu akipelekwa mahakamani na bado hajapatikana na makosa fulani, mbona awekwe rumande? Huyo mtu huko ndani atakonda na hata zile nguvu zake za kuzungumza wakati wa kesi, hatakuwa nazo. Na yule mwingine kule njeanaendelea kula vizuri, wakati wa kesi ukifika, yeye yuko very strong; anatoa point zake vizuri. Lakini yule aliyetoka remand akija anaonekana mnyonge, basi inasemekana yeyey ndiye mrongo. Kwa hivyo hizi free bond ziwe zinatolewa tu, so long as, baado hujapatikana na makosa.. Mambo ya kuwekwa ndani, yani mambo ya kuwekwa hiyo remand iondolewe.

Kuwe na government lawyers: maanake utamkuta tajiri, yeye anasimamiwa na wakili. na maskini anajitegemea yeye mwenyewe, hajui chochote, hajui chochote mambo ya sheria; anazungumza na hapa na mtu ambaye ni kazi yake kabisa, kugeuza urongo uwe ukweli, unaona! Sasa akizungumza na yule mtu sana sana, tayari yeye, mbele ya mtu ambaye ni professional tayari anaonekana mrongo. Kwa hivyo kuwe na government lawyers, ambao watawasimamia wale watu maskini, ambao hawajiwezi.

Lingine ni upande wa local government. Ma-mayor na ma-council chairmen wawe elected directly by the people. Na madiwani, wawe at least wana certificate ya form four, maanake kuna huku ku-reason pia. Mwenzako ametoa hoja muhimu, wewe hauitaki na huna hoja nyingine ya kumpinga; mwisho ni kutumia nguvu na mnapigana. Lakini at least akiwa amefika form four and above, atakuwa an reasoning power. Kunatakikana pia kuwe na sheria ambazo zimewekwa kwa madiwni. Madiwani inatakikana kabisa wawe kama maofisa wengine, wawe answerable kwa kila kitu ambacho watafanya; na kama wako division wawe answerable to the DO: kama wale ma-officer wengine, wawe chini ya DO kabisa, na wandike report ya ile kazi wanafanya. Lakini utakuta leo diwani amemwambia mtu fulani nitakupatia plot-wanzo hiyo plot ni yenu kabisa-lakini amekwambia kwa mdomo, kesho anakupokonya; anampatia yule ambaye anajua yuko nyuma yake. Huna pahali pa kumpeleka, sababu alikwambia na mdomo na hakukuadika; kwa hivyo wawe na reports.

Na zile projects ambazo hii local government itaanzisha iwe inanazisha, project kwambatana na matakwa ya wananchi. Kufafanua hii, ni kama project ambay0 imeanzishwa kijiji nina hiyo local government iwe kabisa wameenda kule wame-research ni kitu gani mnataka? Wazungumze na wananchi kabisa, wawaeleze wanataka nini. Mnataka serikali hii ya wilaya ama serikali ya mtaa imfanyie nini? Tunataka choo, lakini sio kujenga choo na hakuna mtu anayeingia huko. Kwa hivyo iketi na watu kabisa wajue watu wanataka nini. Sio kumletea maendeleo ambayo hata haitamfaa. Ni hayo machache sina mengi.

**Com. Abida**: Asante, jiadikishe pale. Tuna William Kaingu.

**William**: Mimi kwa jina naitwa William Kaingu, na nina mambo mawili tu ya kuzungumzia. Jambo la kwanza ni kuhusu uraia. Katika maoni yangu ningependa uraia upewe yule mzaliwa wa hapa. Sio mtu atoke nchi za nje, awe anaweza kufanywa kama ni raia wa hapa Kenya. Mimi katika maoni yangu, nataka rais awe ni mzaliwa wa hapa. Katiba maoni mengine pia ningechangia yakwamba, mbali na raia kuwe na kitambulisho. Pia nina maoni ya kuwa raia wa Kenya awe na passport ili angalau ikiwa anahaja na kuruka nje awe anaweza kwenda. Pia raia apewe makao kwao kule mkoani, sio raia wakutoka, kwa mfanao Kangundo, aje huku Marafa halafu acclaim hapa ni kwangu. Tunataka raia ni yule ambaye anapatiwa makao huko kwao, ndiyo maoni yangu.

Maoni ya pili ni usalama wa taifa. Vikosi vya usalama viundwe na Katiba. Tena katika maoni yangu vile vile ni kwamba, rais awe amiri jeshi mkuu wa majeshi ya silaha. Kwa mfano ikiwa kutakuwa na kikosi kingine ambacho kitakuwa kina uhuru wa kutumia siasa, ndio tuanona, hata mara kwa mara, kuna vita, lakini ikiwa rais peke yake ndio atakuwa amiri jeshi wa hizo silaha zote; mambo kama hayo yanaweza kupungua kidogo. Pia katika usalama wa taifa, mtu akikosa nidhamu, pengine mtu amue mwenzake, pengine amelewa, mtu kama huyu pia anastahili auwawe. Ni hayo tu kwa leo.

**Com. Abida**: Asante. Jiandikishe pale. Simeon Karisa? Charo Mako?

**Simeon**: kwa jina naita Simeon Karisa. Mimi maoni yangu kuhusu uraia, vile watu wanavyoweza kuishi; waishi bila kubaguana, ili kuwe na utaratibu mzuri kwa kila moja, ampende mwenzake. Hiyo inajumulisha katika upendo kwamba, mtu ampende mwenzake, kama anavyojipenda mwenyewe. Hilo ni jambo ambalo linawawezesha wanadamu, au watu wote katika nchi wawe na hali iliyo nzuri.

Lingine ni kuhusu elimu. Hii elimu ni ya muhimu kabisa. Hiyo ndio kama usukani wa wanadamu wapate kujiongoza katika kutawala kwao. Lakini, inakuwa, ni vigumu wengine kufaulu kwa sababu ya upungufu wa fedha. Na hivyo, ni maoni yangu kwamba, ile fees au karo, iondolewe, watoto wasome, waendelee mpaka university. Maanake hiyo itawezesha wapate elimu na wajitawale vizuri. Maana pasipo elimu, hawataweza kujitawala vizuri. Hayo ndio maoni yangu machache.Mungu awabariki.

**Com. Abida**: Asanti. Charo Mako? Kingi Jefa?

**Kingi**: Jina langu ni Kingi Jafa, mkaaji wa hapa Marafa. Maoni yangu juu ya wa ardhi. Ardhi, kusema ukweli, imesimamia na county council. Huyo ndie mdhamini wa raia wote. Lakini tumepata kujua kwamba katika hali ile ya usimamizi. serikali inaweza kuleta mtu, kwa kumtuza, sehemu ile. Sasa kama mtu anataka atuzwe na serikali, mara nyingi huwa analetwa tu, hawajali kwamba pale mahali kuna watu, ambao wao ndio wanaweza kumiliki ile sehemu. Kwa sababu hiyo, sisi tunasema, wale raia ambayo watakuwa pale, wanze kutambuliwa atambuliwe yule raia, agawiwe kipande pale pale, halafu sehemu zingine kama hawezi kuimiliki; pengine aweze kupewa yule ambaye atatuzwa. Hivo, hivo katika usawa wa kibinadamu, tunaonelea kwamba hii adhi, mara nyingi huwa inapewana kutoka headquaters Nairobi. Utapata ya kwamba raia ambaye yuko chini kabisa, akienda ma ofisini huwa anatupwa pale, na pale bila kujua mahali ambapo atapata karatasi, pia na yeye aweze kumiliki haya mashamba. Mimi naonelea, Katiba isimamie kabisa raia wa chini. Yeye aweze kupata uhaki, hata kama ni maskini wa aina gani. Tajiri asiruhusiwe kuchukua ardhi, halafu aanze kusukuma mwenyeji wa pale au mtu ambaye hata hajui mahali kwa kwenda abako yeye ataweza kupata shamba jingine. Kwa hivyo Katiba izuie tajiri asinyang'anye maskini.

Vile vile kuna huu utamaduni wa ndoa. Utamaduni wa ndoa huku kwetu, ingawa tayari imeshaelezwa, utapata kwamba mvulana na msichana wanasikizana; lakini baada ya kusikizana, hawa watu huja saa zingine wakakosana. Wakati wamekosana, hufikia kiwango kwamba, pengine waachane; kule kuachana, kusiwe Katiba isimamie kwamba wasiwachane kwa urahisu ule. Kuwe na wazee ambao watasimamia hii ndoa, wahakikishe ya kwamba ile ndoa itadumu, ili kuhakikisha ndoa inadumu. Isije ikatawanyika kwa sababu ikifanya hivyo, basi utaona ya kwamba, ndoa ile inakaa hali ya kiholelalela, haina usimamizi wa kutosha.

Vile vile nikirudi upande wa usimamizi wa huduma za mashamba hasa makaratasi, tunaona ya kwamba raia wa huku chini kupata karatasi hadi waende Nairobi. Ningeomba Katiba ichukue zile office ambazo zinahusiana na mashamba, ziletwe mpaka wilayani. Tukisema mkoani, bado ni mbali, kwa sababu mwananchi wa kawaida hana nauli ya kufika hata pengine Malindi. Kwa hivyo, hiyo Katiba iseme kwamba, serikali ilete ofisi mpaka hapa Marafa. Kiwango cha divisional level, ili mwananchi asitapetape kutafuta title deeds mbali.

Na vile vile kwa upande wa elimu. Mimi nasema ya kwamba hii elimu kwanzia kidato cha kwanza, form one hadi university iwe ya bure. Kwa sababu tuanona wazazi mara nyingi, hua viwango hivyo vya elimu, wanatapatapa ziadi, watoto wengi wanarudi kuchunga mbuzi mashambani.,Watoto maskini hawana nafasi ya kusonga mbele na elimu.

Mahakama. Mahakama tumepata kuona ya kwamba kuna mchezo ambao unafanyika. Mtu anaweza kuwa na makosa, lakini wakati polisi wanapigiwa ripoti au mahakama, utaona hiyo kesi inazungushwa zungushwa hivi hivi hakuna nafasi ya hiyo kesi kuendelea. Inachukua muda mrefu sana. Sasa hizi mahakama, Katiba isimamie, bunge iruhusiwe isimamie mahakama: kesi zisikawie zaidi ya miezi mitatu bila kuamuliwa. Kwa sababu ikiwa muda uitazidi sana, yule ambaye ni nimnyonge hatakuwa na la

kufanya. Kwa hivyo Katiba isimamie hapo. Kwa hayo machache, nasema shukrani.

**Com. Abida**: Asante. Paul Mwambime, Dama Karisa, Dama Karisa, haya njoo mama uzungumze. Ndiyo huyu? Huyu ni Dama Karisa? unaitwaje?

**Dama**: Mimi nilikuaa

**Com. Abida**: Jina mama, Jina.

**Dama**: Jina kwangu ni Dama Karisa (not clear)

**Com. Abida**:Wataka kuzungumza kigiriama? Haya (not clear) (interjection)

**Interpretor**: Jina langu naitwa Dama Karisa. Mimi nataka kuzungumza machache lakini naomba serikali, watu wote waliye kuja muniiwe radhi kuwa yale nayotaka kuyazungumza. Sina mengi. Mimi sijazungumza hapa awali. Leo hii ndio naanza kuzungumza kwa hivyo nitazungumza machache tu. Katiba inisaidie mimi, Katiba inipende.

**Com. Abida**: Asante Dama, Naomi Mkane? Joseph Wanje Ziro, Joseph? Adrea Kahindi, Nani huyu? Paul Mwambime, yuko wapi atasubiri?

**Andrew Kahindi**: Kwa jina naitwa, naitwa Andrew Kahindi Mudenge, na ni naishi hapa Marafa. Maoni yangu ni juu ya elimu. Serikali inahimiza kwamba wavulana na wasichana wapate elimu pamoja. Lakini shida ambazo tunazikumba hapa Magarini ni kwamba wale wasichana wakifika darasa la form three, wanadanganywa na wale wavulana na wanatiwa mimba pale kwa shule. Mkiwafuata wale wavulana, wanasema "mimi huyu simtaki" lakini tunakumbwa na shida sana kwa sababu, sisi tunajitolea hali na mali; lakini wale watoto wetu wa kike, hawazingatii yale masomo, kama vile kama tunavyotaka. Kwa hivyo sijui wale wavulana, wakiwa wamefanya hivyo serikali itachukua hatua gani? Kwa sababu wale watoto wanasoma pamoja, na wavulana wanawaharibu wale wasichana. Kwa hivyo serikali ichukue hatua. Kama yule mvulana amemtia mimba yule msichana, hata bibilia inasema mtoto akifanya hivyo, amuoe yule.Sina mengi, ni hayo tu kuhusu wasichana wetu.

**Com. Abida**: Asante. Paul Mwambire?

**Paul Mwambire**: Majina yangu ni Paul Mwambire. Natoa maoni ya kibinafsi. Mimi ningetaka kwanza kugusia sehemu ya Katiba kwamba, hata mimi naunga mkono kwamba, Katiba iwe na utangulizi; ili tupate msimamo mzuri, na kuonyesha mwelekeo wetu, katika ule utangulizi. Halafu baadaye ndio tutapata mwongozo namna tutakavyo endelea.

Na pili, kuna sehemu ya elimu. Huku kwetu, kulingana na mazingira yetu, ni kwamba, elimu iko chini, na ningeomba; kwa sababu tukilinganisha na kwingineko taifa, katika kwa upande wetu tunaona kwamba elimu iko chini. Nataka kuwe na sehemu fulani ya Kiserikali, elimu iwe ya bure, serikali iingilie, isaidie vijana wa kike nawakiume; wasome katika shule za msingi, secondary, hata vyuo vikuu. Serikari igharamie kwa sababu mapato yetu huku, yako chini.

Kuhusu ardhi. Ardhi tunayo, lakini umilikaji wetu, katika sehemu yetu hii, hasa ya Marafa, ni kwamba, tuko katika settlement. Lakini tunavyo ona ni kwamba, watu wengi katika sehemu zetu za Marafa, watashindwa kumiliki ardhi, kwa sababu iko ghali. Ploti moja ni shilingi elfu sabini na tano na mapato ni chini. Mimi ningeomba serikali iingilie, kwa sababu ikiwa ni makao, basi uliyempatia makao, ni mtu amabaye hana, kwa hivyo tumepewa makao, kwa hivyo serikali itugharamie. Hapo mwanzo kulikuwa na mpango mzuri wa kusaidia watu. Sasa hatuoni, ndiyo tunataka iregeshwe ili kwamba wale watu ambao wamepatiwa makao, wasaidiwe hadi wapate zile title deeds. Hiyo itakuwa imewasaidia sana, na hapo bado twaweza kuinuka.

Nataka niingie sehemu ya utamaduni. Utamaduni kikwetu, Kigiriama kuna mambo haya ya uridhi na ya kuowana. Mimi ningeomba kwamba, sehemu zile za utamaduni ambazo zimepitwa na wakati, kwa sababu tumechanganyika tuko watu wengi, tumepata kuingiliwa na elimu mbali, mbali, ambayo inatusaidia; na kuilimwengu kwa jumla. Lakini kuna sheria nyingine katika kiutamaduni ambazo ni muhimu; zidumishwe, na ziwekwe katika Katiba. Kwa mfano, haki ya kuolewa. Naona hiyo ni muhimu sana, hizi ndoa za kienyeji ambazo zinafanywa na baba na mama, baba kwa mtoto an msichana, zikubaliwe. Wakati wameona, wamemaliza ndoa, labda waende kama ni kwa assitant chief, wapewe kile kibali, ile marriage certifacate. Maanake watu wengi huko wanaoana, lakini hawana vyeti. Kwa hivyo inabidi waenda kwa wakili, ama kortini na mimi naona hiyo si sawa. Ile marriage act ikubali ndoa za kitamaduni, ili zikimalizwa na zimesimamiwa na wazazi, basi wakapewe vibali, ili waweze pia nao kuendelea. Vile vile kuhusu hapo ninaona kuna shida ambayo ningetaka kuisema kibinafsi. Siku hizi kuna janga hili; la ukimwi na ninaomba kwamba, watu wakiwa wanaoana, iwe ni sheria kwamba, wale wenye kufunga ndoa wa wachunguzwe ithibitishwe kwamba hawa si wagonjwa wa hii aids, ili waweze kuona. Maanake kuna ndoa zingine zinaendela hivi hivi, na hiyo inaweza kuleta shida ama hata kuangamiza taifa. Kwa hivyo naona hapo ni sehemu muhimu ambapo nataka nipataje.

Mwisho ningetaka kusema hivi. Kulingana na uakilishi wa kisiasa, mimi ninaunga mkono serikali ya majimbo. Tuweze kuwa na majimbo yetu, tuwe na bunge kuu, na bunge ya wawakilishi katika sehemu za mikoa. Pili, ma-councillor vile vile, wajumbe wawe na kiwango fulani cha elimu: kwa sababu tumefika wakati ambapo wale wanaowakilishwa wamesoma. Lakini kuchagua mtu ambaye hana elimu labda ni pesa tu, utajiri, halafu anadanganya watu, kwa sababu ya pesa: ningeomba hivi, councilor, angalau mwisho kabisa qualification zake kielimu, si kupita kiswahili na kingereza pekee ile sijui ni language test, lakini awe amesoma amefika kidato cha nne na angalau ana mean grade C-. Awe councillor huyu. Na ikiwa ni mujumbe, elimu yake ya chini iwe diloma, au degree, kuendelea mbele. Kwa sababu watu wanaowakilishwa, wamepata kusoma. Asante sana.

**Com. Abida**: Manyeso Katana, John Kalama, Katana Menza, Gumbao Nyanje. (interjection)

**Gumbao Nyanje**: Mimi naitwa Gumbao wa Nyanje. Lengo langu la kusimama hapa lahusu ulimwengu wa kileo. Kuhusu sehemu ya uchaguzi, mimi maoni yangu ni Chief apigiwe kura, diwani apigiwe kura, na kila kiongozi apigiwe kura, Mzee wa kijiji apigiwe kura kisha na apate mshahara kwa sababu wanfanya kazi nyingi. Kina mama pia wanalalamika kwa sababu kimila mtoto ni wa babake sio wa mama. Maanake bwana ametoa mahari, bibi hakutoa kwanini achukue mtoto? Wakiendelea kugawa watoto watawachilia wazurure, na ugonjwa wa ukimwi ndio huo umeingia (kicheko na makofi).

**Com. Abida**: Rogers Ndoro, endelea.

Rogers Ndoro: Kwa majina naitwa Rogers Ndoro. Maoni yangu ni mawili tu. Umilikaji wa raslimali. na mfumo mwingine ambao tungetaka pengine Katiba ijayo iwe itaweza kuwakilisha ni Katiba ya majimbo.

Upande wa umilikaji wa raslimali kuna matatizo watu wa sehemu hii wameweza kupata. Tukiangalia tunakuta ya kwamba, raslimali za huku ni hafifu sana. Serikali ya sasa, sijui pengine ni kwa sababu iko mbali na sisi sana, ama ni namna gani. Lakini kama pengine ingekuwa na nafasi ya kuletwa karibu zaidi na ije iweze kuangalia, ingeweza kuruhusu hata pengine kitu kama, uchongaji wa mbao, kwavile hakuna raslimali zingine ambazo pengine zinaweza kuleta manufaa huku.

Sehemu nyingine ambayo ningetaka Katiba ijayo iwe itashugulikia, ni juu ya mamlaka ya rais. Mamlaka.ya rais yapunguzwe, rais awe pia anaweza kufikishwa mahakamani; ili kuwe kutakuwa na haki katika utekelezaji wa sheria: yani sheria iwe itakuwa haipendelei mtu moja, na vile vile kutazuia raslimali zote kuwa zitawekwa pahali pamoja, halafu zote ziwe zinaangaliwa ni mtu moja. Raslimali hizi tuseme ni kama, the consolidated fund, hazina kuu ya kitaifa, iwe itaweza kugawanyiwa majimbo tofauti, tofauti; kuliko ile ya sasa ambaye inawekwa mahali pamoja, halafu ndio inaleta vitu kama sasa, imefika wakati wetu, kabila hili tumpeleke huyu akale, kabila hili tumpeleke yule akale. Vitu kama vile, tukiwa na serikali ya majimbo nafikiri vitaisha vyenyewe: kwa sababu vitu kama kodi zitakozakuwa zikikatwa kutoka kwa raslimali zile ziko kwa majimbo, zitakuwa ni sawa zibaki katika yale majimbo ili ziweze kusaidia miradi ambayo iko katika majimbo yale, na ilete manufaa kwa watu wa jimbo hilo.

Kitu kingine ambacho pengine ningetaka kugusia pia ni kuhusu elimu. Ukiangalia mfumo wa sasa wa elimu, unakuwa na gharama kubwa sana; na gharama hii inaletwa na kwamba wengi wa wale ambao wangaliweza kufaidika katika mutindo ule, hawana zile raslimali, au zile pesa za kugharamia mfumo ule wa elimu sasa. Kwa hivyo elimu kama ikiwezekana, iwe ya bure. Pengine hata university. Lakini ya msingi, kama ninavyojua, imekuwa ni sheria tayari. Tungeomba hiyo Katiba, itakayokuja ihakikishe ya kwamba itakua sheria elimu iwe ya bure, pia kuanzia, form one mpaka pengine form four. Hata ikiwa itakua si ya bure, kuwe kuna ugawanyaji wa gharama. Serikali ina gawa, ina gharamia nusu, na wazazi ama wale wahusika wengine pia wawe wana gharamia nusu. Maanake ukiangalia kama, itakuwa inaendelea jinsi ilivyo, basi pengine miaka kumi ama miaka ishiririni ijayo kutakuwa na kutokuwa na usawa wa kielimu katika taifa letu.

Wale wenye raslimali za kutosha; na ni nikisema raslimali za kutosha yale maeneo ambayo, yana bahati. Kunakuzwa vitu kama

kahawa, miwa, maua, vitu kama hizo ambazo pengine kuwa maeneo mengine, nikitaja kwa mfano eneo hili la Pwani na eneo la Kaskazini Mashariki, vitu kama vile hakuna. Kwa hivyo gharama ya kugharamia elimu kule inakuwa ni tatizo kwa wale ambao wanahusika. Kwa hivyo elimu pia katika Katiba ijayo, iwekwe hali ya kwamba itakuwa ni ya kugwanywa au iwe ya bure kabisa. Ni hayo tu.

**Com. Abida**: Kazungu Tubu? Kuna mzee anaitwa Kazungu Tubu hapa, ambaye anataka kuzungumza? Rachael Mtengo. Diramu Charo, Kazungu Kombe, Festus Iha, Alphonse Karisa, Emmanuel Gonzi, Anderson Mae Kitsao, Philip Kalume, Julius Kombe, Sammy Charo, John Kombe Katana, Karisa Ngala. Sasa tulikuja kuangaliana ama kutengeneza inchi jamani? Dawo Kitu, Joshua Kazungu, Mwangandi Nguzo, Rogers, Bwana DO sijui tufunge mkutano? Kadenge Koi, Katana Kitsao?

**Com. Abida**: Bwana Do sijui tufunge mukutano. Kadenge Koi, Katana Gitau, Garama Karisa, Kahindi Karisa, Mzungu Ngoma, Charo Ndiso, na haturudi tukimaliza, Jina lako basi. kwa sababu lazima tufunge mkutano kufikia saa kumi na moja. Tukitaja jina, hukuitika, hatutarudia tena tafadhali. Charo. Wewe ni nani? Mzungu Ngoma.

**Mzungu Ngoma**: Kwa majina mimi naitwa Mzungu Ngoma na ninashukuru kwa kupata nafasi hii; ambayo ningetaka kuongea juu ya Katiba yetu. Kwanza ningetaka kuongea juu ya sehemu ya elimu. Ninapendekeza kwamba elimu ipewe kipau mbele na ilipiwe na serikali; kwa sababu hata ukiongalia nafasi iliyopo ya makamishna ambao wako hapa, kuchukua maoni ya Katiba hii; ni kwa sababu ya elimu. Ndio ambaye imeweza kuwapa nafasi ya kupewa nafasi hii ya kufanya kazi ambayo wanaifanya. Kwa hivyo elimu ni uti wa mgongo kwa kila moja, na hakutakuwa na usawa kwa sababu, Katiba yetu lazima iwe na haki na usawa wa kila mmoja. Lingekuwa jambo la busara kwamba elimu iweze kupewa nafasi na igharamikiwe na serikali ili kwamba watoto; ama wale wote ambao hawa kupata elimu mapema, na wapate kuwa na elimu. Ili hata kesho labda wanaweza kupewa nafasi ya kushirikisha wanainchi kwa kuchukua maoni kama haya, ama kazi zingine zozote ambazo ziko za serikali. Kwa hivyo mimi sehemu moja abayo naiyangalia kwa muhimu sana ni elimu ipewe nafasi na serikali iwe itagaramia elimu. Ni kwanini? Ni kwa sababu, hata chochote ambacho kinaendelea fedha hizi zimekusanywa kutoka kwa ushuru ambao sisi wenyewe tunalipa. Na ushuru huu ambao umeweza kuwanufaisha makamishna kupata elimu, nafasi hiyo ipewe na wanainchi wengine wote ili nao waweze kupata elimu, na hivyo kuwa na usawa.

Jambo lingine ambalo ningetaka kuongea ni kuhusu ardhi. Ardhi ni sehemu muhimu sana ya maisha ya mwanadamu. Na kwa sababu ni muhimu tunaumuhimi wa kwamba kila mwananchi ya Kenya, Katiba yetu itoe nafasi kwamba kila moja aweze kupata ardhi, sawasawa na mtu mwingine. Sasa hivi hali ilivyo, haiwezi kutupa uhaki sawasawa na wananchi wote wa Kenya; kwa sababu wengine wetu wakubwa katika serikali, ama katika mashirika tofauti tofauti, wana ardhi ambayo ni kubwa kupita kipimo. Na ukiangalia kama sehemu ya Pwani, watu wengi wanaishi kama maskuata, na ni muhimu kwamba Katiba yetu iweze kuangalia kikamilifu, na ishugulike maana sisi wakati huu tunatengeneza ambayo yataweza kushghulikiwa hapo kesho. Kwa hivyo ardhi iwe sehemu moja muhimu ambayo kila mwananchi apate kipande cha ardhi, wala isiwe mtu moja ana ardhi kubwa kupita watu wengine.

Kuna ile sheria ya Wamazrui ambayo wanachukua sehemu ya maili kumi mraba katika mwambao wa Pwani. Hao, Wamazrui sio Wakenya peke yao. Wamazrui kwa kweli ni Waarabu. Na kule uarabuni, sasa hivi sheria hairuhusu kwa mtu mwingine ambaye si Muarabu kuweza kupata ardhi katika sehemu ile. Kwa hivyo kwa nchi yetu tulio Wakenya, sharti sisi tuweze kupata ardhi na isiwe kwamba mwarabu kwa sababu ni Muarabu, ati kwa sababu kuna makubaliano yaliyofanywa zamani ya maili kumi, wawe wao ndio wana ardhi hiyo yote.Kwa hivyo mim napendekeza kwamba, sheria ile ya kuwa waarabu wanachukua sehemu ya maili kumi iondolewe na Wakenya halisi walio wenyeji wa Afrika, kwa sababu hii ni territory ya Waafrika-Waafrika, wawe na ardhi kama watu wengine wowote.

Elimu, ningetaka kurudia kidogo, ni kwamba akina mama hasa kwa gender, akina mama wapewe elimu; kwa sababu tunasoma kwamba, mama anapopewa elimu, mama atamuelimisha kila mtoto anayempata. Kwa hivyo ni muhimu kwamba kina mama, infact iwekwe kwamba, itakuwa ni lazima kwa mwanamke yoyote anayepulia: apate elimu, maana kwa njia hiyo kama kina mama watapata elimu, tunauhakika kwamba watoto watakao zaliwa wataweza kupata elimu kama watu wengine.

Kwa hivyo, akina mama wapewe nafasi ya kwanza, iwapo ni katika bunge, na wapewe nafasi ikiwa ni sehemu ya elimu. Hivyo tutakuwa na uhakika kwamba, elimu itaweza kuwafikia wengine wote. Sehemu hiyo hiyo ya elimu labda ningechangia kwamba, kuna wale ambao wanafanya biashara katika mwambao, kama na wenye mahoteli, na wenye viwanda vya chumvi. Sehemu ya pesa ile ambayo inakusanywa na viwanda hivi vya chumvi, na wenye mahoteli; iletwe ilikuzijenga shule zetu, ambazo ziko huku rural areas:huko ambako ni mbali na sehemu ile ya mwambao ili kwamba mashule yaweze kujengwa vizuri, na watoto waweze kupata elimu bila shida yoyote.

Kingine kile ningetaka kuchangia ni utawala. Utawala ni shehemu muhimu sana katika maisha ya mwanadamu. Tumekuwa na utawala katika kila upande. Kuna machifu, na kuna viongozi wengine katika serikali. Kuna mtindo ambao umekuwa ukiendelea kwa muda mrefu. Viongozi, wana tabia za kuharibu kazi zao. Ikiwa mwalimu atafanya makosa, atatia mimba msichana katika shule ya Marafa, mwalimu huyu afutwe hapo hapo, wala asipewe transfer kwenda mahali pengine. DO akifanya makosa hapa, ikiwa atapatikana ameiba mahindi, ikiwa atapatika ame, labda amezini na bibi ya mtu, ameenda kinyume na zile sheria za kazi zake, DO huyo ama afisa wa elimu huyu afutwe papo hapo. Asipelekwe mahali pengine, maana imekuwa ni kuchukua ugonjwa wa kutoka hapa, na kuupeleka mahali pengine. Mara nyingi imekuwa kwamba mtu anapofanya makosa Marafa, anakuwa transferred anapelekwa Malindi, anafanya makosa Malindi, anakuwa transfered anapelekwa Kiambu, anafanya makosa Kiambu, anapelekwa transfer Kisumu. Hii ninacho ikielewa vizuri kuhusu Katiba; ni kwamba sasa hivi tunaweka msingi wa maisha yetu.

Fedha zinazokusanywa amazitakazo kusanywa kesho, zitategemea vile ambavyo tunaagana leo, ziende. Kwa hivyo fedha zote zitumike kwa njia ya uangalifu, na mtu anapofanya makosa katika eneo lake la kazi, na afutwe hapo hapo, wala asipewe transfer ya kwenda mahali pengine popote. Yako mengi, lakini kwa wakati singetaka kumuharibia mtu mwingine, apate nafasi

naye. Lakini mimi napendekeza kwamba tukumbuke kwamba fedha zote, hata wale makamishina ambao wako hapa, ni kutokana na ushuru ambao tumeulipa kutoka kwa mifuko yetu, ni kutokana na ushuru ambayo tumelipa sisi; ndio magari haya makubwa yako, na ndio kila kitu kinachoendelea, kinavyofanyika. Kwa hivyo tunasema, fedha ile inayo kusanywa kwa ushuru, itoe elimu kwa watu wote, ili sisi sote tuwe na nafasi sawa, na hata wale makamishna ambao wako hapa. Asante.

**Com. Abida**:Charo Ndiso, Nelson Mramba, George k. Kitsao, Peter Ziro.

**Peter Ziro**: Jina langu naitwa Peter Ziro. Niko hapa kutowa maoni ya binafsi. Katiba tuliyo nayo sasa haina utangulizi, na kwa hivyo mimi ni maoni yangu, kwamba tuwe na utangulize kwenye ile Katiba ambayo tunaiyounda. Na utangalizi ule nataka uonyeshe picha ya vile Wakenya wanavyo kusudia kushirikiana ama kuishi kama jamii iliyo na sera za pamoja katika serikali ya Kenya. Na ningetoa maoni kwamba iwe namna hii. In the name of the Almighty God, we the people of Kenya in recognition of the creation and guided by the independent constitution and the subsequent amendments thereafter resolve: to reconstitute Kenya in to a federal soverign democracy, to secure all it's citizens justice, liberty, equality, and fraternity. To recognize every individual's a dignified livelihood in appreciation of our diversity in our nation. Hiyo ndiyo napenda iwe utanglize.

Vile vile tungependa serikali ya sera ya majimbo. Na majimbo tunayoyataka ni kama yafuatayo. Tunataka mikoa iwe ndiyo jimbo. Ile mambo ya kusema kuna ten miles za sijui ni coastal strip, hiyo tusahau, kwa sababu ilikuwa ni pre-independence. Na maneno yale yaliyozungumziwa sidhani kwamba kuna mtu yoyote hapa, Miji Kenda, ama Mugiriama, aliye ulizwa maoni na wale Waarabu. Kwa hivyo hayo yasahauliwe na iwe kama ni mkoa wa Pwani uwe ni mkoa Pwani mzima. Kama ni Western Province, iwe ni Western province lakini sio kusema Pwani itagawanywa ten miles. Hiyo tusahau. Vilevile tukiingia kwa upande wa maofisi, tunataka serikali ama jimbo liwe linaendeshwa na governor. Regional Government: governor awe ana mamlaka ya kuhusu jimbo. Yeye atachukua mambo ya jimbo akayapeleka huko kwa cental government, azungumzie kuhusu shida za wananchi at regional level. Vile vile ofisi zile ambazo zinashughulikia matatitizo ya wananchi madogo madogo; kwa mfano kama vile mambo ya ardhi, ziwe mwisho mkubwa sana wakupata hati ya kumiliki mashamba, ni district level. Kwa sababu tumeona kuna shida kwamba ukiuliza, unaambia haya mambo mpaka Nairobi. Ofisi ya Nairobi haijakubali. Kumbe hata labda hayo mambo huwa yanakoseka hapa hapa, kwa hivyo tunataka iwe ni hapa kwa district level, ambayo ni Malindi kwetu sisi watu wa Magarini; ikiwa tunashida tunajua, tuanimalizia hapa hapa Malindi. Ile mambo ya kupewa sababu ya kwamba mpaka Nairobi, iwe imeisha.

Vile vile majimbo tunayotayataka, tunataka sehemu za kazi, ikiwa ziko, makampuni hapa Pwani, seventy percent, asilimia sabini na tano ya wale ambao wataandikwa kazi; wawe ni vijana wakutoka hapa hapa. Halafu ikiwa kuna nafasi zingine zingine, labda asilimia theladhini, tunaweza tukaruhusu watu wengine nao waje wajipatie makazi. Lakini sio kuchukua watu wa nje wachukue kazi zote, halafu vijana wa hapa wawe hawana kazi.

Vile vile tunaomba university au chuo kikuu kwa kila jimbo, Pwani iwe na university yake, kama ni Western, ni wapi. Sio

kuchukua vyuo vikuu vyote kupeleka Nairobi, mtu lazima atoke hapa aende Nairobi ama Eldoret ama wapi. Hapana. Kila jimbo liwe na chuo kikuu chake. Watu wawe wanaweza kupata elimu at regional levels, sio lazima wende mpaka Nairobi kule naitonal level.

Vile vile mali ambayo inatoka, ama ile revenue ambayo tunaipata hapa, iwe 60% inabaki kwa jimbo, halafu 40% inaenda kwa central government. Nikesema hivyo ni kwamba, yako mashirika tofauti tofauti, ama kampuni tofauti tofauti, ambayo yamefilisika hapa Pwani. Kwa mfano, mkoroshoni umeanguka, na kulingana na reporti iliotolewa, inahitajika million ishirini na moja kuwa revived, au kuletwa mtambo mpya kabisa, ambao utaanza kufanya kazi. Sasa ikiwa ile revenue inabaki hapa 60%, after sometime tunaweza kutuimia, kuangalia kampuni kama zile zimefilisika. Zaweza kurekebishwa, zianze upya tena kufanya kazi, na watu wetu wajipatie makazi.

Maoni yangu mengine ni kuhusu wakati bunge limevunjwa. Tumeona kuna shida kubwa, kwa sababu bunge likivunjwa huwa linakaa labda miezi miwili, au mitatu, kabla uchaguzi kufanywa na wakati huo hatuna rais, hatuna waziri, na hatuna members of parliament. Ni maoni yangu kwamba a special committee iwe formed, wakati bunge limevunjwa, kuwe kuna watu ambao wanaweza kusimamia miradi ya serikali kisawasawa. Sio rais yule ambaye amesema amevunja bunge, awe vile vile ndie anabaki kuwa rais, mamboyote anadelegate yeye. Katiba yetu inasema, the president is the commander-in-chief of the armed forces, na yeye ndiye ana right ya ku declare war. Je wakati bunge limevunjwa na yeye sie rais,kukianguka vita ni nani ataenda ku-declare war? Kwa sababu hakuna provision kwenye constitution ya sasa, kwamba chief of general staff anaweza ku-declare war, its only the president.

Kuwe kuna kamati maalum na ipewe uwezo wa kuendesha mambo, kama vile rais anavyoendesha. Vile vile nikirudi hapo, nataka, ama ni maoni yangu kwamba bunge kama limevunjwa, ikiwa wewe ulikuwa rais ama minister, usiruhusiwe kutumia gari la serikali yoyote, manake wewe si mfanyi kazi wa serikali tena. Kama tulivyo ona hiyo miaka ya nyuma ni kwamba hata bunge likivunjwa, utapata hata wale waliokuwa mawaziri badowanatembea na misafara ya magari ya serikali. Kama ni campaign zao watazifanya na magari yaserikali. Je wale ambao hawako kwa serikali, si itakuwa ni kama kuwaonea? Kwa hivyo ni maoni yangu kwamba, zile public resources, ziwe withdrawn completely from these people. Kama ni president awe hana chochote, arudi Murang'a kama Kamotho, na kama ni mimi nirudi hapa nikiwa Ziro. Hivo hivo, sina chochote, sina gari la serikali, kama nina langu nilitumie, lakini sikutumia gari za serikali.

Nataka kuingilia upande wa ardhi. Upande wa ardhi tuko na shida sana, kwa sababu wakati tulipochukua uhuru, tulidhani kwamba tunanyakua ardhi zetu. Lakini kumbe zile ardhi zilibaki kwenye mikono ya wale ambao walikuwa na nguvu. Leo hii, Kenya ina watu ambao wanamiliki ardhi kubwa kushinda wengine. Maoni yangu nataka kusema hivi; zile ardhi ambazo wale watu walizichukua wakati tukipata uhuru, ikiwa alichukua ardhi kubwa, ichukuliwe kutoka kwa huyo mtu, na igawanyiwe indeginous people, wale wanaoishi sehemu ile. Na kama alinunua labda kwa kutojua alindanganywa akaambiwa hii ardhi ni yangu, ki hivi na hivi. Serikali itafute mpango wa kumrudishia pesa zake, kama ni nusu, ama kama ni compensation kitu kidogo.

Lakini ile ardhi iregeshwe kwa wananchi wenyewe. Vile vile umilikaji wa ardhi. Wengine wana uwezo, na wengine hawana uwezo, siku hizi nasikia kupata shamba ni lazima ulipe elfu sabini; si kwamba hizo elfu sabini watu wameshindwa, lakini hata zile shamba zenyewe hatuzioni, na ardhi ni zetu sisi, lakini shamba hatuzioni. Kwa mfano, kuna watu wengine utapata hizo ploti ambazo zimegawanywa huko, zina majina ya watu ambao hata si wenyewe hapa, hatuwajui, na hatujui wameingizwa vipi. Na hii imekuwa shida kwa sababu zile kamati ambazo zinachaguliwa kusimamia mashamba, zinachaguliwa na watu ambao wanataka zitimize matakwa yao. Kwa hivyo ni maoni yangu kwamba, zile kamati zichaguliwe na wananchi wenyewe.

D.O. akija hapa, yeye ni representative wa serikali, hajui shida ambazo wananchi wa hapa Marafa wanazo. Kwa hivyo ni wajibu wa wanainchi wa Marafa wenyewe, waseme twamtaka fulani, asimamia mambo ya mashamba. D.O. awe kazi yake ni kuangalia hapa kuna shida, ama hakuna shida. D.O. asije hapa afanywe chairman wa mashamba, ama chairman wa bursary. Mambo ya shida za watu wa Marafa yeye hazijui D.O. akiwa transfered na yeye ndiye chairman, na signatory katika bank, akienda Murang'a tutatafuta tikiti twende Murang'a. Si hiyo pesa itapotea? Kwa hivyo ni maoni yangu kwamba, wale wachaguliwe na wananchi wenyewe ambao watasimamia mambo ya mashamba. Of late watu wamekuwa tu appointed labda mtu fulani kama ni chief, au D.O. anasema ita mzee fulani, wewe utakuwa kwenye kamati ya mashamba. Wale wakiitwa, wanaabiwa shamba hili, mpeni fulani, shamba hili mpeni fulani, hawatauliza kwa nini: kwa sababu anajua ameitwa na D.O. na amechaguliwa nahuyo D.O.; ama ameitwa na chief, na amechaguliwa na huyo chief. Lakini kama amechaguliwa na wanainchi, anajua mimi kesho nikifanya makosa kesho kutwa natolewa. Kwa hivyo hayo ni maoni yangu.

Vile vile machief wapigiwe kura kama vile viongozi wengine wanavyopigiwa kura. Ikiwa councillor anapigiwa kura, na anakaa tu kwa miaka mitano, je chief anayeka pale ziadi ya miaka ishirini, au miaka thelathini, kwa nini asipigiwe kura? Ni maoni yangu, wapigiwe kura kwa sababu kumekuwa na shida kubwa sana. Ikiwa wewe huelewani na chief, basi umekuwa mashakani for the rest of your life ama mpaka chief atakapo wacha kazi, ambayo sasa hiyo inatuumiza (makofi). Lakini ikiwa kama chief anaweza kupigiwa kura, atalinda ile posiotion yake anajua mimi nikifanya makosa, kesho hawa wananchi watanikataa lakini, ikiwa atakaa alivyo sasa, kama vile tumesikia wengine wanatia mimba watu, wengine wanakula mahindi, wanafanya nini, halafu anatolewa hapa, badala amefanya makosa afutwe kazi, anapelekwa Malindi, ati amepelekwa transfer. Hiyo mambo ya transfer haitusaidii na chochote. Tunataka mtu kama anafanya makosa anafutwa kazi, full stop. Hakuna cha ati aende, sijui wapi. Kampuni zingine huko nje ukifanya makosa unapatiwa warning letter mara kwanza, mara ya pili, hawasemi watakupatia transfer. wakupeleke mahali pengine, unafutwa kazi. Kwa nini serikali inapeyana ma-transfer kwa watu ambao wamefanya makosa? Wafutwe kazi. Hayo ni maoni yangu.

Upande ule wa ardhi vile vile, nataka niseme hivi. Nataka iwe ni provision kwenye Katiba kwamba yule mtu wa juu sana atakeyemiliki ardhi awe ana acari thelathini, na mtu wa chini awe ana acari tano.Na mtu akipita hizo acari thelathini aulizwe ama kuwe kuna provision kwamba anaweza kupelekwa kortini na akaulizwa hii ardhi ameipata kivipi. Tujue, isije kwasababu mimi niko kwa uwezo labda ni bunge ama ni councillra ama ni DO niwe naweza kuchukua acari mia mbili hapa Marafa na kuna mwenzangu hapa hana. Hiyo itakuwa ni maksoa. Kwa hivyo lile jambo lili lazima tuliangalie sana kwa sababu kumetokea

maonevu ya mara nyingi sana. Plot hata kwa trading center wanachukua watu wenye uwezo.Utakuta mtu ana ploti karibu tatu ama nne na kuna mwananchi pale na anataka lakini hawezi kwa sababu uwezo wake uko chini. That is unfair. Tunataka haki itendeke kwa kila moja kama vile tumesema wakenya sote tuko sawa kama, kama ni ploti zigawanywe kisawasawa.

Jambo lingine vile vile. Hizi ofisi ambazo ziko hapa chini kama vile ofisi ya lands, kama ni Malind au kama ni Mombasa tunataka ziwe zinakuwa run na locals wenyewe. Siyo mtu atolewe huko juu aje hapa ambaye hata ile lugha ya hapa hajui kama vile huyu mama ambaye alikuwa anazungumza hajui kiswahili. Kama hakungekuwa na Mugiriama hapa ambaye anaweza ku-translate akatwambia kiswahili si sote tungedangana. Lakini ikiwa nikienda kwa ofisi mimi Malindi ya lands nataka kuuliza kuhusu mambo ya mashamba siwezi kujielea vizuri kuhusu I mean kupitia kiswahili ama kingereza, naweza nikazungumza kinyumbani na mtu akanielewa tena nikapata masaad. Nafikiri hilo lingekuwa jambo bora sana. Kwa hivyo Katiba hii ambayo inadikwa iwe na provision hiyo kwamba pale ndani hata ikiwa kutakuwa na watu wengine abao watandikwa kazi, lakini kuwe kuna mtu wa area ile ile ambaye anaweza akasaidia hao watu locals ambaao labda hawaelewi ile lugha ya kiswhili na kingereza. Vile vile, nataka kumalizia ni kwa upande wa elimu. Elimu imekuja lakini sasa twambiwa ni free education lakini sii free education. Elimu iko na shida sana. Ikiwa kuna mpango ambayo inaweza kufanyika kuhakikisha kwamba watu wanapata elimu bila ya matatizo ifanyike. Nikikumbuka hapo nyuma Muheshimiwa Rais wetu alisimami akaseima kwanzia sasa elimu ni ya bure. Sawa, tunashukuru elimu ametangza ni ya bure lakini ziko shida ambazo tumezipata na yeye amesema ni ya bure. Mwisho tuanona elimu si ya bule, si ya bure lakini inakuwa ni gharama. Kwa sababu ukiangalia kwenye schools choki zenyewe lazima zinunuliwe na pesa. Rais amesema elimu iwe ya bure na wazazi wasitoe pesa. Je amafanya mipango gani ya kuonyesha kwamba walimu watapata choki? Manake saa hii wazazi wanarudiwa tena wachange pesa, wanunue choki na inasemekana elimu ni ya bure. Sasa ni bure gani hii ikiwa hata choki zenyewe hazipatikani? Vitabu havipatikani, lazima kuwe na provision kwa Katiba. Ikiwa elimu ni bure, everything should be provided for. Si waseme ni bure halafu baadaye warudie mzazi tena ambiwe changa, fanya kitu Fulani, fanya kitu falani. Hapana, this has brought a lot of confusion in the communities, walimu sasa wanateta na wazazi manake elimu ilitangazwa ni ya bure. Wazazi wamekataa kulipa pesa, kwa hivyo ikiwa itatangaza ni ya wazazi kuwe na provision na kuna pesa kiasi Fulani ambacho kitatengewa hizi shule.

Upande wa akina mama. Ni maoni yangu na vile vile maombi yangu, kwa sababu hata bibilia inasema wanawake ni watu wadhaifu. Tuwatambue kwa udhaifu wao, na tuzidi sana kuwasaidia, hasa kwenye nyadhifa za uongozi. Tunaona kwamba kina mama wanafinyiliwa sana. Ikiwa ni parliamentary seats, especially zile za nomination, ambazo rais anateua watu, kuwe kuna special provision, kwamba wengi wao wawe kina mama. Kwa sababu akina mama tukiangalia hata wale wanaogombea viti, huwa ni wachache sana. Hawawezi kusimama mbele wakazungumza ama hivi na hivi, kwa sababu wenyewe wanajichukulia wadhaifu. Lakini ikiwa kutakuwa na kipengle kwenye Katiba, kwamba baada ya election, kutachaguliwa akina mama nambari fulani ambao, watakuwa viongozi, watasaidiana na wamama wenzao.

Vile vile katika serikali wakati rais anapofanya uchaguzi wa mawaziri, ama kama ni kuteuwa watu wa nyadhifa mbali mbali, ningeomba usiwe uchaguzi wa rais peke yake. Iwe ni names zinakuwa floated, halafu zinakuwa debated in parliament, mpaka

wakubaliane kwamba; through veto, kwamba mtu fulani amekubaliwa kushika ministry fulani: ama mtu fulani amekubaliwa kuwa DC mahali fulani. Hapana president kusimama na kusema fulani aende awe minister, ama fulani aende awe kitu fulani, kwa sababu unakuta wengi wao waliochaguliwa kuwa mawaziri ni watu ambao hata kura zenyewe walikosa kwao. Wamekataliwe na wananchi, halafu akifika kule kwa sababu yeye anataka kufurahisha labda mtu moja au wawili, wanachaguliwa wanaingizwa pale ndani. Kwa hivyo ni maombi yangu kwamba, Katiba ambayo tunataka kuiandika saa hii, iwe na provision; kwamba watu kama hawa wapigiwe kura na paliament, kwa sababu paliamentarians tumewapa uwezo wa kufanya mambo on ourbehalf. Wawapigie kura, na wawapitishe, na hiyo nafikiri itakuwa ni sawasawa. Kwa hayo machache nasema asanteni sana. (makofi).

**Com. Abida**: Kwa kufikia hapa tuta ahirisha mukutano kwa nusu saa, na tunatumaini tukirudi hapo saa nane, kasoro dakika kumi na tano; tutaweza kupata watu wengi ambao watakuwa na maoni. Asanteni. Tuonaneni saa nane kasorobo.

**Naomi**: Majina yangu naitwa Naomi Justine Mukari. ni mama wa hapa Marafa. Nimezaliwa hapa, nimekuwa hapa Marafa, hata nimekuwa mzee hapa Marafa. Shida yangu ni kuhusu wazee, yaani wakina baba. Ni watu ambao wanawaonae sana hawa kina mama. Kuna mambo mengine ambayo nilikuwa nasikia ambayo yananihuzunisha sana, hasa ile hali ya kuchangia ule ugonjwa unaitwa ukimwi. Ni hao wazee ambao wanachangia huu ugonjwa, kwa sababu mzee moja, anaweza kuchukua wanawake kumi ama wanawake ishirini. Na hao wanawake hatawatosheleza wote mahitaji yao hata mahitaji ya kinyumbani. Kwa sababu mwanamke akitoka kwao anamfwata bwana, sasa bwana: yule akiwa ana mabibi kumi au mabibi ishirini, wakina mama wale wote wanaweza kutoshelezwa usiku moja ni bwana moja? Sasa wakati mwingine, hao wakina mama wote, wanawake kumi au wanawake ishirini, wanajengewa chumba kimoja, wanawekwa kama ni wagonjwa wako katika wodi. Sasa hawa wanawake ataona mama mwenzake hapa wanafanya mapenzi na bwana hapa, na yule mama akiona vile, ile tamaa na yeye itamzuka. Na wakati ule, hata kama sio usiku huo, kesho yake ataenda kutafuta mapenzi na bwana mwingine.

Sasa yeye akienda kutafuta mapenzi na bwana mwingine, anachangia ule ugonjwa, pengine yule bwana ambaye amepata kule nje, ana ugonjwa; na anarudi hapa, siku nyingine, yule bwana anapitia kwa kitanda chake. Akipitia kwa kitanda chake hatakomea hapo, anaenda kwa bibi mwingine, sasa yule bwana anapanda ule ugonjwa, hata watu wote katika nyumba ikiwa ni mabibi ishirini, ikiwa ni mabibi kumi, wote wanashikwa na ule ugonjwa wanakufa; wanaacha watoto mayatima wanapata shida, na shida hizo zote zinaletwa na hawa wazee. Basi kama kutakuwa na sheria kabisa, ambayo itakuwa hao wanaume, akionekana ana bibi watano, ashtakiwe. Maanake bibi yake ni moja tuu, sasa analete bibi wengi nyumbani na wanaanza kuchangia magonjwa ya ukimwi,magonjwa ya zinaa, magonjwa ya aina mbali mbali, anayaleta hapa nyumbani. Na wote wanakufa sasa wanaacha watoto.

Sasa watoto wengi wanashida kwa ajili ya hawa wazee hawa. Sasa hawa wazee kama kutakuwa na sheria ambayo inaweza kuwekwa katika Katiba yetu, mtu akionekana amechukua bibi wawili ashitakiwe. Akionekana na bibi watatu, ashtakiwe kwa sababu hawa ndio watu wanachangia hayo magonjwa. Wanaleta magonjwa hapa nyumbani, na watu wanakufa kwa ajili ya huyo mtu moja tu. Sasa huyo mtu mmoja basi asiwe na wanawake wengi. Kwa hivyo hiyo ni kwa sababu sisi wanawake

kuonewa nai hawa wazee. Wanatuonea, wanatuketia kabisa, hatuwezi kusema “bwanangu sitaki uwoe bibi mwingine”. Ukisema hivyo unaambiwa una wivu na bwanako. Mimi nikiwa na wivu na bwanangu hivo ni vibaya?

Kitu kingine ni hivi. Akiwa ni mtoto wangu anaanza kuchumbana na mvulana, wakati ule wa mahari, mimi kama mama ambaye ndimi nimezaa yule mtoto, siwezi kuongea. Ni yule bwana, pamoja na ndugu zake, pamoja na babake, watafanya mashauri ya mtoto wangu. Zile pesa ambazo watachukuwa, ni wao ndio ambao wataka kauli. Mimi ambaye nimebeba mimba miezi kumi, pengine nikabeba mtoto, hata mtoto akatembea, nikafanya kazi zote za mtoto, sina ruhusa ya kuulizwa wakati wanataka kuchukua mahari ya huyu mtoto.Sasa mtoto wangu anauzwa kama ng’ombe. Shida zote ambazo ateanda kuzipata kule, watu wamekula pesa, na akija hapa wakati mwingine anaambiwa rudi huko, kwa sababu babake na babu yake wamechukua pesa wakala; mtoto wangu anapata shida. Sasa na mimi mamake yule msichana ninasikia shida, kwa ajili mtoto wangu anapata shida. Watu wamekula mali, yeye anapata shida; na mimi nikiongea, nambiwa sistahili kuongea kwa sababu nimechukuliwa nami nimeolea sina amri. Sasa jambo kama hilo, wakina mama wanaudhika sana. Wa akina mama wana shida sana, wanakaliwa sana na wakina baba, kuwaonea kabisa. Hawana sauti yoyote kabisa.

Kitu kingine ni huyu mzee huyu. Huyu mzee ataenda huko kilabu, anaenda kunywa pombe mchana kutwa, anakunywa pombe tu. Hataki kufanya kazi yoyote, na akirudi hapa nyumbani, anataka apate chakula. Pengine mimi nimeenda kutafuta kibarua, ili watoto wapate chakula; Anakuja anasema, “ninataka zile pesa ambazo umeenda kufanya kazi, unipatie na mimi. Hata kama nimeenda kuuza pishi moja ya wishwa, huko madukani yeye anataka zile pesa, nimugawanyie nayeye aende kuvuta sigara. Sasa mimi mwanamke sina uhuru wakufanya jambo lolote, hata ikiwa ni kuku wangu mwenyewe nimefuga nataka kumuuza, nipate kitu cha kunisaidia, kwa sababu yeye kazi yake ni kwenda kulewa tu huko matopeni, anataka huyu kuku nikimuuza, nimgawanyie pesa nimpatie. Hilo jambo, ni jambo ambalo ni wakinamama tu, ambao wanashida hiyo.

Kitu kingine ambacho kimenisinya sana, kama mama, mimi nimaskini sina chochote, nina mtoto wangu si kusomesha kabisa, yuko hapo nyumbani, kwa sababu sina pesa za kusomesha. Anakuja yule ambaye amesoma, yuko na pesa ni tajiri, anataka mfanya kazi. Anachukuwa mtoto wangu msichana anaenda naye. Anaenda kufanya kazi nyumbani kwake. Sasa zile kazi ambazo atafanya, anafanya kazi nyingi, amabazo hata kama ni mimi mwenyewe, ningemuhurumia. Lakini yeye anaenda kufanya kazi kule, angalau apate yeye mwenyewe ajinunlie nguo; manake babake kazi yake ni kwenda matopeni. Sasa yule bwana mwenye nyumba ambaye bibi yake alitaka huyu mtoto amsaidie, kumfulia nguo za watoto wake wakiwa wamekunia, huyo mtoto wangu ndiye ambaye atafua, akiondoka kidogo tu, yule bwana anapata bibi ni huyu. Sasa atakuwa yule bibi yake akitoka kidogo, huyu msichana mdogo atakuwa ndiye bibi yake. Hata maskini ya Mungu huyu naye abebe mimba. Na sisi Wagirama ni watu ambao tuna uwoga, mali ndiyo ambayo tunataka; mtoto wako umempleka mkule afanye kazi, sasa amewekwa mimba ni yule mzee mwenye nyumba, basi unasema, “basi nipatie mali, si ulikuwa unampenda, nipatie mali” mama mtu hatahusishwa hayo maneno. Msichana anapelekwa tena huko anaenda kukaa huko kuzidi kuwa mtumwa huko. Sisi akina mama hilo jambo, limetusinya sana. Lakini hatuna sauti kwa sababu ya kuuzwa, tunachukuliwa mali, watu wanakula mali, tunabaki na mateso. Kwa hivyo hilo jambo kama ingewezekana, lingefanyiwa marekebisho hilo neno.

**Com. Abida**:Umemaliza?

**Naomi**: Bado ninaendelea kidogo. Naendelea. Lingechunguzwan hili jambo. Mtu akifanya hivyo mtoto wa mwenzake, kama ni mzee umemtaka mtoto wa mwenzako akufanyie kazi sasa unabadilisha unamfanya kama yeye ni bibi; kwa sababu unajua pengine baba yake hana uwezo, hana kitu chochote, hana mahali popote ambapo atakupeleka, hatakusudi lake ni apate mali tu. Sasa huyu mama anateseka, mtoto wake amefanywa mambo ambayo ni ya ajabu sana; tena mzee anasema anataka mali huyo mtoto anaenda. Huo mkasa hata hapa Marafa ulifanyika. Kuna mzee mwingine ambaye mtoto wake alienda nyumbani kwa mtu mwingine; sitamtaja, lakini kama yuko asikie, hilo jambo limeniudhi sana. Akaenda kufanya kazi huko nyumbani kwake, bibi yake akaondoka akaenda matangani. Yeye akawa huyo mtoto wa mwenzake ndiye bibi, hata akamtia mimba; kwa sababu anajua wale wenye huyo mtoto hawana uwezo. Hata hivi leo amezaa mapacha, nyumbani kwake huyo mtoto, maskini ya Mungu. Hilo ni jambo ambalo linahuzunisha sana. Ikiwa inawezekana, watu kama hawa wachukuliwe hatua. Na wale wenye kuwabaka wasichana wa watu, nao wachukuliwe hatua, hata kama ni kufinywa, ile tamaa yao isifanye kazi tena, wafanywe hivyo maanake huwa wanafanya kazi ambaye ni ya aibu sana. Wanaibisha sana watu hao watu. Wanafanya kuchukuliwa hatua. Kama inawezekana wachukuliwe hatua, na huyo mama awe na uhuru hata kama ni kuku wake mwenyewe akiuza, ajinunulie nguo, yeye pesa zake akizipata aende huko matopeni akanywe hiyo pombe mimi aniwachie kama ni pishi ya wiso mwenyewe nikiuza, ninunue mafuta, nipake watoto wangu. Lakini hawa wazee, wamezidi kuleta magonjwa hapa nyumbani kwa sababu ya wanawake wengi.

**Com. Abida**: Asante. Nataka kukuliza swali, unalalamika mambo ya mahari na kina mama kuuzwa, ungetaka serikali ifanye nini, au Katiba ifanye nini kuhushu hayo mahari?

**Naomi**: Kuhusu hayo mahari, kwa sababu hayo mahari, ni desturi ya Kigiriama, yaani kimila, ni jambo ambalo limeanzia tangu jadi. Nikisema lisifanyike, linaweza kufanyika lakini wakati ule wanata kufanay yale mahari, huyu mama naye ahusishwe.

**Com. Abida**: Na pia umelalamika wazee wanakwenda kulewa sana, na unasikia watu wanaomba kwamba mnazi uhalalishwe. Ungefurahia mnazi uhalalishwe ikiwa wazee wanalewa sana.

**Naomi**: Ikiwa mnazi utahalalishwa, uhalalishwe, uwekwe kama biashara zingine, ambazo zinaweza kumsaidia mtu hata kusomesha watoto, maanake huku kwetu, watu wengi walipata elimu kwa ajili ya hiyo tembo. Wakapata elimu kwa sababu hii. Sasa tunataka ufanyiwe marekebisho, ikiwa ni kuuzwa, uuzwe na masaa. Hao wazee wetu wapate nafasi ya kwenda mashambani. Si tangu asubuhi mpaka saa tatu za usiku, basi anakuja nyumbani kuja kunisumbua nimpatie chakula. Yeye tangu asubuhi yuko huko matopeni. Hilo jambo tunataka lifanyiwe marekebisho.

**Com. Abida**: Ahsante mama.

**Naomo**: Asante.

**Com. Abida**:Nani mwingine? Nani mwingine anataka kuzungumza? (not clear.

**Kajifondo**: Mimi Maoni yangu

**Com. Abida**:Waitwa nani mama?

**Kajifondo**: Kajifondo. Maoni yangu ni hivi; ni kusema wanainchi sana wana malalamishi kwa sababu ya malu. Hiyo malu itolewe, serikali iende juu chini, hiyo malu iwe hakuna. Kwa sababu malu hiyo inagonganisha watu nyumbani. Mimi mwanamke nikimshika bwana yangu, siwezi kusema "wewe toa malu" mwanamke hatoi malu. Serikali ifanye bidii ule mpango wa malu uondolewe.

Lingine; mambo ya mume akifa bibi asichukuliwe ni mume mwingine. Hiyo ni kazi nyingine hiyo. Isiwezekane. Kama ni kisawa, mimi nikifa yule bwana akaweza kuchukua ndugu yake, na bibi mwingine akachukua bibi mwingine akampatia; lakini ni sisi wanawake. Ukifa, bwana anasema nitachukuliwa, ni kwa nini yule bwana mimi nikifa yeye hawezi kuchukua bibi mwingine akampatia yule ndugu yake? Maoni yangu ni hayo. Virekebishwe, hivi viondolewe kabisa, maana hii malu inagonganisha sana, maana mimi sina nafasi kumwambia bwana wewe mwanamke yule na atoe malu anipatie mimi. Sitaweza.

**Com. Abida**: Nani mwingine ana maoni? Mama

**Sophia Kombe**: Majina yangu naitwa Sophia Kombe.

**Com. Abida**: Jana hukuzungumza?

**Sophia**: Sijazungumza. Hoja yangu ya kwanza ni kuhusu kazi, hasa kwa sisi vijana. Unaeda shule unasoma, unaenda college unasoma, mpaka unamaliza. Ukianza kutafuta kazi, unaambiwa mpaka uwe, na five years experience, ama three years experience. Sasa ile experience utaitowa wapi kama hujaajiriwa ile kazi ukaifanya ndio ukapata ile experence? Sasa imekuwa ni tabia, kila mahali, wanataka experience. Ningeomba serikali ichukue hatua, mtoto yeyote atakayetoka college apewe first priority, kupewa kazi.

Hoja yangu ya pili ni mahari. Mahari hasa kwenye kwetu sisi Miji Kenda's. Mahari imekuwa ni biashara huku, watoto wa kike wamekuwa kama biashara. Mtoto akipata mchumba, akimleta akijulikana, basi imekuwa wale wazazi ni kuitisha pesa nyingi. Ambazo zile pesa ndizo zinaleta shida sana kwa wanawake. Kwa sababu kama mtu ataitishwa kama elfu kama mia moja

ataenda juu chini akishalipa zile; basi. Mwanamke ukienda kule huwa huna sauti tena ni ukaliwe. Vile bwana atakavyofanya, atakavyosema ni hivyo. Lakini wewe hukutowa hoja yako kule kwa bwana, utakuwa huwezi, kwa sababu utakuwa umeolewa naumetolewa pesa nyingi. Mwanamume atakuwa anasikia uchungu kwa sababu ametoa pesa nyingi kwa hivyo hii mambo ya mahari ingefanyiwa kitu kidogo hata kama itakuwa ipunguzwe, iwe itapunguzwa, iwe at least kutakuwea na maskilizano kidogo.

Hoja ya tatu ni uridhi, hasa watoto wa kisichana pia tumetupwa sana. Ningeomba watoto wa kisichana pia wachukue nafasi ya kuridhi kule kwao, wawe Katika list ya kuridhi. Kama itakuwa ni kuridhi mzazi ame pass away, wale watoto wa kisichana wawe pia wataridhi. Lakini hii imekuwa shida, kwa sababu kule utakakoolewa huwezi ukasema chochote bwanako akifa, unaridhiwa pia wewe, kwa hivyo wasichana pia wawe wanaridhi.

Hoja yangu ya nne ni elimu kwa watoto wakike. Hasa huku kwetu, mzazi atakuwa pengine amezaa watoto wengi, anaangalia watoto wa kiume peke yake; anasema afadhali huyu akasome, kwa sababu ni wa kiume. Wale wakisichana wanabaki nyumbani. Sasa tabia kama ya ukahaba inazidi kuendelea, watoto wanaanza kushikwa na magonjwa. Ni kwa sababu watoto wa kike wamewachwa sana, katika masomo hawasomi. Wanasomeshwa wale wa kiume.

Ningeomba serikali itilie mkazo sana, watoto wa kisichana pia wawe wanapata elimu, sawa na wa kivulana. Na mzazi ambaye atakuwa amewatupa wasichana wake, hawafundishi, achukuliwe hatia.

Mimba. Hoja yangu ya tano, sanasana vijana na wasichana pengine wakifika darasa la sita, tano, la saba utapata msichana ana mimba. Msichana ndiye anayefukuzwa shuleni, mvulana hafukuzwi, na ile kazi ilifanywa na watoto wawili. Yule msichana anafukuzwa, mvulana anabakishwa shule, msichana akifika nyumbani kwao anapata taabu, akizaa anapata taabu. Ningeomba, yule mvulana atakayefanya vile, hata kama ni mdogo, hana kazi, yeye bado anasoma, lakini wazazi wa yule mvulana wamshugulikie huyo mtoto mpaka azae. Huyo mtoto atakayezaliwa pia wamfundishe, wale wazazi wa yule kijana wamfudishe mpaka amalize, mpaka afikie pale alipo yeye.

Hoja yangu ya sita, ni rape. Mtu yote atakaye rape msichana wa mtu, achukuliwe hatua. Na kina baba kunajisi watoto wao. Kuna baba wengine wanajisi watoto wao. Sasa kina baba hao wakipatikana, wachukuliwe hatua kali sana.

Hoja yangu ya nane (not clear) iwekwe kwenye Katiba. Chiefs wapigiwe kura kama watu wengine wote wale, kwa sababu haiwezekani; pengine chief anakaa hapo miaka yote, hamsikizani naye, hamumtaki lakini hamna la kufanya. Lakini kwa sababu mpaka siku zake ziishe haiwezekani. Chiefs pia wawekewe vipimo, kama vile miaka miwili, ama mitano, wawe wanapigiwa kura, ili upate wale watu ambao unawataka wewe mwenyewe. Na hoja yangu ya mwisho, Katiba iwe na utangulizi.

**Com. Abida**: Nani Mwingine?

(Not Clear)

**(No name)**: Mimi maoni yangu ni kuhusu elimu ya wasichana, huku kwa Miji Kenda. Elimu huku ya wasichana, inazorota sana. Hasa upande wa kifedha ndio sisi tunashindwa. Lakini hata hivyo, zaidi sana twaomba serikali kama itatutilia mkazo ili watu wote wajue umuhimu wa elimu; na hasa, wale wazazi pia, waone ile nguvu kwa sababu serikali itakuwa inatupunguzia gharama, kama ilivyokuwa ikifanya kitambo. Hasa, kitu kama hicho kinachangia, wasichana wetu huwa wanaandikwa kazi; halafu mtu akiajiriwa anakuwa maid pahali, halafu wakati wakiendelea na hiyo kazi, mzee wa hiyo nyumba anamunyemelea analazimka. Hata serikali imetuacha kabisa haitusaidi. Wala hoja hiyo ukipeleka mbele, inazimwa na senti, maana watu huwa hawana pesa. Tunaomba sisi kama wazazi, tunasikia uchungu na tunaomba usaidizi hapo juu.

La pili ni kwamba, kunazo shule nyingi za malezi, tunaomba wakati wa kuandikwa Katiba hizo; tusaidike sisi kama wanaolea wale watoto wadogo.Kwa upande wa kimshahara, pengine kama hivi, mtu ameandikiwa kazi, ni mwalimu wa kawaida, hawa walimu ambao, wanalipwa na serikali, huwa wanapangiwa mishahara mizuri. Lakini kupitia hawa watoto wadogo, huwa serikali haijawatambua sana. Kwa hivyo walimu wanao wafundisha watoto wadogo nao, twaomba hoja yao ifike huko kwenye Katiba ihesabiwe. Yangu ni hayo asanteni.

**Interpreter** (not clear)

**Kasele**: Mimi nazungumza kwamba watoto wangu walikuwa shule hapa, ikabidi wasimamishwe kwa sababu pesa sina. Nguo sina, nasikitika sana ikabidi niwambie wakae nyumbani, maanake wanaume ni hivo walivo tayari. Maoni yangu ni kwamba, watoto wangu nataka waregeshwe shule na wasome. Mimi sina pesa, lakini nataka waregeswe wasome. Kwa hivyo hayo ndio yalikuwa ni maoni yangu.

**Com. Abida**: Mzee yuko wapi? Mume wako?

**Kasele**: Yuko huko nyumbani

**Com. Abida**: Hafanyi Kazi?

**Kasele**: Mume wangu ana kibarua tu, anapata kitu kidogo, akija nyumbani haitoshi, kwa hivyo ni mashaka yako nyumbani.

**Com. Abida**: Asante.

**Hilda Chome**: Kwa majina ninaitwa Hilda Chome

**Com. Abida**: Nani?

**Hilda**: Hilda Chome. Hoja yangu ya kwanza ni rape, kwa watoto wa kike, ambao wanarepiwa na wazazi wao. Ningeonelea, kwa sababu wakati huu tayari, vile wanavyo adhibiwa; kama kukikuwa na kesi, nafikiri? Hawaadhibiwi vizuri. Kama ingewezekana, kwa sababu hata huyu baba anaujua uchungu wa huyu mtoto, angeadhibiwa zaidi ya vile wanavyoathibiwa sasa.

Hoja yangu ya pili ni pande ya machief. Hawa machief ingekuwa vizuri pia kama inawezekana nao pia wachaguliwe, kama vile viongozi wengine wanavyochaguliwa; kama vile MP ama councillor. Kwa shauri saa ingine, inaweza kuwa chief haelewani na watu, halafu ile hali ya kuwa sasa anaendelea hivyo hivyo, haelewani na watu; ni mpaka sijui mpaka kufa, sijui ni mpaka vipi, sasa ile huwa inatusumbua zaidi kwa sababu wakati mwingine tuna kosa kuelewana na hatuwezi kupatanishwa na chief. Hatuwezi kurekebishika kupitia kwa yeye. Sasa ingekuwa vizuri kama anagechaguliwa kama viongozi wengine, kwa muda kama miaka mitano, ama hata kama ni zaidi, lakini at least kwa muda fulani; awe anaweza kubadilishwa kuwe mtu mwingine.

Hoja yangu ya pili, ni kama vile mama ameolewa mahali. Sasa mama ameolowa, halafu tuseme wakosane na yule mzee. Wakati wa kuondoka yuaondoka yule mama pekee. Na pale mama ameolewa, amekuja kweli ameolewa na mahari, lakini amekuja pale wameelewana na yule mzee, wamezaa miaka yote hiyo; pengine wana watoto kama vile watano. Wakati wamekosana yuwaenda kwao kabisa, kabisa, hakuna cha kusema tutagawanya watoto, ama vipi. Ingekuwa vizuri, at least na yule mama naye akiwa ameolewa, naye aende na sehemu; kama kugawanya sawa kwa sawa, kama hata yule mzee atazidiwa, at least yule mama aodoke na kitu. (not clear)

**Com. Abida**: Kuna Mwingine

**Somebody**: Mimi masikitiko yangu ni kuhusu.

**Com. Abida**: Sema jina lako.

**Mary Masha**: Mimi naitwa Mary Masha.

**Com. Abida**: Mary Masha.

**Mary Masha**: Mimi masikitiko yangu ni kuhusu mambo ya kuolewa. Kuolewa tunaolewa kweli, lakini wakati wa uridhi, sisi tunatengwa. Na walio tutenga mwanzo ni wazazi wetu. Na ni sababu ya ile mali wanayoitisha wale watu wanatuowa. Sasa mtu unakuta umeolewa hujui mzee amepaka pesa ngapi, unasukumwa tu kama mbuzi. Hasa ukifika huko, halafu wewe unakuwa

kama mtumwa, na ukijaribu kuondoka hapo huwezi, kwa sababu ya ile mali aliyotoa. Sasa tunaomba serikali iweze kutusaidia. Hata kama hiyo ni mapatano watakuwa wamepatana isiwe ni lazima uolewe; uambiwe uko hapo, wewe umeolewa, umetolewa mali. Hata kama ni kuoa, mtu unatamani kuolewa. Uolewe kwa kukubaliana. Wazazi wako, wapewe kama shukrani, si kitu kitajwe kama mali. Inaonekana hiyo mali imetufunga hata akili. Hata sisi ambao tunaolewa, hatuna uhuru, kwa sababu ya kile kitu kinaitwa mali. Kwa hivyo mimi naomba hii jina mali, liondoke.

Pili ni kubaguliwa kwa watoto wetu wa wasichana. Watoto hao wasichana tunawazaa wake na waume. Lakini ikifika wakati wa kusoma, utakuta mtoto huyu wa kike hana uhuru wa kusoma, sababu ni yule Katana anaweza kwenda kusoma, lakini Sidi hana uwezo; sababu yeye ni mwanamke wa kufanya kazi za nyumbani. Kwa hivyo tunaomba ikiwezekana hata hao wasichana nao watiliwe maanani.

Tatu ni kuhusu kunajisiwa kwa watoto. Unakuta mzee anakuwacha wewe mama nyumbani, halafu anaenda kupembeleza mtoto wake, mpaka anamfanyia hayo mambo mabaya. Na anafanya ya siri mpaka mwisho yake unajua. Na ukijua, huna uwezo wa kuzungumza, kwa kuwa wewe pia umeolewa hapo, na ulitolewa mali. Sasa tunauliza ama tunaomba, ikiwa kuna uwezekano, mtu kama huyu akifanya jambo kama hilo la kunajisi mtoto, wake, ama wako pia achukuliwe hatua. Manake hilo ni jambo la aibu, na ni jambo la kutoa imani baina ya wewe na huyo mzee hapo nyumbani. Mambo ni mengi lakini naona nitakomea hapo.

**Interjection**: Endelea kama uko na mengine.

**Mary Masha**: Mambo ni mengi, kwa vile kuna mambo mengi kuhusu sisi ambao tuko hapa kama uridhi. Umeolewa na hapo kwenu huhesabiwi kitu, huko utakako olewa hutahesabiwa kitu. Sasa utakuta kule ambako umeolewa, kama pengine umewachiwa ngombe ama mbuzi, huko ukijaribu kuzungumza; basi unaambiwa "basi hapa umeletwa na mali", na kule ulikotoka ukitaka kuzungumza zaidi unaambiwa "basi we nenda huko huko maanake huku sisi hatukuhesabu tena; maanake wewe ni mtoto wa kike". Kwa hivyo tunaomba kama wakina mama, ama kama wasichana, tutambulike kwetu nyumbani, ama huko tutakapo kwenda. Asanteni.

**Com. Abida**:Hebu nikulize, hii mambo haya umetuambia kuhusu kunajisiwa kwa wasichana wa kike, yanatendeka sana?

**Mary**: Yanatendeka sana, na hata ukijaribu kuzungumza kimtaani, ama ukijaribu kuyapitisha kwa upande wa kiserikali hivi, lina zimwa zimwa. Kwanza jambo lingine nimesahau ni hili. Wajua mambo mengine yanatendeka kwa sababu sisi wanawake, si sana kuwekwa kama mzee wa kijiji. Kwa mfano kama umeambiwa mambo ya malu; ukifika kule, utakuta walio kule wote, ni wanaume. Sasa wewe huyu mtu wamjua ni sawa, humjui pia, utaambiwa afadhali, ukubali halafu hayo mambo mtazungumza baadaye; sasa wewe unakubali kulazimishwa; Lakini je? Kama kungekuwa na mwanamke mwenzako hapo, mngezungumza naye pia angekutetea kwa upande mwingine. Kwa hivyo hapo tunaomba hata hao wazee wa kijiji na wanawake wa emo. Asante.

**Com. Abida**: Majina kama mlivyojiandikisha, tutamwita Bwana John Mweni

**John**: Kwa majina ni kama mlivyosikia. Naitwa John Mweni. Nimekuja hapa kutoa maoni yangu binafsi. Kwanza: serikali iwe ya majimbo, na si majimbo tu, bali mfumo wa vyama vingi. Hiyo ni kwanza. Tukisema vyama vingi, ni watu mahali wanaposhindania, kwa mfano, mimi niwe nyumbani nimezaliwa na mwenzangu, nitafanya nini ili, baba anipende? Hapo ni kumaanisha kwamba serikali yetu hii ikiwa ya vyama vingi, tutapata kuona watu kama sisi wa huku mwisho mwisho wa Kenya vile tutakavyo fanyiwa. Kwa sababu nikirudi hata mahali pengine kama maji, sisi huku tangu tupate uhuru, bado tunatumia ile maji ya mvua. Tunangoja mvua inyeshe maji yale ikwame mahali, ndio twende tuchukue tutumie nyumbani. Hiyo ni kumaanisha kabisa kwamba, serikali yetu Imetusahau. Ndiyo maana nikisimama hapa, maoni yangu ninasema, kuwe vyama vingi, angalau tutaangaliwa upande wa maji.

Pili, upande wa uchaguzi. Uchaguzi wa debe unatumaliza, kwa sababu yule anayepita, tunayesema amepita; inaviringwa hapo, tunapelekewa yule ambaye sio mshindi, tunaambiwa, “huyo ndiye mbunge wenu”. Hilo mimi nakataa, ule uchaguzi wa debe, kura za debe ninakataa. Kura zile za mlolongo zirudishwe. Tukisimama kwa mlolongo, tukimpitisha fulani, kama diwani wetu, awe yule yule. Ndiye diwani atakaye enda kule, ama mbunge atakaye enda kule, ama rais atakaye enda kule. Kwa sababu tunaweka kura kwa debe, madebe, yakipelekwa kule, kuhesabiwa hesabu zikirudishwa hapa, tunaambiwa mtu wetu ameanguka, na hatuna la kufanya. Kwa hivyo ninasema, kura zile za debe tuondoe.

Tatu. Mamlaka ya rais. Rais tunamchagua sisi, na si ati kwamba tunamchagua halafu atuchagulie viongozi. Hapo mimi ninakataa. Kwa sababu yeye mwenyewe tumemuchagua , kwa nini wale viongozi wengine tusiwachgue na sisi? Mimi maoni yangu ninasema; rais tumemchagua kwa kura, wale viongozi wengine watakao fuatana naye, tuwachague kwa kura zile zile zetu tulizomchagulia rais. Hayo ndio maoni yangu.

Nne. Upande wa elimu. Elimu huku kwetu iko chini. Na si ati sisi huku, hatutaki kusoma. Kusoma tunapenda, sana lakini serikali bado haijakubali sisi tusome. Kwa sababu tukiangalia upande wa karo; inatuzidi sana. Pili. Shule kwetu ziko mbali mbali zaidi, kiasi ya kwamba, mtoto mdogo, hawezi kusoma kwa wakati wake, ama kwa umri wake unaofaa. Inabidi mtu atembee mbali, ndiyo afike shule, apate elimu. Bila hivo, hawezi kupata elimu. Shule za upili, tukiangalia, hapa Magarini, shule za upili ni mbili tu. Kuna Marafa, na Galana; kusema kweli, hizo shule mbili hazitoshi Magarini.

Tukirudi upande wa university. Mimi hapa nikishamaliza shule, karo tayari mzazi wangu zimemchokesha, amenipeleka mpaka form four nimemaliza, imebaki sasa nifuate university. Hizo pesa za kunitoa hapa, mpaka kule, tayari mzazi wangu akiangalia hivi mfuko nimwake, hana. Kule mimi siwezi enda, ndio maana hata utakuta, D.O. mwenyewe hapa kwetu, atatolewa Bara; kwa sababu watu wa Bara wamesoma, university ziko kule kwao. Na hiyo inamaanisha kwamba elimu hapa kwetu iko chini. Lakini ingekuwa serikali itukumbuke upande wa elimu, mtu kama D.O., hangetoka mbali, angetoka hapa hapa kwetu, mtu kama D.C.

hangetoka mbali, angetoka kwenye mkoa huu wetu. Lakini tukianza kufikiria hivi, siwezi kukuhesabia ma D.C. kumi, ambayo wametoka kwenye huu mkoa wetu, ama tuseme, hata wawili. Na hiyo ni kwa sababu elimu sisi hatuna, na ni serikali ndio imetufanya tukose elimu. Kwa hivyo nikirudi pale juu, ndiyo ninaunga mkono mfumo wa vyama vingi. Vikiendelea kushindana sisi tutapata usaidizi.

ardhi. Arhi yetu tukipewa, malipo ya karatasi za kumiliki mashamba zilikuwa ni pesa ndogo. Sasa tunaambiwa kwamba kulipa shamba lazima uwe na elfu sabini. Kumaanisha kwamba, watu kama mimi ambao hatuna pesa kupata karatasi zile za kumiliki mashamba. Ndio maana unakuta tuko huku, wewe unasema umekalia shamba lako, kumbe mtu anapita kwa gari hapa na yuko na karatasi ya shamba lako. Kwa hivyo mimi naomba serikali ilete hizi ofisi ambazo zinaweza kutoa hizi karatasi karibu ili kusudi nasisi tuwe tunaweza kupata hizi karatasi, na zikapate kutusaidia.

Nikirudi upande wa bibi na bwana nyumbani. Maoni yangu nasema hivi. Kwa sababu tumekuwa sisi waume nyumbani hatuna uwezo. Kwa sababu mimi nikikosana na bibi yangu kwa mfano aende, hata asiende mbali, aende kwa chief, nikaribu sana hapa kwa chief. Ukifika pale utaona wale maskari wachief vile watakavyo kuangalia wewe. Hata itakuwa ni kama sijui umewafanya nini, na umempiga bibi yako nyumbani maanake amekukosea. Unajua umejaribu sana kuvumilia lakini sasa amezidi. Nikimtia kofi, mara anakimbilia kwa chief. Akifika pale kwa chief, pengine chief hayuko karibu, anawaona wale ma askari; kuna ati mtu ni mkubwa pale. Basi akikuona wewe bwana vile atakuangalia, hata wewe mwenyewe pengine utaanza tayari kumlegezea. Mara anaweza akufuate tayari akupige mbele za yule bibi yako. Serikali iwe na inaweza kutuangalia zaidi juu ya nyumba ya mtu. Kwa sababu hizo sheria wanazozitunga, nikizaliwa mimi, nilikuwa ninaweza nimwuone mama ana adhibiwa na baba; na hakuna lolote. Lakini kufikia sasa, sisi mabwana tumekua ni kama tunashikilia mioyo yetu. Ikiwa bibi umemchukua kwa babake, umemtoa kwao, ni wewe mmependana. Lakini sasa kama amekukosea unashindwa na kumuadhibu kwa sababu kitu kidogo tu, anaenda. Na akienda kule unachukulia hatua, juu ya hatua, hatua juu ya hatua hata mwisho unaweza kumkosa yule bibi. Wanawafurisha hao mabibi zetu, kiasi ya kwamba hata nyumbani hakuna uwelewano tena. Kwa hivyo hili jukumu la nyumba zetu serikali pia iliangalie. Asanteni (Makofi).

**Unknown person**: Mzee umesema kwamba sisi wazee tuwe na haki ya kupiga mabibi wetu wakikosea, ungetaka nao mabibi wawe na haki ya kupiga akina baba wakikosa?

**John**: Mimi, hapo nataka tuelewane kitu kidogo. Hapo ninataka tuelewana kitu kidogo, kwa sababu si ati bibi apewe mamlaka ya kunipiga, na mimi pia si ati kwamba nitapiga yule bibi yangu kupita kiasi. Nimesema kwamba hii nyumba iangaliwe, iangaliwe kwa sababu bila kuangaliwa, itakuwa zile kesi za bibi na bwana wakienda pahali, wanaenda tayari ni kama kutenganishwa. Kwa sababu sasa limekuwa halitiwi maanani halitiwi mkazo. Mimi yule bibi nitampiga kama bibi yangu, maanake hata kama ni upatanisho, hakuna upatanisho zaidi kwa chief ama kwa D.O. au kwa D.C. isipokuwa upatanishi uko kwa yule yule babake aliyenipa yule mtoto. Na ninaonelea kwamba, kama yule bibi tumekosana; hata akinipeleka polisi kwa mfano , nikapigwe makofi, nikitoka kule nikirudi, kuna uwelewano baina ya mimi na yeye? Hakuna uwelewano. Kwa hivyo pale pale nilipomtoa

yule bibi, kama nimekosa naye ananirudisha, pale pale. Pengine pale, wazazi wake hawatakosa la kuniambia. Ziko kajama huwa tunawapa wazazi wao, na tunapatanishwa. Maoni yangu ninasema, yale mambo ya polisi yaishe. (makofi na kicheko)

**Com. Abida**: Justus Kazungu?

**Justus**: Kwa jina mimi naitwa Justus Kazungu. Niko na maoni haya. Kitu ambacho ningeanza kuzungumzia kwanza, ni juu ya ugawaji wa misaada ile ambayo inatoka nje. Katika Katiba hii mpya, tunataka misaada ile ambayo itatoka nje ihakikishwe kwamba inagawanywa kisawa. Utakuta kwamba, kufikia wakati huu kulingana na serikali au Katiba, vile ambavyo iko, sijui kama ni Katiba au ni ile serikali vile ambavyo imeamua kwa wakati huu, utakuta kwamba misaada inatoka nje, lakini inaelekezwa mahali pamoja. Pengine watu wa Bara wameendelea, lakini hapo mimi nakataa kwa sababu hao wanafanya kuendelezwa. Misaada ikitoka inapelekwa huko. Ningetaka serikali hii inayokuja ihakikishe kwamba, Katiba, ihakikishe kwamba; ile misaada ambayo itatoka, inagawanywa sawasawa. Kama ni maendeleo yawe kila mahali. Hilo ni la kwanza kuhusiana na ugawaji wa misaada.

Pili, Katiba hii ambayo tunataka kuifuta ni kwamba, hii iliundwa na wale wakoloni; na tulipopata uhuru au tukarithi na tunaona kwamba yule mkoloni wakati alipo unda hiyo Katiba yake: alikuwa anaunda kiasi cha kuwa impendekeze mwenyewe. Kwa hivyo utakuta hiyo aliunda kiasi cha kuwa kwanza alipokuja hapa, alijaribu kuchukua nchi au zile sehemu ambazo ni nzuri nzuri ili ajipendekeze mwenyewe. Sasa utakuta Katiba ile ambayo iliundwa na mkoloni ili ajipendekeze. Tulipopata uhuru tukaona kwamba tulichukua hiyo Katiba na hatukuibadilisha, tulichukua mamlaka, tukarithi hali ile ya kujihurumia wenyewe.

Tukiingia upande wa ardhi utakuta, tangu tupate uhuru utakuta katika hii division ya Magarini siwezi kusema kuwa kuna mtu yoyote ambaye amepata title deed. Na hii ni kwa sababu wale ambao waliochukua uongozi walitumia mbinu ili wajipatie ardhi ile wenyewe. Kwa hivyo utakuta hapa Pwani, ziko title deeds, lakini wale wenyeji ni wachache ambao wamepata. Waliopata ni wale ambao wanatoka sehemu za Bara. Na hii inaweza ikaondolewa kama tutakua na majimbo. Kwa hivyo hapo mimi ningetaka serikali ya majimbo. Kama ni ugawanyaji wa ardhi, utakuta nasi tutapatiwa uwezo wakupata ardhi kama watu wengine wa Bara wanavyopata.

Na kama ni title deeds tuzipate. Mtu ambaye yuko katika Head Office, Nairobi: utakuta huyo atafanya kuwa allocated tu, “okay, wewe nenda Magarini au pengine nenda Shakadulla, au pengine nenda sehemu za Pwani, mahali fulani utaenda kupata shamba. Lakini shamba lile, mahali pale ambapo inajulikana kwamba hakuna mtu katika karatasi hiyo tupu; utakuta hapo kwa kikweli kuna mtu. Kwa hivyo ningeomba hii Katiba mpya ambayo itahusiana na ugawanyaji wa ardhi, wategemee ma sub-chief na chief, au na wazee wa vijiji. Kama title deeds zitatolewa, ziletwe lakini wawe ni kama macho ya serikali. Wawe wanategemea wale wenyeji, wale ndio watatambua hapa hakuna mtu; kwa hivyo atapatiwa yule mtu ambaye anastahili. Kwa hivyo hii hali yakutowa hizi title deeds, tafadhali, ningetaka katika Katiba, ihakikishwe kwamba inaletwa hapa chini; na hawa wazee wetu wahakikishe kwamba wanatoa pale ili yule mtu ambaye anastahili, kupata, apate. Wao ndio wanamjua zaidi. Hiyo

ni upande wa ardhi.

Tukiingia upande wa uridhi, utakuta kwamba kufikia sasa, mtoto ni mtoto wewe kama mzazi umezaa mtoto msichana, umezaa mtoto mvulana, lakini mtoto ni mtoto. Siku hizi wacha siku za nyuma, lakini siku hizi utakuta kwamba, kuzaa nyumbani ilikuwa ni aibu siku za nyuma, lakini kufikia wakati huu, imekuwa ni kama kawaida. Its just the order of the day. Sasa utakuta hapa kama mimi ni mzazi nimezaa watoto wangu, okay. Akiolewa, ataenda kwa bwana yake, lakini kuolewa si kwamba yeye ataenda kuishi huko. Anaweza pengine hata akashindwa na maisha ya kule, akarudi hapa: au pengine ni mzae na kwa bahati mbaya au nzuri, yule mtoto azae hapo. Yule mtoto siwezi kumfukuza, ni wangu. Kwa hivyo yule mtoto ni wangu na sasa niwe na watoto wawili wanaume na watoto wawili wasichana. Hawa wawe hawakupata nafasi ya kuolewa, hawana mtu wa kutegemea. Mimi siku zangu zimewadia ni aage dunia, hawa watoto nichukue ule uridhi kulingana na mila za kikwetu haswa Kimiji Kenda. Uatakuta mtoto anayestahili kupata ule uridhi ni mtoto mvulana. Je wala wasichana? na kama hataolewa na abaki pale kwa maisha yake yote, yule mtoto utamwona yuko namna gani? Kwa hivyo ningesema katika Katiba hii ambayo inataka kuundwa, huu uridhi, mtoto ni mtoto. Kwa hiyo hata naye agawiwe kiwango fulani; hata kama sio sawasawa, lakini ahakikishwe kwamba yule mtoto anapatiwa kitu pale ndani, kwa sababu mtoto ni mtoto. Hii ni kwa upande wa wasichana, na hawa kina mama, wasichana kwa wavulana, iwe kuna ratio fulani.

Nikingia upande wa sheria. Utakuta kwamba kufikia wakati huu kuna sheria kwamba kuna wengine wako, "they are above the law". Hii kitu hii ni mbaya kwa sababu binadamu ni binadamu, hata kama wewe ni kiongozi. Lakini itakuwa makosa, mwingine awe huko juu ya sheria. Kila mtu anastahili kuwa chini ya sheria, ili akifanya makosa, sheria, imwangalie kwa macho mawili. Kwa hivyo hapo, singetaka katika hii Katiba ambayo inakuja, kuwe na mtu yoyote hata kuanzia president, kila mtu awe chini ya sheria, na akifanya makosa, imkabidhi. Sheria vile vile utakuta kama raia, hatujui sheria. Hatujui sheria ni kwamba hatujui haki zetu. Utakuta askari anaenda miezi sita, au kulingana na wakati wa training yao, anaenda kufunzwa sheria. Anaabiwa mtu akifanya hivi, amefanya makosa. Akifanya hivi, amefanya makosa; lakini sasa wewe mwananchi ni ufate ile sheria.

Hujui unaenda wapi, hiyo sheria inakukabithi kwa kutojua. Kwa hivyo hapa upande wa sheria kulingana na hii Katiba ambayo inakuja, ningetaka sheria zifunzwe kwenye shule; na vile vile kwa wale ambao hawatabahatika kwa sababu umri wa shule umewapita, tuhakikishe kwamba hizi sheria zinasambazwa kwa machief. Au pengine kuwe na vikosi au vikundi fulani ambavyo vimelimika hali ya kuwa wanaweza wakaelimisha hawa raia vile vile juu ya haki zao; ili anapoenda kukosa, au kama amefanya makosa aweze akajua kweli hapa ni makosa. Lakini sasa utakuta askari anajua tayari huyu nikimpata, nitaenda kumshtaki kwa kifungu fulani. Kwa hivyo hapo hakuna usawa. Maoni yangu ni kwamba, sheria, shule zifunzwe na wale ambao wamepita ule umri kuwe na mafunzo fulani ambayo itawaonyesha, itawangaza ili waweze kuena mbele zaidi.

Kwa kumaliza, kitu kidogo tafadhali, ningetaka kuzungumzia juu ya mahakama. Mahakama kulingana na vile ambavyo tuliichukua hiyo sheria ya mkoloni tukaileta: ni kwamba hapa upande wa mahakama kuna kitu fulani ambacho sisi kama raia au kama Miji Kenda, kuna kitu ambacho hakiangaliwi. Lakini hii ningetaka kiangaliwe, hii ni upande wa utamaduni, haswa uchawi.

Uchawi utakuta sisi kama Waafrika, mzungu hajui uchawi, lakini sisi Waafrika tunajua uchawi. Kama mtu ananiroga nikienda, kotini kwa sababu yule mtu ananiroga, nikifika kule utakuta wanataka documentary evidence, kwamba wewe sasa umerogwa, unarogwa, iko namna gani? utowe document; sasa hapa ninaona kuna makosa. Katika Katiba mpya ningetaka hii nayo iangaliwe, hii sheria ya utamaduni kwa sababu uchawi uko. Tuwe na vikundi vya wazee au wa kienyeji ambapo lile koti kule, itategemea huku. Mtu kama amerogwa, okay hakuna documentary evidence, lakini kama wale wazee, ambao wanajua uchawi uko, wakidhidhirisha kwamba huyo mtu amerogwa na yeye mwenyewe anaamini hivyo akifika kule aaminiwe. Isiwe mtu akifika kule kesi inatupwa, na sasa utakuta hapo itakua ni hali ya kukutana na mapanga. Na kweli inawezekana huyo mtu ameingizwa katika hizo madawa.

Pengine la mwisho ningetaka pia, hii Katiba ikiundwa, adhabu ya kutadikwa viboko wanafunzi wa shule, isiondolewe, iweko, kwa sababu tumeona madhara ya kutokuwa na adhabu katika shule. Shule nyingi, serikali ilisema kwamba hakuna ile hali ya kuathibu watoto, utakuta shule nyingi zimechomwa; na mambo mengi haswa katika secondary utakuta yamefanyika, unywaji wa pombe, bangi, na vitu vingi. Kwa hivyo, kama ile adhabu iko, ile adhabu ya kiuzazi, ya kimwalimu iweko, ile ya kupitisha kiasi, basi kama mtu amepitisha kiasi, hiyo sheria imwathibu. Lakini ile adhabu iweko katika mashule. Nikimalizia mimi ningependelea serikali ya majimbo ije. Asante. (makofi)

**Com. Abida**: Charo Katana Mwambire, Shariff Chome. Asante, Hezron Toya.

**Hezron**: Kwa majina yangu ninaitwa Hezron Toya. Kwa maoni yangu kuhusu Katiba, mwanzo ningetangulia kuhusu utamaduni ama mila. Yaani kama bibi mumeachana umempa talaka na ameenda kwao, hapo kama ameolewa kuingine kabla ya wewe, kuregeshewa mali yako, una haki ya kudai malu. Ninakosowa moja wetu, ambaye amekuja kuongea kuwa tutegemee upande moja. Lakini mimi nasema kama ni kuacha, tuache upande zote, na kama ni kuendelea, tuendelee pande zote. Huwezi kuchukua mamlaka, bibi yangu uwe utamuuza, hiyo ni ngumu na haiwezekani, hiyo haitawezekana kabisa. Nimemuowa bibi yangu kwa elfu thelathini; na umemuuza kwa shilingi elfu sabini ama arobaini, zile zingine unachukua wewe, hiyo hakuna. Uchukue na ujue kuna adhabu, ambayo hapo nitakata; hiyo ni kawaida kulingana na mila. (kicheko) Kwa hivyo, incase bibi yangu amekufa kule, na sijaregeshewa changu patakuwa na ulazima na apelekwe huko aende kuzikwa huko; maanake huyo ajaregeshwa mali, sasa ananiletea maiti kwa nini? Kwa kuwa ni shida lakini kama ni raha hunitambui hiyo nakataa.

Nikurudi tena kwa upande wa kuwa, mali itoke kwa mvulana na msichana, hiyo ni ngumu. Mali itoke kwa mvulana yule ambaye anaoa, hapo ndio utakuwa na uwezo, maanake bibi atakuwa anakuheshimu. Lakini ukisema kama ni shilingi elfu hamsini itoke kwa bwana, elfu hamsini itoke kwa bibi, itakuwa hakuheshimu anakudharau, atasema nini, hata kama ni pesa baba alitoa elfu hamsini, wewe unaniletea nini? Hiyo ni ngumu, na maanake imesemekana kuwa kama umempa talaka munaweza kugawanya watoto, hiyo haiwezekani. Watoto watakuwa ni wa mbari gani? Unaenda huko nyumbani, mimi nimechukua watoto wawili, bibi amechukua watoto wawili. Kule hawatakuwa na urithi, watakuwa ni wageni katika nchi ya

ugenini, na hawatakuwa na uridhi, watakuwa wanasumbuliwa na wataulizwa, nyinyi watoto mulitoka wapi? Watamlazimu mama, "tunataka baba yetu, yule ambaye ametuzaa". Kwa hivyo hiyo ninasema mimi ikatwe kulingana na Katiba, hakuna kitu kama hicho. (kicheko)

Kuhusu mamalaka ya rais, kuwa rais awe atakuwa sawa tu kama mimi, awe raia; haitajulikana mzee ni nani. Lakini yale mamlaka ambayo yamezidi yapunguzwe, inasikitisha kama rais atakuwa na uwezo, tuseme tumegomea jambo fulani, tumegomea kazi, mshahara ni kidogo, lazima ionekane kuwa lile jambo ni muhimu na litatuliwe. Lakini kama atasema kuwa, kama umegomea kazi, nenda nyumbani, kutaandikwa mtu mwengine, itakuwa haina maana. Hiyo lazima ifikiriwe katika Katiba hiyo mpya ambayo tunaunda; ni sisi wanainchi ambao tumeunda hapa na lazima ifikiriwe. Yale mamlaka ambayo yamezidi mwanainchi zaidi, yamemkera ile iondolewe, rais awe na mamlaka ya kawaida, sikuwa ati awekwe pingo apelekwe jela, hawezi kuwa raia kama wewe, hiyo lazima ujue.

Na zaidi ambayo tunataka, tukisema Katiba ibadilishwe, kumekuwa na chama kimoja, tukawa na vyama vingi, na sasa kuna huu mfumo wa Majimbo, tukusema Katiba ibadilishwe, ibadilishwe ndio, lakini itatatanisha mahali fulani, lakini vile nasema majimbo iwe mbele, tunataka majimbo. Majimbo ikiletwa itakuwa ina serikali yake, kutakuwa na serikali ya kutawala majimbo sasa hii Katiba itakuwa zile sheria ambazo ni ngumungumu, zitakuwa zimeondolewa. Majimbo yatakuwa na serikali zao ambazo wananchi hawatakuwa na shida, kama kuna tatizo fulani linasuluhishwa, maanake kila mahali jimbo kila mahali kulingana na mikoa, hiyo itakuwa sawa.

Jambo lingine nikuhusu hongo kwa polisi, kuhusu usalama kwa mfano, niseme hivyo. Tuseme polisi amenishika saa hii, ni msako wa usiku; nampatia elfu moja, natembea naenda nashikana na wengine, wananisumbua niwe sina kitu wananipeleka ndani, na hapa nimetoa elfu moja. Itakuwa ina maana gani? Naenda kufungwa na elfu moja nimetoa. Kwa hivyo hakuna haja, kama nimeshikwa, nipelekwe, niende kujitetea; inaweza kuwa lile kosa ni kidogo, siwezi fungwa na naweza toka tu na kitu kidogo: hata naweza kuachiliwa bila kutoa pesa. Lakini hapa naenda, natoa elfu moja, haitakuwa kitu, hiyo ni bure; kulingana na Katiba hiyo hongo iachwe, niende mbele kujitetea. Kama nitafainiwa, itakuwa faida kwa serikali zile pesa ambazo nitazitoa. Lakini hongo napatia polisi, inaenda hivo, na hakuna mabadiliko; la hasha, hiyo haiwezekani, kulingana na Katiba tunayounda, hiyo haiwezekani.

Na lingine, mamlaka ya polisi: awe atakuja nyumbani kwako na search warrant, barua kutoka kotini, siaje tu kienyeji, ati nyumba yako nigani, hutaki kufungua anavunja; anaenda hata kwa choo, anaangalia kila kitu. Lazima aonyeshe barua, ijulikane kuwa ni halali, amekuja hapo, ametumwa; lakini siati anasearch tu hivi hivi kienyeji, kama kutapotea pesa itakuwaje? Malalamishi yangu nitapeleka wapi? Kwa hivyo polisi hapo mamlaka yao ni kama kuchukua sheria mikononi. Hiyo, kulingana na Katiba ambayo tunayounda mpya, hiyo hakuna. Tunaongea yote lakini zaidi, nasema tunataka utawala wa majimbo, kwa hayo machache asanteni."

**Com. Abida:** Hebu subiri kidogo, nataka unifafanulie. Kuhusu hili swala ambalo umesema kwamba watoto wasigawanyishwe, na hasa wasipewe mama, kwa sababu watapoteza mbari yao, sio?

**Hezron**: Ndio.

**Com. Abida:** Sasa kazi kubwa ya mama ni gani si ni ulezi?

**Hezron**: Kazi kubwa ni ulezi, ndio.

**Com. Abida:** Haya unasikia pia kuna haki za watoto sio?

**Hezron**: Ndio

**Com. Abida:** Sasa huyu mama ukimunyima mtoto wake, atalelewa na nani?

**Hezron**: Watoto ni wa bwana na bibi, tukiwa pamoja. Watoto ni wa mke na mme wakiwa pamoja; lakini kama kutakuwa na uwezo huo tumeachana, na achukue watoto aende nao. Sasa kama watoto watateseka kule, tunasema nihaki tugawane, kama watoto watateseka mimi sitataka, sikuwazaa watoto wangu wateseke. Nitahitaji watoto wangu wanijie, kama watakuja nitawasomesha, sitawaruhusu tena waende kwa mama. Kwa hivyo hapa naona, kulingana na Katiba, itakuwa si mzuri tukifanya kitu namna hiyo. Hayo ni maoni yangu.

**Com. Abida:** Asante. Eric Mae, Josphat Karisa, Daniel Karisa.

**Daniel Karisa:** Ehh, kwa majina naitwa Daniel Karisa naniko hapa kutoa maoni yangu ya kibinafsi. Kulingana na Katiba tunayoitaka, nataka Katiba hii iundwe na serikali ambayo itakuwa ni ya demokrasia halisi. Si serikali ambayo ni ya maneno matupu, lakini tuone vitendo ambavyo vitakuwa vinafanywa na serikali. Wananchi wapewe maamuzi zaidi, si serikali tu kujiamulia mambo yake lakini kuwe kuna uhuru wa kutoa maoni, ama uhuru wa kutoa malalamishi. Kwa mfano, utaona ya kwamba, kama kuna hali ambazo wananchi hawaridhiki; wakati mwingine huwa wana andamana yaani kuonyesha ya kwamba zile hali hawaridhiki nazo. Lakini wakati mwingine wanapofanya maandamano ya amani utaona ya kwamba yavunjwa na polisi. Wakati mwingine wanapokusanyika kwa ajili ya mikutano, utaona ya kwamba, serikali inaingilia na kuvunja mikutano. Kwa hivyo utaona ya kwamba hakuna uhuru kamili wa kidemokrasia. Kwa hivyo langu mimi, nasema ya kwamba serikali iwe inaangalia masilahi ya wananchi sawa sawa. Pia ninataka serikali ambayo itaweza kumlinda mwananchi na mali yake. Nasema hivyo kwa sababu katika hii sehemu ya kwetu; ukiangalia huko ndani ndani, utaona ya kwamba Kenya hii yote, yale mananasi matamu yanatoka huko ndani ndani; lakini kwa sababu hii tunaona ya kwamba hakuna usalama wa kutosha. Wale wananchi kule wametoka, na serikali tu inaangalia mambo hivi hivi, kwa hivyo tunaona ya kwamba hali ya uchumi huku inadhorofika, kwa

sababu serikali haitupatii ulinzi wa kutosha. Wakati mwingine serikali inatangaza hali ya hatari; kwa mfano kukiwa na janga fulani, la ukame ama mafuriko, utaona ya kwamba kuna misaada ambayo serikali inatoa kusaidia watu: lakini huku ndani ndani ile misaada hatuipati kwa njia inayofaa. Ukiuliza ni kwa nini? "Nyinyi toeni pesa za mafuta, halafu mletewe ule msaada." Na huyu mtu ni maskini, hana chakula, je, hizi pesa za mafuta atatoa wapi?

Kwa hivyo mimi ningependa serikali inapotambua kuna hali ya hatari na hakuna chakula; basi itoe transport, kama ni malori ya jeshi, yatolewe yapakie kile chakula watu, wapelekewe, ili kuondoa hii hali ya shida.

Pia, kuna hivi vikadi vinavyo tambulisha mwananchi ni raia wa wapi. Kwa mfano, hii kadi ya ID, ama passport. Mimi maoni yangu ni kwamba, hiki kikadi cha kura hiki, pia kiweze kutambulishwa kama kitambulisho halisi, ambacho kinaweza kumtambulisha mwananchi. Kwa sababu utaona ya kwamba wakati mwingine tunahangaishwa na polisi, unampatia ile kadi ya kura, anakwambia hiki si kutambulisho; lakini kina majina kamili, tena kina ID card number. Kwa hivyo kuondoa ule usumbufu, napenda Katiba iweze kutambua hiki kitambulisho cha kupigia kura kama kutambulisho halisi. Wakati mwingine unaweza kuvibeba vyote pamoja, na kwende kutokee hatari pengine kipotee ama ID ipotee, lakini ukiwa na kile kikadi kinaweza kukusaidia.

Vyama vya kisiasa ni vingi sana, vinatatanisha watu. Vinawakilisha masilahi ya mtu binafsi ama viko hali ya kuwakilisha ukabila. Kwa hivyo, ningependa Katiba ipunguze hivi vyama, angalau viwe vyama viwili, ambavyo vitaleta ule mchuano halisi wa kisiasa na kidemokrasia ili kuweza kuondoa hii hali ya wananchi kutatanishwa. Kwa hivyo tunaona ya kwamba leo hii nikama arobaini, vile vyama. Hivi vyama vyote vinatuelekeza wapi? Vinatupoteza hivi vyama. Kwa hivyo kama vitakuwa viwili, ama vitatu, basi utaona ya kwamba siasa zitakomaa lakini sio vyama vingi tu.

Tena napenda hii serikali itenge fuko maalum, kuweza kugharamia hizi shughuli za kampeini. Wakati wa siasa, utaona ya kwamba serikali ndio inanufaika na vile vyombo vya usalama, kama vile magari, radio na T.V. ni hiyo serikali. Lakini vile vyama vya siasa vinawachwa vikihangaika; serikali inafanya jambo ambalo sila kidemokrasia. Kwa hivyo serikali iangalie hivi vyama, vipatiwe ulinzi, pamoja na transport.

Pia, hawa wabunge maalum mimi maoni yangu nasema ya kwamba, waweze kuondolewa; kwa sababu hawa ni watu wamekataliwa, ni vibaraka wa vile vyama. Kwa hivyo waondolewe kabisa, hawa wanakula pesa zetu bure na wamekataliwa. (MAKOFI). Badala yao, mimi ningependa hivi viti, vitengewe wa akina mama, watakao wakilisha akina mama katika bunge, na vijana watakao wakilisha vijana, na welemavu pia, waweze kupewa nafasi katika ile bunge; ili kila jamii, ama kila tabaka, iweze kuwakilishwa vyema katika serikali.

Pia, nataka kusema tusirejelee kosa ambalo lilifanywa na marehemu Ngala. Mwanzo kabisa alipokuwa akifanya kampeini alikuwa na jozi nzuri sana, ya majimbo. Lakini baada ya kushindwa na KANU, akaweza kushawishiwa kwa njia ya urahisi,

akajiunga na KANU, tulipata nini? Tulipoteza, miaka 38 yote ambayo tumepata uhuru, sisi bado ni maskini; sababu gani? Ni kosa lililofanywa na Ngala, ndilo ambalo linatutatiza. Kwa hivyo mimi nasema ya kwamba, tunataka serikali ya majimbo. Jambo la kwanza, hii mikoa iweze kufanywa majimbo na badala ya PC tuwe na Governor. Yule Governor, aruhusiwe kugombea cheo cha uraisi. Na kuwe na bunge ndogo, katika kila jimbo; ambalo litakuwa linaangalia bunge au baraza ndogo katika kila jimbo.

Serikali kuu, central government, ile serikali ya kule Nairobi; isiundwe na kile chama ambacho kimepata wingi wa kura. Nasema ya kwamba, kile chama ambacho kimepata idadi kubwa ya kura; kiwe ndicho ambacho rais atatoka. Lakini hivi vyeo vingine vya uwaziri, vigawanywe, yaani design ya msetu vile. Kwa sababu tukiachia chama kimoja, utaona ya kwamba, kama ni maendeleo ya kiuchumi yana concentrate upande mmoja lakini kule kwingine kunapuuzwa na hii serikali central government. Ikiwa ya mseto wale wengine wa wakilishi wa vyama vya upinzani, watakuwa wana act kama watchdogs, kuangalia ni kasoro gani wale wengine wanafanya. Kwa hivyo tutaondoa hii hali ya corruption.

Wakati wa kupiga kura napendelea uchaguzi wa siri, lakini kuwe na mabadiliko haya. Wakati wa kupiga kura, na kura zinapo maliza kupigwa; zihesabiwe pale. Na wale ambao watahesabu ni wale maofisaa, ambao wanasimamia upigaji kura; pamoja na maofisaa wanaowakilisha wagombea uchaguzi wa viama mbali mbali, pia na maofisaa wa usalama waweze kukaa pamoja wahesabu zile kura halafu wasigu form kila kitu kimalizikie pale hii itaondoa hii hali ya wizi wa kura na ufisadi mwingine. Lakini tukisema hali ya mlolongo, wengine hata wana haya ya kusimama wahesabiwe, mtu kama mimi sitasimama mimi. Ni maoni yangu lakini. (KICHEKO). Pia wakati wa upigaji kura, utaona ya kwamba hizi kura za by-elections, huwa zinafanywa siku za ibada, kwa mfano juma mosi. Na tuna ndugu zetu wanaoabudu siku za jumamosi: ni haki kila mtu raia wa Kenya kupiga kura, lakini utaangalia ni lipi linakuja mwanzo, Mungu ama mwanadamu, of course ni Mungu. Kwa hivyo utakosa kule kupiga kura, lakini utakuwa unasikitika sana, kwa hivyo hizi siku za ibada, iwe ijumaa, jumamosi, ama jumapili zitolewe inje kabisa, zisiwe ni siku za kupiga kura. Siku za kazi ni za kazi kama ni kupiga kura zile siku zingine za wiki sawa sawa lakini siku za ibaada hapana.

Pia oni lingine ni kuhusu umilikaji wa ardhi. Tunaona ya kwamba, mimi sitaki kabisa mgeni atoke huko na pesa zake basi aje anunue ardhi hapa, apatiwe Title Deed, hiyo ni mbaya sana. Kama tutaendelea kuuza hii ardhi yetu wajukuu wetu watakaa wapi? kwa hivyo mtu yeyote ambaye si raia wa wa Kenya, asiruhusiwe kununua ardhi, au kumiliki ardhi; badala yake aweze kukodisha hii ardhi ambapo sisi tutakuwa tunapata faida. Hii mambo ya Mazrui, ati mwambao wa pwani haya mambo yakome mara moja. mazrui ni hio ni warabu wametoka Omani hao! Vipi watatusumbua mpaka leo? Tangu tulipopata uhuru bado tunakaliwa kimawazo na hao watu. Mimi nasema ya kwamba hao Mazrui nikiachiwa mimi nitasema waende kwao. Na hii mambo ya kudai ridha wasida na hata instead watulipe ridhaa, kwa kutumia raslimali zetu kinyume cha sheria. Na kama ni kudai, waende wakadai kule kwao. Kwa hivyo mimi nataka hawa watu kama wanaleta nyoko nyoko, basi waambiwe wende kwao. Watuachie sisi ardhi yetu na umaskini wetu sawa sawa.

Wakati wa uchaguzi wa urais, kuna power vacuum. Ama hakuna uongozi kwa sababu raisi, si rahisi anapiga campaign, yule spika naye, hana mamlaka zaidi, kwa sababu bunge limevunjwa. Mimi nasema ya kwamba kile kipindi kile cha ambapo raisi si raisi huyu jaji mkuu aweze kupatiwa mamlaka ya kuangalia maendeleo ya serikali. Ashikilie serikali mpaka rais atakapochaguliwa. Wakati anapoapishwa na jaji mkuu, jaji mkuu ampatie ufunguo wa kuingia ikulu. Kwa hivyo mimi napendelea kwamba jaji mkuu achukulie kile kipindi kile ambapo rais hayuko.

Jambo lingine, na sema ya kwamba, rais awe chini ya sheria. Akifanya kosa ashtakiwe kama mtu mwingie, na tutaona haya majukumu yake, ama zile kazi zake, ambazo anafanya, ni nyingi sana. Utapata yeye ni mbunge, yeye ni rais, yeye ni vice chancellor, tena amri jeshi. Sasa haya majukumu yote, ayatekelezaje wakati mmoja? Haya majukumu yake yapunguzwe pia tutakuwa tuna, create job opportunities, kiasi cha kuondoa hii hali ya kuwa watu wengine hawana kazi. Kwa hivyo mtu mmoja kazi moja, si mtu moja awe ana kazi nyingi alafu hapa watu tunalia, oh hakuna kazi, na hawa wakubwa ndio kazi zote wanazichukua. Sasa kweli, huo umasikini utaondoka? Hautaweza kuondoka.

Pia hii idara ya kupambana na ufisadi, iwe huru, ipatiwe mamlaka kamili, mtu akipatwa na kosa ashtakiwe: na pia iwe inachaguliwa na bunge, na si raisi. Raisi atachagua vibaraka wake. Bunge lipatiwe jukumu la kuchagua hii idara, ama kikosi cha kupambana na ufisadi. Mimi nasema kwamba ma-sub chief na ma DO waondolewe, kwa sababu imeonekana kwamba haya majukumu yao majukumu yako pamoja na chief yanagongana. Ni kupatanisha watu na kudumisha sheria na utengamano. Lakini leo hii inaonekana ni kama ufisadi tu. Ukienda kwa chief, unaambiwa toa mia sita, kitu ya mzee, tuangalie mambo yako, kama ni mambo ya mashamba unaabiwa, toa mbuzi na mia nne ya kiatu ya mzee. Mambo haya yaleta mgongano, instead, kuwe na wazee wa vijiji. Wachaguliwe na wananchi na, chief achaguliwe na wananchi, halafu kuwe na badala ya DO awe ni DC, halafu juu kuwe ni Govenor; na huko juu kabisa, kuwe ni President. Kwa hivyo, huyo mzee wa kijiji ni mtu ambaye anadharauliwa, wakati mwingi anachukuliwa kama mtu wa kubebe mkoba wa chief, au sub-chief. Aheshimiwe, sababu ndiye yuko karibu na wananchi, na ikiwezekana apatiwe kitu kidogo, kwa kazi yake njema anayoifanya.

Katiba iandikwe kwa lugha ambayo mwananchi wa kawaida ataweza kufanya ni kuelewa barabara. Hii Katiba ya leo ina lugha ngumu ambayo mwanainchi wa kawaida hawezi kuelewa. Kwa hivyo mu iandike na lugha ambayo hata pia mimi nikishika nitaweza kuielewa barabara. Na iwe inachunguzwa mara kwa mara kwa sababu hii Katiba mimi nataka iende na wakati. Wakati kwa mfano, mambo yamekuwa magumu tutaweza kuibadilisha. Lakini si serikali, kama vile Moi alivyofanya ule wakati kabla ya vyama vingi ya kuondoa sheria ya vyama vingi, hakuuliza maoni ya wananchi, waliweza kubadilisha tuu na serikali ikawa chama kimoja ambayo ilikuwa kosa kubwa sana, wananchi walipokuwa wakilia wakawa walishikwa na kutiwa ndani. Kwa hivyo tunataka refendum kama mambo yamekuwa magumu. Maoni ya watu ndiye ambayo inaweza kutuamulia maisha yetu ya baadaye, kwa hivyo ni hayo tu, ahsanteni.

**Com. Abida:** Felix Charo

**Felix Charo:** Jina langu ni Felix Charo Katana, basi mimi ningependa kuzungumzia kwanza juu ya serikali. Tunaona kwamba tuna shida kwa sababu ya serikali moja. Kwa hivyo ningependa serikali iwe serikali ya majimbo, ili kuwe namashindano. Hii italeta manufaa kwa wanainchi. Kwa mfano, kwa upande wa wachezaji tunaona ya kwamba, katika area hii ama sehemu yetu ya Pwani, tuna wachezaji wazuri sana ambao wanaweza kucheza mpira kwa njia ya uzuri kabisa. Lakini sasa tunaona ni watu wa bara, ama sehemu nyingine, ambao wanachukuliwa katika timu ile ya kuwakilisha Kenya yetu. Kwa hivyo ningependa serikali ya Majimbo ili kwamba, waziri mkuu asimamie jimbo lake la Pwani, na yule mwingine asimamie jimbo lake. Ikiwa ni mambo ya kupanga timu ya taifa, iwe katika kila jimbo kutatoka wachezaji, kama ni timu ya kitaifa inahitaji wachezaji thelathini, basi wagawanywe katika ile mikoa minane. Kwa hivyo kila mkoa iwe ina idadi ya watu ambao watatolewa katika mkoa huo, ili kuwe na ushirika kamili.

Pili, ningependa serikali ya majimbo, kwa sababu tunaona ni muda mrefu sana tumekaliwa na watu na hawa wa bara. Raisi ndiye mfisadi mkubwa, kwa sababu vyombo vyote vikija vinapelekwa huko, vinapitia Mombasa ambayo iko sehemu yetu ya Pwani, hiyo ingekuwa inatunufaisha sisi watu wa Pwani. Lakini sasa utakuta vikija ni vipelekwe Nairobi. Vikipelekwa huko watu, wa Nairobi wanapata kwa bei rahisi, watu wa Pwani wananunua kwa bei ya juu. Hiyo inakuwa ni hali mbaya na hali ya kuhuzunisha, na zikifika huko wengine tunashindwa, na hata saa hii tunashindwa kununua baiskeli. Ingekuwa inapatikana hapa ingekuja hapa moja kwa moja, tungekuwa tunanunua kama hata ni 2,000/=. Lakini unalazimika ununue baiskeli kwa shilingi 7,000/=. Kwa hivyo hiyo inakuwa ni vigumu. Kwa hivyo ningependelea serikali ya majimbo ili kwamba kila sehemu iweze kunufaika na mali zile ambazo zinapatikana katika sehemu hiyo.

Pia nikizungumza juu ya mamlaka ya rais, mimi ningeomba ya punguzwe. Katiba hii tunayoipanga sasa ikaweza kupunguza mamlaka ya rais. Akiwa rais ataendelea kuwa jemedari mkuu wa majeshi, aendelee hivyo, lakini mambo ya kuteua mawaziri, wabunge maalum na madiwani maalum, hayo asiingilie hata kidogo. Ikiwa yeye alichaguliwa kwa kura, wanainchi wenyewe wakaweze kukaa na kuchagua watu hao. Pia ikiwezekana rais awe na umri wa miaka 35 hadi 65. Zaidi ya hiyo hawezi kupigania urais, kwa sababu ameingia umri wa uzee na itakuwa ni kuharibu tu.

**Com. Abida:** Hapo umesema 36, rudia hapo,

**Felix:** Umri wa kuanzia 35 hadi 65. Kwa hivyo pia ningependa kwamba yakiwezekana kiti kile cha uraisi, ikiwa tumepanga majimbo, kiti kile cha urais, kikaweze kutembea katika kila mkoa. Uchaguzi huu tukipata rais ametoka katika mkoa wa Pwani, uchaguzi mwingine rais asitoke mkoa ule, ili kuwe na usawa wa kiti, ili kila mtu aweze kunufaika na kiti hicho.

Pia kuna ile sheria ya kusema kwamba raisi yuko juu ya sheria, hiyo inahuzunisha sana. Kwa sababu raisi akiwa juu ya sheria ni kuonyesha kwamba amekalia hayo yote. Basi ikiwa kwa mfano, ni ugonjwa, umeingia katika sehemu hii yetu, pengine ni malaria, na sasa tumechunguza tumeona kwamba tuna ugonjwa wa malaria, na sasa inabidi tupate chanjo ile, itabidi itujumulishe sote. Ikiwa ni mtoto wa miaka miwili ita bidi apate chanjo hiyo, na hata wa miaka thelathini au miaka sitini itabidi chanjo hiyo

aipate. Kwa hivyo ikiwa ni sheria, kila mtu awe chini ya sheria kila mmoja. Yule wa chini hata yule wa juu aweze kutawaliwa na sheria. Na ningeomba kwamba, hata ni rais mwenyewe akipatikana na makosa, aweze kupelekwa kotini moja kwa moja. Na kukiwezekana, aweze kufutwa kabisa; ikiwa ni makosa makubwa ama aweze kufainiwa, ili kupunguza ile hali ya ufisadi.

Pia nikizungumzia juu ya afya, inaonekana sehemu ya Pwani, au sehemu hizi za mashambani zimezorota kiafya. Ni wimbo tu ya kwamba kuna maofisa wa afya, lakini hakuna kazi yoyote inafanyika. Utachunguza ni duka hapa liko, lakini choo chenyewe hakuna, shule iko choo hakuna, sasa wanafanya kazi gani? Ama kazi yao wanaifanyia wapi? Ukienda kwake nyumbani, yule anayejiita kwamba ni afisa wa afya, hakuna hata choo. Sasa utashindwa huyu mtu kazi ana ifanyia wapi? ni kuingia tu ofisini na kwandika karatasi na lulala tu na kungojea mshahara. Kwa hivyo hiyo mambo ningependa Katiba ya sasa ikaweze kuyachunguza sana.

Na mambo ya elimu, pia nikizungumzia juu ya elimu. Ningependa kwamba kuwe na elimu ya bure, kwanzia nursery hadi darasa la nane. Na kule kwingine wazazi wapatiwe msaada kidogo, kuwe na cost sharing. Kwa hivyo hayo mambo yatiliwe maanani, na pia hata kuna wazee ambao wamekomaa hapo jijini, lakini wanastahili ku-elimishwa siku hizi. Kwa hivyo ngumbaro ikaweze kuenea kila mahali, ili kila mtu, hata yule wa chini, akaweze kuinuka, na yule aliyekuwa amelala, akaweza kuinuka.

Pia ningependa kuzungumzia juu ya umilikaji wa ardhi. Ni muda mrefu sana tumesumbuka katika sehemu hii yetu ya Pwani, kwa sababu utakuta kwamba tumepata mashamba, tunalima, lakini tukitaka karatasi, hatupati ni pesa ya kulipa mashamba tunakosa. Tunalipa katika ofisi ya division yetu Marafa hapa, tukiuliza mambo ya title deed, unaambiwa uende Nairobi. Sasa ni ya nini kwenda Nairobi? Ikiwa ni pesa kwa nini tusiende kulipa Nairobi? Kwa hivyo ningeomba ikiwa pesa tutalipa katika Division, basi zile karatasi zinazokwenda ofisi kwa ofisi hadi Nairobi, title deeds itoke huko ofisi kwa ofisi, mpaka Division, ili kila mtu aweze kupata Title Deed kwa njia ya urahisi.

Pia nikizungumzia vile vile juu ya ardhi ama upande wa mashamba ni kwamba: tumekaliwa kwa muda mrefu na hawa watu wa bara. Kulingana na makubaliano ni kwamba, kila aliepata shamba alikuwa ni ajengewe. Awe atajengewa nyumba, na mfereji awekewe, na ikiwezekana kuwe na msaada fulani ambayo atakuwa anapata; ili kujiendeleza, na hatimaye kulipia ile shamba yake. Lakini sasa ukichunguza katika sehemu hii yetu, ni wale wa bara ambao walitoka huko na kuja ili kusimamia kazi hiyo, walichukua mashamba, na wakajiwekea mifereji wenyewe, na sasa hao ikifika wakati wa kulima ni matinga inakuja kwao tu. Mtu wa huku mwenyewe anaweza kuwa anahitaji tinga hilo linalima kwake shambani litakuja liondolewe kabla haijamaliza kazi hiyo, lipelekwe kwa mtu wa bara; kwa sababu yeye yuko na pesa nyingi kushinda yule mwenyeji wa huku.

Kwa hivyo serikali hii ya majimbo ningependa ikaweze kuweka maanani sana mambo haya: ili raia mtu kuitwa raia kamili, awe anatoka katika Kenya hii, na pia awe anatoka katika jimbo lile ambalo anakaa. Ikiwa ni mtu wa bara aweze kwenda kwao na kuangalia mambo ya kwao huko. Mambo ya huku tukaweza kuwachiwa wenyewe. Kwa hivyo mimi ningependa kusisitiza

sehemu hiyo ya kwamba, ikiwa kuna uwezekano, hata wale ambao walipata mashamba kinyume cha sheria; hao tuna wahesabu kuwa ni wezi. Kwa hivyo, wachukuliwe hatua na hatimaye waregeshwa kwao, na wenyeji wamiliki sehemu zile ambazo zinapatikana huku.

Pia nikiingilia hata upande wa uhuru wa raia, tutakuta ya kwamba raia hatuna uhuru wa kutosha. Unaweza kuwa umetoka pengine ni nyumbani, unaelekea dukani, ni usiku, unakutana na askari hapa anakuuliza "unaenda wapi? Haya naingia hapa dukani na nichukue "hapana wewe hebu ngoja," anaanza kukuchakura mifuko na usiku, pengine ameshikilia kipande cha bangi anaweka ndani ya mfuko, anasema huyu nimemshika kwamba anavuta bangi. Sasa unakuta unaanza kusumbuliwa, mpaka ukitoka hapo elfu tano zimekutoka. Hilo ni jambo la kuhuzunisha sana. Kwa hivyo ningependa Katiba ifikirie mambo kama haya, ili kila mtu awe na ule uhuru wa kiraia kama raia wa Kenya. Ahsanteni.

**Com. Abida:** Asante. Mwenda Mwaro, Charo Kitsa, Dama Papa, Rose Jeffa, Zawadi Karisa, Naomi Andrea, Elizabeth Shehe, Nyevu Iha, Bahati Samuel, Baraka Morris, M. N. Katana, Kobe Evans, Lemmy Tuva

**Lemmy Tuva:** Kwa majina naitwa Lemmy Tuva. Mimi niko na maoni yangu na maoni yangu ni ya vijana wa Madina Location. Kwanza tulitoa maoni kuhusu uraia, tukasema ya kwamba raia wa Kenya ni yule yuko na kitambulisho cha taifa. Pili tukasema, kitambulisho kile cha taifa kipewe yule mtoto ambaye amezaliwa na baba na mama ambaye ni mkazi wa Kenya. Halafu pia uraia upewe mtu ambaye ameishi Kenya kwa muda wa miaka tano, au zaidi; bila kupatikana na hatia yoyote. Hii ni kumaanisha kwamba, hii miaka mitano, ni yule mtu pengine ametoka nchi ya ngambo amekuja hapa; pengine anataka pia uraia awe Mkenya. Yule anakaa hapa miaka tano na pia anahakikishwa kabla hajapata; ile miaka mitano hakwenda kando ya sheria. Halafu pia uraia upewe, mtoto ambaye mzazi wake moja ni raia wa Kenya. Pia tukasema ya kwamba, Katiba iruhusu uraia wa nchi mbili. Pengine niko raia wa Kenya halafu pia niko na uraia pengine Tanzania. Kazi pengine Kenya hakuna, naweza kwenda kule nikapata kazi.

Upande wa vyama vya kisiasa, visitekeleze majukumu mengine, mbali na kuhamasisha watu. Pili tukasema Katiba itoe ielekeze uundaji, uongozi, na tabia za vyama vya kisiasa. Hii ina maanisha kwamba, Katiba itoe ule uundaji, uongozi na pia tabia. Kama chama cha kisiasa ni cha kikabila Katiba isiruhusu kisajiliwe. Halafu pia, kuwe na idadi ya vyama vitatu vitakavyosajiliwa, na pia viwe na muundo wa kitaifa. Shuguli za chama zigharamiwe na kodi za wanachama wenyewe.

Tukachambua miundo na aina za serikali. Structures and systems of government. Tukasema Katiba iwe na muundo wa serikali ya Majimbo, ambapo mamlaka ya nchi na bunge, yamegawanywa baina ya serikali kuu na majimbo maalum. Pia uwezo wa mkuu wa wilaya, upewe baraza la wilaya. Hiyo ni kwamba, kama, mamlaka ya ugawaji mashamba, yawe chini ya baraza la wilaya. Hii inamaanisha kwamba, baada ya utoke hapa, uende mpaka Nairobi, pengine uende kutafuta title deed; yule mwenyekiti wa baraza la wilaya, awe pia na jukumu hilo. Awe kwa ofisi yake. Mambo ya ugawaji wa mashamba iwe pia ni kazi yake hapo. Halafu pia, mwenye kiti wa baraza la wilaya, achaguliwe moja kwa moja na wanainchi.

Bunge: umri wa mpigaji kura uwe miaka kumi na tano. Mgombea kiti cha bunge, asiwe na umri maalum. Hii inamaanisha kwamba wewe ni kijana ambaye umesoma vizuri, uko na miaka kwanzia kama kumi na nane na uwongozi unaweza ukapata. Halafu pia mitihani ya bunge iwe ya kiswahili hii language test iwe kiswahili, na kingereza hizi mbili tu.

Katiba ianzishe masharti ya kimaadili ya kitabia yatakayotimizwa na wagombeaji viti vya ubunge. Pengine wataka kugombea kiti cha ubunge lakini umefungwa na sheria, hio tumeonelea kwamba, mtu kama yule awe hawezi akagombea kiti chochote. Halafu wanainchi pia, wawe na haki ya kumrejesha nyumbani mbunge wao. Halafu ya mwisho upande wa bunge, tumeonelea kwamba kushiriki kwa wanawake mbungeni kusiwe na hatua maalum. Hii inamaanisha kwamba mwanamke au mwanaume, anaweza akagombea kiti. Kusiwe na hali ya kwamba kuna hali fulani, ambaye yule mwanamke itamsaidia. Upande wa mamlaka aahh upande wa bunge mwisho kabisa uchaguzi wa bunge ufanywe kwa wakati moja.

Upande wa mamlaka ya nchi. Katiba ifafanue masharti ya kutimizwa na wagombea kiti cha urais. Masharti hayo ni kama, rais mwenyewe awe na wafuasi elfu moja, wanachama kwa kila jimbo. Awe na shahada ya degree, pia tukaonelea kuwe na kipindi maalum; rais aongoze vipindi viwili, vya miaka mitano kila kipindi.

Pia tukaonelea Katiba iweke viwango vya uwezo wa rais. Rais asichague mawaziri mbungeni. Rais asichague majaji wa mahakama kuu. Rais asichague tume ya uchaguzi. Katiba itoe kibali, ili rais aweze kuondolewa mamlakani, kwa kitendo kisicho halali. Kuwe na kifungu fulani cha sheria inayoweza kumtoa, pengine amefanya, amefuja mali ya umma, pale kuwe na kifungu fulani katika Katiba kinachoweza kumtoa yule pale madarakani. Na pia tukaonelea ya kwamba rais awe anajishungulisha kwenye mijadala ya bunge, na asipendelee upande wowote. Tena rais asiwe mbunge, yani awe non-partisan.

Tukaenda upande wa serikali za mitaa. Katiba iruhusu meya na mwenyekiti wa baraza wachaguliwe moja kwa moja na wanainchi. Halafu pia kuwe na vipindi vya miaka mitano, kwa meya, na wenye viti vya baraza. Pia, kuwe na elimu ya chini kwa madiwani kufikia kidato cha nne. Pia mabaraza yafanye kazi, chini ya utawala wa jimbo. Pia kuwe na mitihani ya lugha, inayotosha kwa wagombea viti vya udiwani; lugha ya Kiswahili na ya Kiingereza. Halafu pia kuwe na kuwe na masharti ya kimaadili, na yakitabia kwa wagombea viti vya madiwani. Hii inamaanisha kwamba ukitaka kugombea kiti cha diwani, lakini wewe ushafanya maasi; masharti yatakutoa. Wananchi wawe na haki ya kumrejesha nyumbani diwani wao pia.

**Com. Abida:** Fupisha.

**Lemmy Tuva:** Sawa, haya. Haki za kimsingi. Katiba ifutilie mbali hukumu ya kifo. Katiba ilinde usalama, afya, maji, elimu, makazi, chakula na ajira. Katiba ilinde haki ya wananchi kupata elimu ya lazima, bila malipo, mpaka kidato cha nne. Wakenya wawe na haki ya kupata habari zilizoko mikononi mwa serikali au shirika lolote au tawi la serikali. Katiba ihakikishie wafanyi kazi wote, haki ya uwakilishi katika vyama vya wafanyi kazi. Wanaostaafu wapate haki zao, mara tu wanapostaafu. Serikali

istaafishe wafanyi kazi waliohudumu kwa muda mrefu, badala ya kustaafisha vijana.

Haki za vijana. Katiba ilinde haki za vijana. Mzee anapotaka kuuza mali, ahusishe watoto sio ajiuzie mwenyewe; anauza halafu, wewe hujui kama mali ile imeuzwa; utaanza kuletania shida na yule mtu ambaye ameuziwa, na anahifadhi ile mali. Pia Katiba iruhusu vijana kuoana bila pingamizi ya wazazi. Katiba ifutilie mbali ulipaji wa mahari, instead mtu ambaye ameoa atoe kama shukrani. Ile mali hutatoa, lakini mtu ameridhika, mkewe amemjengea kama nyumba, amenunulia shamba, amemununulia gari, mbali na ile mahari, ni kama unauza kondoo (kicheko).
Katiba izingatie haki za vijana katika uongozi, vijana pia wana haki ya kuongoza. Katiba ipe vijana, haki ya ajira. Na mwisho Katiba idumishe vipawa mbali mbali za vijana, katika kila upande wa michezo na miziki; hii ni ile tuna sema talent. Vijana wengi ni wazuri katika talanta fulani. Lakini sasa inaonekana hakuna mwelekeo wowote wanaopata wale vijana. Mtu utakuwa ni mchezaji mpira, kwa mfano pengine mimi tayari ni mchezaji mpira, hali ile ya kwamba ninakuwa exposed, hakuna kabisa.

Halafu kitu kingine cha mwisho kabisa ningependa kugusia ni kuhusu mali hizi za community. Nikigusia hasa upande wa mnazi. Ule mti wa mnazi ni mti hapa pwani ume nawiri kwa wingi sana. Ule mti una faida nyingi; ule mti una mbao, una makuti, hiyo thatching material, ule mti, unatoa pombe, ile pombe ni kama zile pombe zingine tu, isipokuwa pengine ifanyiwe ukarabati fulani, fulani, iwe pia inaweza ikauzwa katika masoko ya hapa nchini. Asanteni. (makofi)

**Com. Abida:** George Kitsau, Kazungu Kombe, Kaingu Chula, Winfred Msumba, Silas Ziro, Gangira, Philip Mitanze, Kazungu Maingi, Swaleh Chengo, Peter Karisa, Joshua Charo.

**Joshua Charo:** Iwe size yangu, maanake iko juu zaidi ili niweze kutoa maoni yangu. Kwa jina naitwa Joshua Charo Kazungu, ni mkaaji wa Magarini. Ninayo maoni. Na nitajaribu kwa haraka.

**Com. Abida:** Dakika kumi.

**Joshua Charo:** Maanae nataka kukombowa wakati. Kwanza nitazungumzia kuhusu ardhi. Hili ni swala la nyeti, kwa lugha ya kiswahili sahihi. Kwa kweli hapa Pwani tumeonewa. Tumeonewa kabisa, na vyombo vya habari tunasoma kila siku. Mojawao mimi msomi. Ardhi kama serikali tunayolipa kodi, itapotugawiya-na taka hii iwe katika hiyo Katiba tunayounda leo-kwamba iweze kumpa yule mtu iliyemgawia ile ardhi, cheti mara moja, pasipo masharti; maana ndio njia ya kujiendeleza. Mimi ni msomi kwanza ni mtaalam wa kilimo, na nilistaafu, na ndio sababu na sema cheti kipewane mara moja. Maana nani atazidi kuwa maskini, kama ni kweli na haki, ni ile ardhi nimepewa ni muhimu nipewe cheti, niwezeke kumiliki; na niweze kwenda kwa zile financial institutions, nipate mkopo niendeleze lile shamba langu; kwa hivyo ni muhimu hiyo ni moja.

Haya nafikiri nitaenda la pili, nitagusia security, yaani usalama. Katika kikosi cha Kenya Police, na mimi nitataja maana nina uchungu, nilikuwa victim, na sitaki kusema mambo mengi, kiwe restructured kile kikosi; hasa kwa wale wanao tumia nguo za

raia. Un-uniformed policemen, siku moja kanisimamisha sitaki kuendelea; kwa sababu ya kimo changu kifupi, hata mumeona nimerudishwa chini, na waidharau waliona kana kwamba sio mtumishi mwenzi wao; hata ingawaje ni lijitambulisha. Na mimi nasema na uchungu, maana ilikuwa tarehe ishirini na nane, mwezi wa tatu mwaka wa tisaini na nane, nikitoka kazini. Nikasimamishwa pale Mwembe Tayari, na waliposema ni maofisa, hawakutowa zile vitambulisho vyao, ya kwamba wao ni maofisa. Mimi niliwaambia ni mtumishi mwenzenu na nilitoa, lakini mshangao mkubwa wao hawakutoa. Kwa hivyo hao wanaovaa nguo za raia, kama hakuna njia nyingine, Katiba hii iwe na njia sasa. Maana wamenidhulumu mimi. Hata niliandikia yule mkuu wa kikosi cha polisi, the commissioner of police, nilimwadress kabisa, na nilipeana biography yangu, hiyo baura iko huko kwa commissioner, hata commissioner Abongo akitafuta ataipata. Hicho kikosi kiwe restructured, maana hiyo hali yakutoangalia wengine wafupi, wakidhania sisi ni wahalifu, si vizuri. Maana, si vizuri kumwona mtu tu awe basi yoyote mfupi, ni muhalifu (kicheko). Mimi nitasema ukweli, na nina hasira; kiwe restructured, and I repeat myself. I remember that day maana ni masomo pia, nimestaafu, lakini nasema hivi hicho kikosi cha polisi wanao vaa raia, na rudia pale.

**Com. Abida:** Tushaasikia

Asante, nitaendelea upande mwingine sasa. Na nitaongea kuhusu wazee, maana hata mimi ni mzee, sasa mimi nimestaafu. Wazee, ambao wana miaka sitini na tano, na kuendelea, huwa nguvu zao hawana. Hii Katiba tunayoiandika leo, iwafikirie hao wazee; katika nchi zingine za nje wazee hufikiriwa, maana hao ndio wamelipa kodi muda mrefu; na bado wanalipa wanaponunua kiberiti, wanaponunua eeh peremende, wanaponunua chocolate, bado wanalipa kodi. Value added tax, sitasema zaidi ya hayo maana ni msomi. Wafikiriwe hao wazee, kuanzia miaka sitini na tano kuendelea, wasaidiwe na allowance zozote katika nchi yetu hii. Wasaidiwe, maana hawana uwezo tena. Maana kuna wengine ambao hawana watoto wa kuwaangalia. Hiyo ni muhimu kwa wazee. Waangaliwe sana. Wale ambao labda walipata pesa za N.S.S.F. na pengine wametumia imemalizika na hata ambao hawakupata chochote, na wamefikia miaka sitini na tano kuendelea, wasaidiwe katika Katiba hii. Na sasa ni naenda kumalizia maoni yangu hapa. Na nitayasoma ni meorodhesha kwa kizungu na nina kusia pension act. Na poleni nitasoma.

Pension act: hii inastahili kufanyiwa amendments. That an employee, nitasoma kwa Kiingereza, in a government, or local government or parastatals, (government corporations) and in private bodies; in other words those who pay pensions to their employees. An employee, is due for retirement he should be paid his or her dues; within a period of ninety days, and I think that will really help that person; it is avery important thing. (Makofi).

Haya pili, that the office of the director of pensions, should be decentralized to create room for the provincial director of pensions. I think that can really help, because if it comes to majimbo back to where we are, and I like them; if that song can reach everybody, tukisema majimbo, basi ije. Pwani, kila mahali, popote nchini yetu. Tuwe na ofisa, ama director wa pension, ili awe anasaidiana na yule provincial director of pensions. Kuwe na district pensions ofisa. Hapa tu nikienda Malindi, niweze kukutana na ofisa wa pension, anisaidie, nisiwe na haja ya kwenda Nairobi. Mimi nilikaa Nairobi mwezi mmoja na nusu,

nikifukuzana na mambo yangu, na sikuhongana, maana mimi ni mukristo, nimeokoka. Walipotaka niliwaambia, poleni, maana nina haki yangu ninaitafuta (not clear) nataka ikanisaidie. Ndio hapo walijua kwamba huyu mtu hee na kweli, na nililipwa mwenyewe. Kwa hivyo ni vizuri tuwe na hizo ofisi. That the above two offices that is the provincial director of pensions, and the district pension officer, will assist and lessen the work load of the director of pensions in the processing of the retirement benefits especially from the government services and I think that is good. That is my own opinion. Four, that the monthly pension due to the pensioners, these one should be taken seriously, should be paid, and these one is serious, because I am among them, should be paid exactly month end of that particular month in question, and I think that is right. Five, that the monthly pension, I am still on the pension. That the monthly pension should be increased yearly, as it is in the case of the serving civil servants. I think these one is good. Yes. Sasa ilituweze kulipa kodi sawa sawa (not clear) si uwe stagnant pale, elfu mbili basi iwe ni elfu mbili. Kila mwaka ni elfu mbili aah aah. Kila mwezi elfu mbili iongezwe at least kama wale wako pale. Maana sisi pia pale tulipo pia, bado tunalipa kodi, tunaihudumia taifa. Hayo ndio machache, au mengi niliyokuwa nayo jioni ya leo. Asanteni sana. (Makofi)

**Com. Abida:** Hilda Chome, Paul Nyoka, James Kirimu

**James Kirimu:** Natoa shukrani kwako Bibi mwenyekiti. Jina langu ni James Kirimu Menza. Niko na maoni machache, nikiwakilisha kata ya Adu. Katiba yetu ya Kenya, instahili kuwa na utangulizi. Na huu ndio utangulizi unaofaa au unaostahili katika Katiba yetu ya Kenya. Jamhuri ya Kenya itakuwa Jamhuri ya kidemokrasia halisi, nayo italinda haki za kibinadamu, ardhi, na mali za watu. Itahakikisha haki na usawa unadumu kwa kila Mkenya. Itaangalia masilahi ya wananchi wote, hasa wanyonge wa mali na wasiojiweza pia. Itafanya juhudi kuinua maisha ya wananchi wote kiuchumi. Itaatazingatia mila na utamaduni za Wakenya wote. Haitapendelea nchi yoyote wakati wamafarakano, lakini utajiunga na nchi zingine za ulimwengu, katika harakati za kuleta maendeleo na ushirika kwa jumla.

Bibi mwenyekiti, wananchi wote wa Kenya, watafurahia kufuata Katiba ya Kenya, na kuilinda pia. Tunasema, Mwenyezi Mungu aisaidie Kenya. Kanuni za kuongoza sera ya dola, kanuni za kuongoza state policy. Bibi mwenyekiti, Wakenya wanahitaji kanuni za kuongoza serikali, au nchi ya Kenya, ili kuhudumia wananchi kwa haki na ukweli. Serikali ya Kenya itakuwa na jukumu kama ifuatavyo. Itainua masilahi ya wananchi kiuchumi, kisiasa, kitangamano, na kihaki, katika nyanja zote za maisha. Itapunguza unyonge wa mapato, kuondoa ile hali ya kutokuwa sawa kimadaraka, na kinafasi kwa wananchiwote wakiwa nyumbani, na kazini pia. Kutambua kua wananchi wote wa Kenya, wake kwa waume, wana haki ya kujitafutia maisha, yaani wana haki ya kujichumia. Kuhakikisha kwamba, mali ya umma inatumiwa vilivyo, kunufaisha wananchi wenyewe, walioko katika mazingira hayo. Na kuona kwamba shughuli za kuichumi hazitategemea utajiri na uzalishaji pekee. Bibi mwenye kiti nitaendelea. Kuhakikisha kwamba, watu wote, wake kwa waume, wanapata mishahara kulingana na haki zao. Kutambua vile vile, afya na nguvu, za wafanyi kazi wote wa Kenya, wake kwa waume. Na kuhakikisha kwamba wananchi wa Kenya, pamoja na watoto, hawalazimiki kufanya kazi kinyume cha umri wao, afya na nguvu kwa sababu ya hali ya kiuchumi. Kuhakikisha pia, kwamba wanapewa nafasi na vifaaa, ili wajiendeleze sawasawa wakiwa na uhuru wa kujivunia. Kutambua kwamba, wanainch

wana haki ya kufanya kazi, kupata elimu na kuhakikisha kwamba usaidizi fulani unatolewa kwa wale wanaokosa kuajiriwa kwa wazee, wasiojiweza, na wengine wenye mahitaji.

Bibi mwenyekit, inastahili pia, itambulikane kwamba, tunastahili kuwa na uhuru wa kuabudu kwa wananchi wote wa Kenya.

Ukuu wa Katiba: bibi mwenyekit, inastahili kufahamika kwamba jukumu ya kuunda Katiba lina gharama kubwa, kwa hivyo, Katiba ni chombo muhimu, katika maisha ya Mkenya. Isiwe rahisi kuibadilisha. Pia vile vile, iwapo kuna umuhimu wa kubadilisha au kurekebisha sehemu ya Katiba hiyo. Basi wanainchi wajulishwe kwanza, na kuhusishwa pia. Wabunge wawe na uwezo wa kubadili Katiba, lakini kwa wingi wa asilimia tisaini ya kura zote. Hii nikuonyesha kwamba, kusiwe na urahisi wa kubadilisha Katiba iliyochukua muda, na gharama, kuitengeneza.

Bibi mwenyekiti, kuna sehemu nyingine za Katiba ambazo, hasistahili kabisa kurekebishwa, au kubadilishwa. Sehemu, kwa mfano, kama demokrasia, haistahili kubadilishwa. Demokrasia na idumu milele. Haistahili pia vile vile kugeuza haki za kibinadam, haki za kibinadam ziko pale milele. Na haistahili pia kubadilisha haki za changamano. Ukiniruhusu bibi mwenyekiti, nitaendelea katika sehemu za haki za watoto.

Mengi yamezungumuzwa, lakini kwa sababu nawakilisha ile kata ya Adu, hata kama nitakuwa narudiarudia, itanibidi nifanye hivyo. Haki za watoto. Inastahili kila mtoto wa kike au wa kiume, asomeshwe. Utanisamea nikisemehe hata, kama mtoto amepata bahati mbaya akapata mimba shuleni, ailee mimba ile, akazae, arudi darasani, aendelee na masomo. Bibi mwenyekiti, elimu inastahili kuwa ya bure, kwa hivyo ni iwe ya bure, na iwe ni ya lazima. Kila mtoto mzaliwa wa nchi yetu ya Kenya; alazimike kwenda shule. Ndio maana tunasema, elimu iwe ya bure. Na hata hivyo, shule nyingi ziko mbali mbali, shule ziwe karibu na watoto, wasipate taabu, kutembea maili nyingi kutafuta shule, kutaingia uvivu hapo, na shida nyingine. Kufanya mtoto akose kusoma, elimu ni ya lazima.

Bibi mwenyekiti kwa sababu elimu tunasema iwe ya bure, hata shule zijengwe na serikali. Serikali ni kubwa ina nafasi ya kutafuta uwezo wa kujenga mashule, kama zamani, Bibi mwenyekiti, elimu inastahili kuwa ya bure, kutoka shule za malezi, hata kila chuo kikuu. Mtoto asibahatike kusoma, akiwa na akili ya juu, akasoma mpaka darasa la nane, kwa hali ya kielimu ya bure; halafu akiwa ni aende shule ya upili, kwa sababu ya kusoma nafasi, abaki nyumbani. Akiwa ni wakati wa yeye kwenda chuo kikuu, abaki nyumbani, kwa sababu ya kukosa nafasi, hapana. Elimu na iwe ya bure kutoka shule za malezi, “nursery school”, mpaka chuo kikuu.

Watoto wawe na uhuru wa kuzungumza pia. Si kama yeye anataka kutoa maoni yake unasema “wewe umezaliwa juzi, huna haki ya kutoa maoni, hapa ni kwa wazee”.  Watoto wawe na uhuru wa kuzungumza. Bibi mwenyekiti, mzazi ampatie mtoto wake malezi meema. Umemzaa mtoto, bila shaka ulipanga. Mpatie mtoto yule malezi meema.

Mtoto ana haki ya kupata uridhi kutoka kwa mzazi wake. Ningetaka bibi mwenyekiti, pia vile vile, kwamba Katiba itilie maanani, mambo ya kuajiriwa watoto. Mtoto asiajiriwe kazi akiwa chini ya umri wa miaka kumi na minane. Utakuta ukienda huko miji mikubwa, kuna watoto wanafanya kazi: kuuza barafu, kuuza peremende, na kadhalika, wakiwa na umri mdogo kabisa. Hiyo ikataliwe, watoto wasome (bang, bang). Hiyo ni kuniondoa au ni kufanya nini Bi mwenyekiti.

**Com. Abida**: Saa mbaya.

Bibi mwenyekiti hata kama saa ni mbaya, ninataka kugusia mambo fulani yaliozungumuzwa kuhusu mila, na tamaduni za Kiafrika. Nataka niguzie mambo ya ndoa. Bibi mwenyekiti, ni haki kabisa katika hali za ndoa kuwa na mali. Mali ni sawa zilipwe, mali zinaimarisha ndoa, na ni haki kabisa. Bibi mwenyekiti, mambo ya malu, sisi hapa kwetu kuna mpango wa malu. Malu ni sawasawa itolewe, na mama asitishwe akasema ikiwa mimi nimekosea utachukua malu, na wewe pia umenikosea nitachukua malu kutoka kwa bibi mwenzangu. Hapana. Na ifahamike kabisa Bibi mwenyekiti, kwamba, katika hawa watu wawili, baba na mama waliooana moja alienda kwa mwingine kumtafuta, na yule alieyenda kumtafuta, ni huyu baba. Na mama akakubali, na baba akatoa mahari. Kwa hivyo baba ana haki ya kuwa na uchungu na malu yake. Kwa hivyo ikiwa mama amekosea, ameshikwa na bwana mwingine, baba niajituze kwa kupata makosa, na Bibi mwenyekiti, haya makosa haingekuwa ya kiwango fulani. Makosa haya Bibi mwenyekiti, yangekuwa kulingana na vile baba aliyekosewa, vile anavyotaka mwenyewe. Akiwa anataka shilingi elfu hamsini apewe; kwa sababu yule amevunja nyumba ya mtu.

Bibi mwenyekiti namaliza hapo, kuhusu ndoa. Ningetaka Katiba itilie maanani sana, haki na tamaduni za Kiafrika, hasa kwa mambo haya ya ndoa. Bibi mwenyekiti, mama akikubaliana na baba, akikubali kuolewa, ni afahamu kwamba, kule nyumbani watakako kwenda, Bibi mwenyekiti; lazima afahamu kwamba yeye atakua sasa chini ya yule bwana wake. Kwa hivyo kuna maana kwamba akiwa chini ya bwana wake, bwana pale ndiye kichwa, na kwa hivyo anastahili kumuheshimu. Mambo mengi ni sawa kushauriana, lakini mambo mengine mama ni aseme afande. (makofi). Kuna mambo mengine Bibi mwenyekiti, ambayo yanastahili kuzingatiwa. Baba na mama, tunasema baba pale, ndiye kichwa pale nyumbani. Bibi mwenyekiti kule shule ukimchapa mtoto hustahili, kama ni mwalimu, hustahili kuona mtoto naye kwa hasira zake anakurudishia na kukuchapa, hiyo itakuwa ni vita, na huwa nidhamu pale haiwekeki sawa sawa. Ukimchapa mtoto Bibi mwenyekiti, hata kama mtoto anawashwa, ana haki ya kuvumilia. Hata nyumbani Bibi mwenyekiti, ikiwa baba amekasirishwa kwa mambo fulani, hayo hutokea, ikiwa wewe umekasirika, Bibi mwenyekiti, kuwe na haki ya kumwonyesha kidogo mama, kwamba amemkosea, hata kama ni kwa kumchapa kidogo (makofi). Na Bibi mwenyekiti, akimchapa, tamaduni, sheria, na tamaduni za Kiafrika zinasema; hata kama mama yule anawashwa, hastahili kurudisha, na kumchapa bwana. Akifanya hivyo ni vita hivyo; na bwana anaweza kuingiwa na ghadhabu na kupiga na kumuumiza mama. Tafadhali mama avumilie, aombe msamaha yaishie pale. Asante Bibi mwenye kiti (kicheko na makofi).

**Com Abida**: Samuel Bashora.

**Samuel**: Haya, mimi kwa majina naitwa Samuel Bashora. Mimi natoka Adu, na nimekuja hapa kutoa maoni kwa tume ya Katiba ya Kenya. Nataka kuanza na ajenda ya ardhi. Ardhi imezungumziwa sana hapa, na wtu wengi, lakini ni sawasawa kuongeza kwa sababu, ziko katika ajenda zetu kule, katika makao yetu kule ambako tumezungumzia mambo ya Katiba. Ardhi ni kitu kizuri sana ambacho ni makao ya mtu na ni chakula cha binadamu, na ni uridhi wa wa binadamu, na serikali yetu iko na sheria nyingi sana kuhusu mambo ya ardhi.

Lakini kusema kweli katika huu, mkoa wetu, tuseme sijui mikoa mingine, ardhi haifai watu. Tuna ardhi hapa ambazo tumegawanyiwa vizuri sana. Tupatiwe title deeds, na mtu awe na access huko Malindi Commercial Bank, au kwa A.F.C. uende ukapate chochote, angalau ulime. Lakini haiwezekani kabisa, tumepata haya mashamba, lakini mashamba haitoi title deed, tunaambiwa tulipie tena, wamelipa wengi, na ma-title deed hakuna. Na ukiangalia sasa huwezi kujivunia hiyo ardhi, na huwezi kuiendeleza, huwezi kujenga nyumba ya kudumu, kwa sababu wewe pale, huna hakika kwamba ni yako. Kwa hivyo, sisi mimi kwa maoni yangu, na maoni ya kule nakotoka; ni kwamba mamlaka hayo ya mashamba ambayo yanatekelezwa kule Ardhi House, yagawanywe (makofi). Commissioner of Lands ambaye anakaa Nairobi, tunataka awe ceremonial commissioner, lakini ma-commissioner wa kushugulika na mambo ya ardhi ya wananchi wakae mikoani (makofi). Na wawe na full power ya ku process mambo ya ardhi, Mpaka mtu apate title deed yake akiwa Mombasa, akiwa Nakuru, akiwa popote, lakini siyo Nairobi.Kwa sababu pale Nairobi pana dhiki. Tunasikia kwamba kuna ma-ofisi kumi na sita ya kupitia pale, kable ya title deed kuwa processed. Nafikiri hizo sheria, hata ni za kikoloni kabisa. Kwa sababu kama ni haki, na yule anayepewa title deed ni mwananchi wa Kenya; kuna process ndefu namna ile ya kutoka wapi? Si ingelikuwa inakuwa processed na kujulikana, huyu definitely ni mtu wa hapa, na hata kama amenunua shamba hio ni yake, title deed apewe, ili tuwe na maendeleo. Kwa hivyo sisi, kwa ardhi zetu za hapa Magharini, ama katika sehemu hizi za mikoa, hatuna maendeleo kabisa kwa sababu, haturuhusiwi kupata title deed.

Tunashangazwa kusikia kwamba huko Athi House, kuna title deeds zimelala huko na wananchi hawataki kuchukua, kivipi? Kwa sababu sisi hatujapelekewa title deeds tukakataa, hatujaambiwa kwamba ziko mahali fulani tukakataa. Kwa hivyo tunataka mamlaka ya mashamba, hii Katiba yetu mpya igawanywe ilete mikoani, kwa sababu hata tukienda kule Nairobi, tunaona watu wa Pwani, watu wa Kakamega huko, watu Nyanza wote wanahangaika kule Nairobi. Ni kwa sababu madaraka yana mtu mmoja. Na yangawanywe yale madaraka angaa iwe mikoani ili hata kama tutataabika twende kwa headquarter zetu.

Nakitu kingine ni kuhusu malipo ya mashamba, hasa upande wa Magarini. Zamani ilikuwa shillingi elfu mia tisa na hamsini, na hivi imegeuka imekuwa shillingi elfu saba, na elfu sabini na tano, sasa wale wakulima ambao wana hizi pesa, ni akina nani? Hizi chache tu, hatuwezi, tukalipa hizi nyingi? Kwa hivyo zile pesa zile nyingi Katiba mpya nai scrap (makofi) kwa sababu hizi ardhi ni za wananchi. Si kwamba ni ardhi za kununua. Serikali haikunua ardhi hapa, ispokuwa ina demacate kwa watu ambao wana ardhi zao tayari. Kwa nini sasa sisi tunapata hizi pingamizi mradi tu, title deed hupati? Hukulipa shillingi elfu sabini na tano, kwa hivyo hupati, na hata kama umelipa zile; mimi nimelipa mwaka wa sabini na tisa, sijapata hata barua ile ambayo inatangulia title deed. Sasa ule uchumi tunauua au tuna uzidisha? (makofi).

Ajenda nyingine ya pili ni mamlaka ya nchi. Sisi tunataka sana hii mamlaka iwe mahali pamoja, na hiyo ni vizuri sana. Lakini tunaona mamlaka ya liyoko headquarters Nairobi; na wale wanaokaa katika mikoa, wanapata taabu sana; kwa sababu, watu wa kule wakiona watu wakitoka kwa mikoa, mtu ana haja kwa ofisi ya ardhi, an haja kwa ofisi ya elimu, ana haja kwa ofisi ya pension, hachukuliwi kama ndugu yake, anachukuliwa tu kama huyu ni mtu mnyama. Wewe umepoteza tikiti, na Nairobi hujui mtu, kisha ukifika pale unahangaika, hata ni kama kwamba wewe huko katika nchi yako. Hii tume yetu, angalieni sana kwa sababu watu wanalilia majimbo kwa sababu ya shida, ambazo zimezidi sana. Hata barua yenyewe siku hizi uki-communicate na Nairobi, wengine hawajibu kabisa. Wewe utaandika barua uangushe tu, na inaenda kwa ofisi za serikali, lakini no response. Utafanyaaje? Mpaka uende, na kule nako kuna shida, hakuna pesa, utaendaje? Kwa hivyo haya mamlaka ambayo yako kule, kama ya lands, hii ya pension, hii ya mambo ya elimu, mambo kadha, wa kadha yale ambayo yanahusu mwananchi wa kawaida. Tafadhali Katiba yetu na iruhusu hayo madaraka yateremshwe mikoani, katika ofisi ya P.C. Hata kama ni kwenda kulala Mombasa, inajua hapo nina majamaa naweza ni kalala, ni karibu; lakini Nairobi. Kisha kule kuna majambazi wengi, saa zote marisasi (makofi na kicheko) hata huenda ukauwawa na stray bullet kule. Kwa sababu unatafuta haki yako tu namna hii. Hii imezidi sana, kwa hivyo tunaomba hizi mamlaka ziteremshwe. Kule katika ile kamati yetu kule tumezungumzia kwamba, tusiwe na serikali ya majimbo. Kule tumesema hivyo kwa sababu pengine iko ghali na inaweza ikaleta hata mvurugano, kutoelewana huku na kule. Lakini yale mamlaka makubwa, makubwa, yarudishwe kwa ma-province. Kisha hao wanaokalia yale mamlaka, ikiwa itawezekana, kuwe na special appointments kwamba wawe wananchi wa mkoa huo: maana atakuwa na uchungu na pale kwake. Pesa zinatoka nyingi kutoka Nairobi, lakini zingine haziwafikii hawa. Kwa hivyo akapitisha kwamba kama inawezekana, yale mamlaka yajaribu kusawazishwa vizuri ili yanufaishe hata wananchi wa mikoa hiyo. Si kwamba hapa peke yake, lakini sehemu mbali mbali.

Uchumi. Uchumi tumesema, umezorota sana. Hivi sasa katika tume yetu, nawambia haki kabisa, pesa, kuona pesa, ni kitu cha ajaabu sana katika Kenya ya leo. Kazi hakuna, mvua hainyeshi, watu ni wakulima sana, lakini hakuna mazao, kwa sababu hakuna mvua. Kwa hivyo irrigation schemes zijaribiwe kutiwa maanani. Ili tukiwa hatuna mvua ya Mungu, tupate irrigation ya serikali. Na hiki kilimo chenye kusema ukweli, hata ndicho kimeinua hata wale walioendelea sana katika zile developed countries zote. Wametumia zile natural resources, zao na wakatajirika vibaya sana, na wamekua watu wanaitwa industrialized countries, rich countries. Ni kwa sababu serikali zao zimetumia resource zilizoko hapo, na wamefaidika; hata kifedha, na wananchi wametajirika, na serikali imetajirika. Kwa hivyo mashamba yetu yanongezewe irrigation, vile viwanda vifunguliwe. Tuna viwanda hapa Pwani, sijui huko sehemu zingine, lakini mkoa wetu hapa tuna viwanda kama vile vya Bixa, tuna viwanda kama vile vya korosho, tuna viwanda kama vile vya pamba, pamba yenyewe ilikuwa ni cash-crop, hapa. Hata wazazi wetu walikuwa wakiuza pamba, kwa musimu wa mwisho wa mwaka, na kupata pesa za kununulia nguo za Christmas. Leo hakuna kitu kama hicho. Pamba itangazwe kabisa, kama zamani ilivyokuwa katika serikali zile za mkoloni. Alikua anaweka cinema na kutangaza manufaa ya pamba, na wananchi walipanda pamba sana.

Na viwanda vifunguliwe, na vile vilivyoko viajiri watu kirasmi. Hapa tuna viwanda vingi sana vya chumvi. Viwanda hivi basi ni

casual labour peke yake, lakini haviajiri watu vile unavyo ona ni sawa sawa. Kwa hivyo uajiri, kuwe na kufuata zile njia za kanuni ili hizi kampuni zifaidi wananchi. Ma-hoteli yote yafufuliwe, kwa sababu mahoteli along the coast yalikuwa inaleta pesa. Tuna watoto wamesoma hawana kazi, wakizunguka, wanazunguka, wanakuja hawana kazi. Tubunishe nafasi za kazi, ili shida hizi ziondoke, na katika kilimo vile vile kwa sababu ndio uti wa mgongo tungestahili tupateat least agricultural institutes kwa wingi; at least Magarini Settlement Scheme tumejengewa hizo wananchi wa waelimishwe mambo ya kulima. Tusilaumiwe tu kwamba,hatujui kulima na hatusomeshwi, na tusomeshwe tujuwe kulima,kilomo cha kisa. Na vitu kama ma-ractor na majembe ya ng'ombe, kuwe na assistance. Hizi Ministry of Agriculture, zi siwe tu, zakunguka mashambani. lakini kuwe na technical assistance, kutoka kwa wizara. Maana ina jukumu yakuhakikisha wananchi wanalima kwa njia nzuri. Mambo yauchumi nimemaliza.

Nimekuja mambo ya mahakama. Mahakama yetu tunalumiwa sisi ma-chief, na ma-asistant chief, kwa sababu ya kula rushwa na pesa nyingi ambazo si za kawaida. Mimi naona ya kwamba, kuna upungufu fulani ulifanyika. Wakati wa mkoloni, alijua kwamba, hii mambo ya mahakama; kuna mengi ambayo ni local; ya kienyeji, ambayo inastahili mahakama ya kipekee. Kwa hivyo wakaanzisha sub-ordinate courts katika sehemu za mashambani. Vile kama hapa Marafa ilikuwako, Ganda ilikuwako. Katiba mpya na irudishe hii mahakama, ili chief, ama assistance chief, asiwe na kazi yoyote kuhusu mambo ya local cases. Local cases ambazo zinaabatana na customary law ziende kwa sub-ordinate courts, zile ambazo ni za kienyeji ili zisikizwe pale. Yule presidng judge pale, si lazima awe ni yule graduate wa university, lakini hata akawa mzee wa ki-giriama, yule anajua mila za kienyeji, yeye anaweza kuongoza hii mambo za malu, na mambo za mila za ndoa, na uridhi wa kikabila; anaweza kuendesha hiyo. Lakini mahakama zetu zinazidi sana, kwa sababu ya kuchelewesha hata civil cases, zinachukua muda mrefu. Mtu amekasirika mpaka ame lose hope, anelewana na yule mtu amemshtaki, na gharama zimeenda. Na gharama za korti zimekuwa nyingi sana. Hivi mwananchi wa kawaida hawezi ku-sue, kwa sababu zimekua nyingi sana, na pesa hakuna. Kwa hivyo zipunguzwe. Na murder cases, zinakuwa delayed sana katika high court, na hii inafanya hata kunaongezeka la mauaji kabisa. Watu kuuana kwa sababu mtu anaona kwamba hata mtu akiua, hawezi kuhukumiwa. Anaenda kuwekwa kwa remand na anakaa tu. Kuna cases mingi sana ambazo zina karibu miaka mitatu, miine, mitano. Ya nini basi na sisi tunalinda usalama wa wananchi? Yataka hizi murder cases zichukuliwe very serious, kwa sababu, ukifanya hivyo wewe judge, unalinda yule ambaye yuko kule shambani. Lakini ukiwa very loose, na mambo ya kuona tu kwamba hii ni kawaida, na ku-acquit mara moja, sasa umesema watu waende wakauane. Kwa hivyo mahakama yetu iongezee jitihada. Kama korti hazitoshi na ziongezwe. Lakini, murder cases, na zile serious cases, ziwe resolved mapema, ili wananchi wawe very confident, kwa sababu najua, mtu akinifanyia hivi atashtakiwa, atafungwa. Na kuna wengine wamesema mambo ya msaada wa mahakama, kama vile haya mambo ya advocate, kwa watu wasio na kitu, ni kweli. Wakati mtu ana kesi, na kama yeye hana kitu, kuwe na special, najua iko, lakini sasa iongezwe kabisa; kuwe na msaada kwa mambo ya mahakama. Yaani mshtakiwa asaidiwe.

**Com. Abida:** Tafadhali, fupisha muda wako umekwisha.

**Bashora:** Haya, kitu cha mwisho nataka kusema ya kwamba, mahakama yetu mpya, ambayo tunaiunda sasa, iangalie haki ya

makabila madogo. Kuna makabila ambao wako ndani ndani na wao hawana kwao, na hawana representation katika parliament na katika local authorities. Kwa hivyo, wajaribu kupewa makao, na mimi ni mmoja wao. Tupewe makao ili tujivunie kwamba nasi kwetu ni mahali fulani, na sisi tujivunie kwamba tuna machifu, tuna MP, tuna local authority, wale nominated members ambao mmesema ya kwamba ni wengi sana, wafutwe ama wapunguzwe; lakini na wapewe wale ambao ni kama sisi ambao kabila zetu ni ndogo. Tuwe represented, ili wawe representatives wa wale minority tribes katika nchi.

**Com. Abida:** Kabla hujaondoka, tungetaka utuambie hizo minority tribes ni zipi hapa? sehemu hii. Kabila lako ni lipi?

**Mzee:** Hapa Coast, hapa nafikiro ni sisi tu.

**Com. Abida:** Nyinyi ni kabila gani?

**Mzee:** Sisi twaitwa Wata tribe.

**Com. Abida:** Wata tribe … mwapatikana wapi?

**Mzee:** Twapatikana hapa around Magarini.

**Com. Abida:** Asante, Asante mzee.

**Mzee:** Nilikuwa nataka kuongeza kitu kingine nimalizie.

**Com. Abida:** Saa zimekwisha mzee, nusu dakika peke yake umalizie.

**Mzee:** Nusu dakika!! Ilikuwa ni mambo ya pension. Pension mimi nime retire, kwa hivyo sasa ni pension. Mambo ya pension katika sis watumishi wa serikali, tuna aibu sana. Mtu anapostaafu mara moja, hapewi pesa zake anawekwa karibu miaka miwili mizima. Hivi mimi nime retire ni chifu na hata family inaenda kwa kibarua ina choma makaa, inaiba kwa sababu hatuna chakula, hatuna nguo, hatuna chochote.

Hii process ya pension inatuabisha sana sisi upande wa administration, sisi tunafaa tukiwa tuna retire, immediately tupewe zile pesa, ili mtu aende akajisaidie mwenyewe.

**Audience:** (CLAPPING)

**Mzee:** Hatukuweka pesa kwa sababu ya mambo mengi. Ikiwa chifu wewe unatafutwa harambee nyingi, ikiwa wewe ni chifu

unasomesha watoto, nilisomesha wote, watoto wangu, na sikuweka hata ndururu katika bank. Nawezaje? nitakula nini? kama nimetoka katika kazi. Hivi sasa, we are hata imekuwa nikama. Na wengi wamepata hypertension kwa sababu ya kukosa pesa. Na wanakufa kabisa kabla mtu hajapata pesa zake za pension, kwa sababu ya delay inayofanyika Nairobi.

Na ndiyo sababu tunasema, ikiwa mambo ya majimbo, mnaona kwamba ni vigumu, hii mamlaka makubwa, makubwa tafadhali Katiba yetu na ilete.

**Com. Abida:** Asante.

**Mzee:** Katika mikoa.

**Com. Abida:** Asante.

**Mzee:** Otherwise we are dying kabisa (laughter and clapping)

**Com. Abida:** Sasa waliobakia tutawapa dakika tano tano ili tusimuache mtu yeyote bila kuzungumza; na tunaona list ni kubwa, na lazima tufunge kazi saa kumi na moja. Samuel …. Ha … Samuel amezungumza, Katana Mwambire, Katana Mwambire, yuko? Rev. Justin M. Mramba, yuko wapi? Justin Muramba.

**Rev. Mramba:** Majina ni Justin Masha Mramba. Mimi mzaliwa wa hapa. Yangu ni mafupi sana, na nataka kuyafanya mafupi zaidi. La kwanza, ni kwamba machifu, ninaomba wachaguliwe, kama vile wabunge wanavyochaguliwa na raia wenyewe. La pili, wasichana wakiolewa, au wasichana wanapofika umri wao wa kuolewa na kuenda kwa mume; lakini huyu mzazi, yaani huyu msichana awe na uridhi kutoka kwa babake mazazi, kwa sababu mara nyingi, wanapoolewa na kuenda, mara wanazoroteka huko, au wanakosana na waume zao, wanarudi pale. Kwa hivyo naomba iikiwezekana katika Katiba yetu ambayo tunaendelea kuitengeza, wapate, uridhi hawa wasichana. Na tena wakiolewa, wakikosana na waume zao, wakirudi nyumbani kwao, ile mali, maoni huenda ikawa wamepata watoto wawili, watatu. Wakirudi nyumbani, huyu bwana na huyu mama, ikiwezekana, hawa watoto wagawanywe. Yule naye apate asiwe kama hakufanya lolote. Na tena hata ikiwezekana, ile mali ambayo mvulana alitoa, desturi ya kimila ya kimijikenda hapa, hata akiwa hawenganya, lakini ile mali ni lazima airudishe kule. Naomba kwamba, hii mali asiirudishe. Najua ni sumu, lakini ni hivyo, (laughter).

Umilikaji wa ardhi, kuwe na urahisi wa wale ambao wanahusika, kutoa vyeti vya wale ambao, wamepewa ardhi uwe karibu ili kila mwananchi aliyepata shamba, ikiwezekana apate title deed haraka iwezekanavyo. (clapping). Tena, huu ulipaji wa hizi pesa, kama nilivyosikia mwenzangu akitaja, zisiwe nyingi namna hiyo ikiwezekana. Tunajua ni gharama, lakini isiwe shillingi elfu sabini! Hii,sijui nikunyanganywa mashamba ni kufanywaje.

Tafadhali ifikiriwe sana kwa katiba mpya hii: ili mwananchi aweze kupata shamba na hata ikiwa si kwamba asilipe kabisa-lakini ni nyingi mno. Jambo lingine la nne, shule ikiwezekana kutoka standard one mpaka standard eight, ikiwezekana, iwe ya bure. Jambo la tano, raia wawe na uwezo wa kumfuta mbunge wao, na diwani wao, wawe na uwezo. La sita ambalo ni la mwisho, nataka ikiwezekana serikali iwe ni ya majimbo. Asante. (clapping).

**Com. Abida**: Jonathan M. Yao.

**Jonathan**: Asante. Kwa majina naitwa Jonathan Mure Yao. Ninawakilisha maoni ambayo yanatoka katika makanisa mawili, ya sehemu za huku Singwaya na Dakacha Seventh Day Adventist Church. Kabla, sijasema yale yalipendekezwa kwenu. Ningependa kusema kwamba, mimi binanfsi ninaheshimu uhuru wa yeyote kulingana na imani yaki pahali alipo. Maoni haya yako katika sehemu tano kuna, utangulizi, halafu mwisho kuna kufunga.

Tunaomba kwamba, Katiba ambayo tunaendelea kuunda, ni kwa kwamba, mamlaka ni Mungu mwenyewe ndiye ambaye anayatoa. Na serikali yote, ni Mungu ndiye ambaye ameiweka hapo. Na uhuru wa kuabudu, ni Mungu ambaye anatoa, si mwanadamu, kwa hivyo mtu akiamua kuabudu siku yoyote anataka, aruhusiwe, Katiba hiyo iangalie. Kwa sababu nawakilisha Kanisa hili la Seventh Day Adventist Church, nataka kuwe na uhuru wa kuabudu, siku yao ambayo ni siku ya Jumamosi. Kwa lugha yetu ni masaa ishirini na manne, kuanzia Ijumaa jioni, jua kutwa hadi Jumamosi, jua kutwa. Tunataka kuangalia katika uhuru wa kuabudu, hasa katika nyanja za kuajiriwa. Katika parastatals za serikali na hata private sector, wale ambao ni wa imani hii ya Seventh Day Adventist Church, ya kwamba; waweze kuruhusiwa kwenda kwa ibada siku yao ya kuabudu bila masharti.

Jambo lingine, kumekuwa na cases ya kwamba watu wanayimwa uajiri kwa sababu ya imani zao, basi hao wasabato pia wameweza kupatiwa na hayo. Kusiwe na kunyimwa, kwa sababu mtu anaheshimu siku yake ya kuabudu.

Jambo lingine ni uhuru wa kuabudu katika mashule, ama nyanja zozote za mashule ya kiserikali, ya kwamba wote ambao ni washiriki wa kanisa hili. Waweze kuruhusiwa kuabudu siku yao. Wasilazimishwe kuenda kwa mitihani, wasilazimishwe kuenda kwa darasa, wasilazimishwe ku participate katika games, na functions zingine, siku ile yao ambao ndiyo Sabato, siku ya Jumamosi.

Jambo lingine ni uhuru wa kuabudu katika public functions. Katika mikutano ya hadhara. Harambees, na public barazas, na uchaguzi, wale ambao ni wa imani hii waweze kutegewa siku zao, kwa ajili ya kuweza kupiga kura. Nataka kuzungumza kitu hapa, tulipoteza kesi, kanisa nzima la Wasabato Kenya hii, ile by-election ambayo ilifanyika kule Taveta, kwa sababu, constitution au Katiba ya Kenya kweli iko uhuru wa kuabudu, lakini haijazingatia kujali uhuru wa mtu binafsi. Kwa hivyo tafadhali, elections zinapofanyika, basi zisifanywe katika siku hii ya Sabato, na public barazas, na harambee hizo, ili nao hawa waweze kuchangia, kwa sababu ni wananchi wa Kenya.

Kuna public holidays, naomba kwamba ikiwezekana, kama zinaanguukia siku ya Jumamosi, basi, kwa wale ambao ni wa Sabato, jumatatu inayofuata, wasiende kazi, iweze kuwa yao ya kupumzika.

Mwisho, kwa kamati hii ambayo ni ya Katiba, ningependa muangalie Katiba za nchi zingine, ili muweze kujua zaidi, vile ambayo serikali zinajali thehebu hili la watu wa Jumamosi. Ningeomba muweze kuendea katika constitution ya nchi zinazofuata, Italy, Colombia na Poland. Wao, serikali na bunge imeweza kuweka sheria maalum; ambazo zinaangalia watu amabo wanaenda kanisani; siku ya Jumamosi.

Na mwisho mungu awabariki, sababu nu jukumu kubwa ambalo mnaendelea kulifanya. Bwana awabariki.

**Com. Abida**: Ahsante, Shadrack Kenga – Dakika tano. (Not clear)

**Com. Abida**: Ahsante, nashukuru.

**Shadrack:** Ni shukrani kubwa, jina langu mimi naitwa Shadrack Kalu Kenga, kama vile mlivyosikia, siku ya leo, ni kwamba, tumetangaziwa ya kwamba tutakuja kubadilisha Katiba ya Kenya; ambayo ni serikali mpya. Kwa hivyo ni shukrani kubwa nyinyi viongozi, ambao mmejitolea kwenu, kwamba tunaenda mpaka Marafa tusikize vile watu wanataka Katiba igeuzwe. Kwa hivyo mmefanya vizuri sana, na Mungu awabariki.

Mimi na wenzangu ndio tuliwaanzia, kura zile za mwanzo. Mwanzo alikuwa Ngala na Kenyatta ndio waliopiga kura, na wakati huo kulikuwa hakuna vitambulisho, ni kodi tu pekee yake. Mtu ambaye ana cheti cha kodi ndiye anaenda kwa kura.

Mimi nilikuwa na miaka mitatu wakati huo. Kwa hivyo tumeenda tukapiga kura, kutokea hapo tunapiga kura mpaka sasa. Kila mbunge tukumpigia kura huku kwetu, haimalizi miaka mitano.

Kwa hivyo sisi, tunang'ang'ana nao wabunge, akitoka huyu twasema hakutosha, hakutengeza ya kutosha, tunamtoa, huyu naye hakutengeneza nafasi yakutosha, tunamtoa, kwa hivyo wabunge wamekuwa sasa ni kama miaka mitano tunamtoa tayari kwa sababu hatoshi. Na ni kubwa na wale hawawezi kuitekeleza vizuri, hawaiwezi, Kwa hivyo mimi langu binafsi, oni langu la kutia ndani ya Katiba, mwandike vizuri sana. Tungetaka sisi tuongezewe mbunge mmoja huku kwetu, kama chain of D.O. Marafa yuko, na Gongoni yuko. D.O. wa Gongoni awe na mbunge wake na wa Marafa naye awe na mbunge wake. Na ninazungumza kwa hivi, siku moja huyu mbunge tuliye naye hapa kombr amejaribu kwamba "hii nchi nitaimaliza, kwa nini wenzangu hawakuimaliza? Mimi nitaimaliza" Ameweka mkutano huko, akaweka hapa, akapumzika akaenda Chabari, akaenda Hadu, alipofika barabarani amechoka ana njaa, gari likapinduka, ikaua mtu hapo hapo. Na kama ni uongo watu watasema ni uongo. Siku hiyo imekuwa hivyo, lakini tukathibitisha kabisa sisi wazee ya kwamba, hii nchi ni kubwa, mbunge mmoja hawezi.

Kwa hivyo tunataka sisi, Katiba hii ya zamani kama ilikuwa huyo mbunge mmoja anatosha; lakini hii mpya ambayo tunabadilisha tunataka tuongezwe mbunge mmoja huku kwetu. Kama huko juu nao watafanya hivyo, nataka waseme hivyo nao. Tunataka sote kila location moja iwekwe mbunge, location ya D.O. moja, iwekwe mbunge, location ya D.O. moja, iwekwe mbunge. Sasa haswa kabisa akitembea hii nchi aweze kuimaliza, nasi tupumzike wazee. Tumechoka kupiga kura na wabunge hawatoshi, nchi hawaimalizi kwa hivyo tumechoka, hata wengine wanasema "mimi sitaenda kwa kura kabisa". Kwa sababu hata nikienda mbunge sitamwona, nikimpigia, basi ameenda vimekwisha. Hiyo ndiyo ambayo tumeafikia na sisi wazee, nii hii nchi kwamba ni kubwa mno.

Tunataka tuongezewe wabunge, kwa DO kuwe na mbunge, mpaka wamalize, mkimaliza hivyo sisi wazee tutapumzika, kabla hivyo tutapiga kura kila siku, na kutoa wabunge mpaka mwisho. Sina zaidi mimi langu ilikuwa hilo moja tu peke yake, asanteni sana

**Crowd:** Clapping and Laughter.

**Com. Abida:** Asante mzee. Solomon Kimwandoro, Hezron Mbayo, Immanuel Ihatoyo, Peter Ziro, Daniel Mwendwa, Chengo Kazungu, Chengo Kazungu, Fondo Kalama, Baya Charo Baya

**Baya Charo:** (Speaks fast in mother tongue)

**Com. Abida:** Ngoja basi (laughter),

**Baya:** Mimi nafunga

**Com. Abida:** Kuna mama, kwanza ngonja.

**Translator for Baya:** Kwa majina naitwa Baya Charo, Katiba hii nataka iwe serikali ya majimbo. Wazee wa kijiji wa kazi kubwa sana. Wazee wa kijiji vile wana kazi nyingi, itabidi walipwe mishahara. Chifu na masub-chief wapigwe kura na wananchi.

Chief na awe mtu mzima, maanake yeye ndiye anayejua mambo na anaweza kutupatia mwongozo mzuri.

**Crowd:** KABISA (Laughter)

**Baya:** Asante sana.

**Com. Abida:** Rosemary Wekesa, Rosemary Wekesa (INTERJECTIONS)

**Rosemary:** Ni mimi, vile mmesikia ni mimi.

**Com. Abida:** Wewe ni nani?

**Rosemary:** Naitwa Rosemary Wekesa. Mimi vile msikiavyo wanasema kwamba watu wa bara, ndio ni mimi sasa mmoja wao. Tuseme kwamba kwa mfano, mtu amechukuliwa kama hapa coast, mtu amechukua wewe ni msichana, amekupenda, mmefika huko nyumbani wazazi wake hawakupendi, na wewe una mimba tayari. Tuseme kwa mfano umezaa tayari, mtoto unaye, haya amekuambia kwamba "mimi sitaki watu wa bara, wabara ni wagirenge". Wewe tayari una mtoto wake, ama may be wawili mmoja, tuseme kwa mfano wewe, huyo mtoto utampeleka wapi? Utamwonyesha babake ni nani?

Tuseme kwa mfano; si atakuwa chokora au mwizi? Wewe utakuwa huna idi, mfano huna kazi, ama ulikuwa una kazi, akakuharibia maisha yako, na wewe sasa. hakukutolea mali, lakini mmeketi naye, kama kuanzia miaka kadha, kuanzia naye, amekuharibia maisha yako! Tuseme mtu kama huyo unaweza kumfanya nini?

(INTERJECTIONS) Mwache.

**Rosemary:** Mimi kweli nina shida kweli, mtu amenichukua nikiwa msichana, nilikuwa mtu na kazi zangu akanipenda kweli, tukasikizana, akasema wewe ndiye bibi sasa kufika kwao nyumbani, wakasema hawanitaki, na mimi sasa tayari nina watoto. Nimekaa naye kuanzia mwaka tisaini na sita, mpaka hadi sasa nina watoto wawili. Hivi sasa, hata hana haja na mimi, nikifika, kule hata hanishughulikii, yeye ndiye baba … hata nashindwa kama itakuwaje?

Najua kujiepusha mtoto asiwe chokora au mwizi, ni muhimu tena ataniuliza namtaka baba, nitamfanyaje? Ama nao wanapenda asiwe na baba? Si ni sawa, mtoto anapenda awe na babake na mama. Pale alipo naye anajua nina babangu. Lakini sasa nimeambiwa mimi, watoto ni wako kupandisia kimila. Mimi niko na uchungu sana, sasa nimeshindwa, kama pengine ile serikali ingine inakuja, pengine itasaidia sijui? Sikuwa mimi nasema, pengine itatokea kwa wengine. Mimi tayari nimeharibiwa maisha kweli. Mtu kama huyu utampeleka. Wewe kwenyu ni mbali, unaambiwa nyinyi ni watu wa firenge. Wagerenge! Sasa nitafanya nini? Watoto nimezaa naye, na watoto ni wake, baba ni yeye, nitawaonyesha baba gani tena?

**Com. Abida:** Anafanya kazi yeye?

**Rosemary:** Niwa County Council.

**Com. Abida:** Mwone Bwana D.O. D.O., see what you can do for her, please.

**Rosemary:** Naambiwea mimi nimepewa na watoto, kufuatilia mila sijui kutoa tembo, anasema sikutoa tembo na mimi nimekaa naye kuanzia tisaini na sita.

**Unknown:** Shida ni kwamba, mtoto anakataliwa kwa sababu hujalipa mahari,

**Rosemary:** Hakutoa mali, tena ameniharibia maisha yangu kuanzia wakati huu. Amechukua bibi mwingine naambiwa mimi mgirenge, basi niondoke, mkabila. Nikifika pale sijui pesa zinatoka ananisumbua sana, ananitatiza sana, nafukuzwa pahali pale ndani ya nyumba. Nifukuzwe nitafute pahali pa kulala baba yao yuko, mtoto akimwambia baba nasikia njaa, "ulizeni mama yenu". Nitafanya nini mtu kama mimi baba yao ndio huyu. Yeye yuko Gongoni kule pale kwa chumvi, naninaambiwe (interjection).

**Rosemary:** Ameenda kwa mkubwa wa soko. Nimeenda nikaambiwa kwa kiwao kama hakutoa mali, hakuna pakwetu utampeleka. (Interjection) not clear.

**Rosemary:** Sasa yeye amechukua mwingine, juzi nimeenda ananipeleka peleka hivi, nayeye ndiye baba yao.(Interjection) Pale kwa chumvi pale ukitoka … hii ya Gongoni pale (not clear) sasa nikienda pale ananisumbua sumbua. Mimi niwakwanza tena wa pili ameondoka, nikaambiwa sina uwezo wakupeleka popote sababu sikutolewa mali, nimgirenge mimi, watoto ni wako nimekupa wewe sikutolewa tembo. Nitamfanya nini, mimi sina kazi, nitawalisha nini watoto? Watoto wanajua kwamba baba ni huyu, si watakua waizi ama chokora? (interjection) ameniharibia maisha.

**Com. Abida:** Wale watu wako hapa tungependa kuwashukuru sana, kwa vile mlijitokeza katika mkutano wa leo, na kabla hatujafunga mkutano, tungeomba Reverend ikiwa yuko atufungie mkutano kwa sala. Ikiwa Revelend hayuko, ajitokeze mzee yeyote. Nafikiri kuna mzee hapo, huyu wa pension, ambaye atatufungia kwa sala. (NOT CLEAR).

**Com. Abida:** Na ikiwa kuna mtu ambaye ana memorandum, nakala ambayo ameandika, si lazima kuzungumza, waweze kuileta hapa, ukaipeana kwa maafisa hawa wa tume. Ahsanteni.

**Mzee wa pension:** Ahsanteni, na tusimameni sote na tumuheshimu mungu. (BACKGROUND NOT CLEAR)
Natuombe, asante Mwenyezi Mungu, kwa rehema zako, umetufadhili kutoka asubuhi mpaka kutufikisha jioni ya leo. Umekuwa pamoja nasi sote, waliofika mahali hapa, sawa natulivyo kuomba, ulipata kutuongoza katika hali hizo zote, tukitarajia kubadilishwa kwa Katiba ya nchi yetu ya Kenya.

Tunashukuru kwa nafasi hiyo, ambayo ilipeanwa kwa kila mmoja wetu. Naamini Bwana ndiwe, uliyekuwa kiongozi. Na sasa

tunarudisha ama mkutano huu mikononi mwako, maana umepata kutuongoza. Naamini wakati tutakapo kumbukana, utapata kuwalinda, makamishna wetu wote, waliotutembelea hapa, katika vyombo watakavyo safiria tunajua vimeundwa na wanadamu upate kuwalinda. Upate kutulinda nasi pia, tutakapoondoka, tuondoke katika amani yako. Ni katika jina la Yesu Kristo, Bwana na Mwokozi wetu, nimeomba na kuamini, AMEN.

Meeting ended at 5.30 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&